JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

RIPOTI YA JUMLA YA UKAGUZI WA UFANISI NA MAALUM KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 MWEZI MACHI 2015

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Machi 2015

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Dira
Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi zaUmma

Dhamiri
Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha Uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma Katika kutoa huduma zenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

Uadilifu
Sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo

Ubora
Sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi

Uaminifu
Tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.

Mtazamo wa watu
Tunatazama na kukazia zaidi katika matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye ari ya kazi.

Uvumbuzi
Sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi

Matumizi bora ya rasilimali
sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za umma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Mtaa wa Samora, S.L.P 9080,
Dar es Salaam Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: 255(022)2115157/8,
Nukushi: 255(022)2117527,
Barua Pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Tafadhali unapojibu taja
Kumbukumbu**Na.FA.27/249/01/2013/2014** 26 Machi, 2015

Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
1 Barabara ya Barack Obama,
11400 Dar es salaam.

Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa tatu (3) za Ukaguzi wa Ufanisi na Taarifa za Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa Miaka ya Nyuma toka kwenye Ripoti Tano za Ukaguzi wa Ufanisi

Kwa mujibu wa ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano waTanzania (iliyorekebishwa 2005) na kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti yangu ya sita ya Ukaguzi wa Ufanisi na maalum kwa kipindi kinachoishia Machi, 2015.

Taarifa hii inajumuisha taarifa tatu za Ukaguzi wa Ufanisi na taarifa za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye taarifa tano za Ukaguzi wa Ufanisi ambazo ziliwasilishwa Bungeni miaka iliyopita ambazo zinahusu Serikali kuu na Serikali za mitaa. Taarifa hii inategemewa kuwasilishwa Bungeni mnamo mwezi Aprili 2015.

Nawasilisha.

Prof. Mussa Juma Assad
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

YALIYOMO

SHUKRANI xv

MUHTASARI xvi

SURA YA KWANZA 1

UTANGULIZI 1

1.1 Usuli wa Ukaguzi 1

1.2 Mamlaka ya Kukagua 1

1.3 Madhumuni ya Ripoti 2

1.4 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu 3

1.5 Muundo wa Ripoti 3

SURA YA PILI 4

MAELEZO MAFUPI YA KAGUZI ZILIZOFANYIKA NA UFUATILIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAGUZI 4

2.1 Utangulizi 4

2.2 Usimamizi wa Mipango Miji nchini 4

SURA YA TATU 12

MAPUNGUFU YANAYOJIRUDIA KATIKA UTENDAJI WA SERIKALI KAMA YALIVYOAINISHWA KATIKA KAGUZI ZA UFANISI 12

3.1 Utangulizi 12

3.2 Mipango Isiyotosheleza ili kutimiza malengo husika 12

SURA YA NNE 38

4.2.1 Mapendekezo Yaliyotekelezwa kikamilifu 45

4.3 Hitimisho na Matarajio 48

4.3.1 Mapendekezo Kwa Halmashauri ya Mji wa Babati 48

Mapendekezo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa 49

Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa inapaswa: 49

SURA YA TANO 51

KUFUALIA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU UTOAJI WA HUDUMA YA AFYA YA MSINGI 51

5.1 Usuli wa Ukaguzi......51

5.2 Hali ya Ujumla ya Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa......51

5.3 Utekelezaji wa Pendekezo Moja moja......53

5.4 Hitimisho na Matarajio......59

SURA YA SITA......62

KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU PROGRAMU YA UKAGUZI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA......62

6.1 Usuli wa Ukaguzi......62

6.2 Utekelezaji wa Mapendekezo......63

6.3 Hitimisho na Matarajio......69

SURA YA SABA......70

KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU USIMAMIZI NA UDHIBITI WA TAKA NGUMU KWENYE MIJI MIKUU NA MIKOA NCHINI......70

7.1 Usuli wa Ukaguzi......70

7.2 Utekelezaji wa Jumla wa mapendekezo yaliyotolewa......71

7.3 Hitimisho na Matarajio......87

SURA YA NANE......88

KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA UFANISI WA USIMAMIZI WA UJENZI WA BARABARA NCHINI......88

8.1 Usuli wa Ukaguzi......88

8.2 Hali ya Ujumla ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa......88

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho cha kwanza: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Kuzuia na Kukabiliana na Mafuriko	99
Kiambatanisho cha pili: Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa katika Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Afya ya Msingi ya Jamii Tanzania	111
Kiambatanisho cha tatu: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Programu ya Ukaguzi kwa Shule za Sekondari Tanzania	125
Kiambatanisho cha nne: Hali ya utekelezaji ya mapendekezo ya ukaguzi katika usimamizi wa taka ngumu katika Miji mikuu na Mikoa	130
Kiambatanisho cha tano: Hali ya utekelezaji wa Mapendekezo Ukaguzi wa Kifanisi Kuhusiana na Usimamizi wa Ujenzi wa Barabara Tanzania	153

ORODHA YA VIFUPISHO

CDA	**Mamlaka ya Undelezaji wa Mji wa Dodoma**
CHMT	**Council Health Management Team**
LGAs	**Serikali za Mitaa**
MoHSW	**Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii**
MTEF	**Medium Term Expenditure Framework**
MTUHA	**Health Management Information System**
NEMC	**Baraza la Usimamizi wa Mazingira**
RAS	**Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa**
TAMISEMI	**Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
ULGSP	**Urban Local Government Strengthening Program**

ORODHA YA MAJEDWALI

		Ukurasa
Jedwali 2.1:	Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi	10
Jedwali 2.2:	Idadi ya Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa	11
Jedwali 3.1:	Uzingatiaji Hatua za ukarabati majengo katika Mikoa kama ilivyoainishwa katika muongozo wa ukarabati wa Majengo	13
Jedwali 3.2:	Ukarabati uliopangwa na ambao Haukupangwa (2010/11 hadi 2012/13)	15
Jedwali 3.3:	Tathmini na hali za majengo zilinazotakiwa na idadi halisi ya tafiti hali zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2012/2013.	16
Jedwali 3.4:	Mipango inayoandaliwa katika ngazi ya mikoa kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa shughuli za ukarabati wa majengo	17
Jedwali 3.5:	Uwasilishaji wa ripoti za Makisio ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwenda ofisi za Bohari Kuu ya Madawa Kanda kwa kipindi cha miaka mitatu ya fedha 2010-2013	19
Jedwali 3.6:	Mlinganisho wa manunuzi sambamba na makisio yake kwa madawa 15 kwa miaka 2010-2013	20
Jedwali 3.7:	Mauzo yaliyofanyika kulinganisha na Makisio yake kwa dawa 15 za katika miaka mitatu ya fedha (2010/11-2012/13)	21
Jedwali 3.8:	Hali ya Upelekaji wa Maagizo kwenda katika vituo vya Afya kutoka katika kanda tano zilizotembelewa 2012/2013	26
Jedwali 3.9:	Kiasi cha bajeti kinachotengwa (Matumizi tarajiwa) kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya serikali	32
Jedwali 4.1:	Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi kwa taasisi mojamoja zilizokaguliwa	40
Jedwali 4.2:	Idadi ya mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa kila kundi	42

Jedwali 5.1:	Idadi ya mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa kila kundi	54
Jedwali 6.1:	Idadai ya Mapendekezo Yasiyotekelezwa kwa Mgawanyo	65
Jedwali 7.1:	Idadi ya Mapendekezo yasiyotekelezwa kwa makundi	79
Jedwali 8.1:	Idadi ya mapendekezo yasiyotekelezwa kwa kila kundi	92

ORODHA YA VIELELEZO

		Ukurasa
Kielelezo 3.1:	**Idadi ya oda za mahitaji na kiwango halisi cha oda zilizofanywa na kanda kwenda Bohari Kuu ya dawa Makao makuu (2011/2012-2012/2013)**	**………22**
Kielelezo 3.2:	**Mlinganisho kati ya muda rasmi wa kuandaa na kusafirisha oda za dawa na muda halisi uliotumika kuandaa na kusafirisha oda hizo kutoka Bohari Kuu kwenda Bohari za Kanda**	**………23**
Kielelezo 3.3:	**Mlinganisho kati ya muda wa kuandaa na kupeleka oda za dawa kati ya Bohari Kuu na Bohari za Kanda (2010-2013)**	**………24**
Kielelezo 3.4:	**Uwiano wa idadi ya oda kulingana na muda uliochukua kuandaliwa na kupelekwa kutoka Bohari Kuu kwenda Bohari za Kanda**	**………25**
Kielelezo 3.5 :	**Mwenendo wa ruzuku ya Serikali kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya serikali kwa miaka ya fedha 2006/2007 hadi 2013/2014**	**………33**
Kielelezo 3.6:	**Kiwango cha fedha zinazotolewa katika kila mkupuo kutoka Wizara ya Afya katika mwaka 2012/13 kwa manunuzi ya dawa na vifaa tiba muhimu**	**………34**
Kielelezo 3.7:	**Mtaji wa Biashara wa MSD dhidi ya Deni la Serikali**	**………35**
Kielelezo 4.1:	**Utekelezaji wa jumla wa mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi**	**………39**
Kielelezo 5.1:	**Asilimia ya Utekelezwaji wa Mapendekezo yaliyotolewa kwa Wakaguliwa Wakuu (TAMISEMI na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii)**	**………52**
Kielelezo 5.2:	**Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwa Ngazi ya Wizara,Tawala za Mikoa na Halmashauri**	**………53**
Kielelezo 6.1:	**Utekelezaji wa Ujumla wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Kifanisi wa Usimamizi wa Ukaguzi katika Shule za Sekondari Tanzania**	**………64**
Kielelezo 7.1:	**Utekelezaji wa Jumla wa Majumuisho ya Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Usimamizi wa Taka Ngumu kwenye Miji Tanzania**	**………72**

Kielelezo 7.2:	**Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwa Ngazi ya Taifa na Halmashauri**	**………73**
Kielelezo 8.1:	**Utekelezaji wa Mapendekezo 20 yaliyotolewa kwa Wizara ya Ujenzi na TANROADS**	**………90**

DIBAJI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti yangu ya sita ya jumla ya ukaguzi wa ufanisi na maalum. Ripoti hii ya jumla inahusiana na taarifa tatu za ukaguzi wa Ufanisi kwa serikali kuu (Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa). Vilevile ninapendakuwasilisha taarifa za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa miaka ya nyuma kwenye ripoti tano za ukaguzi wa ufanisi ambazo zilihusisha serikali kuu na serikali za mitaa.

Ripoti hii inalenga kutoa taarifa kwa ufupi kwa wadau (wabunge, maafisa wa serikali kuu na Serikali za mitaa, wanahabari, wafadhili,asasi za kijamii na zisizo za kiserikali kuhusiana na matokeo ya ukaguzi yaliyopo kwenye ripoti za ukaguzi wa ufanisi na maalum zilizofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali mpaka kufikia Mwezi Machi 2015. Ufafanuzi wa kina kuhusiana na taarifa zilizoandikwa kwa kifupi unapatikana kwenye ripoti husika ya ukaguzi ambayo ilikabidhiwa kwa katibu mkuu wa wizara husika.

Ripoti hii imekabidhiwa kwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa mujibu wa ibara 143 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Kifungu 34 (1) na (2) cha sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008.

Chini ya Ibara 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya1977 kama inavyorekebishwa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu waHesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila taarifa aliyotoa kufuatana na Ibara ndogo (2) ya Ibara iliyotajwa. Mara taarifa hiyo inapopokelewa, Rais atamwelekeza waziri husika kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge kabla ya siku sabakupita toka kikao cha kwanza cha Bunge kuanza. Ibara hiyohiyo inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake kwa Spika wa Bunge iwapo Rais kwa sababu zozote zile atashindwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa Spika kama sheria inavyotaka.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya Mwaka 2008 kumeimarisha uhuru wa utendaji kazi wa ofisi yangu katika kutimiza majukumu yake ya kikatiba. Haya ni matokeo ya juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge letu Tukufu.Uhuru wa kufanya kazi kwa ofisi yangu pamoja na uwepo wa rasilimali watu na fedhaambavyo vitaniwezesha kufanya kazi yangu bila kuingiliwa na mamlakayoyote zikiwemo zile ninazo kagua.

Sheria hii imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kunipa mamlakaya kufanyakaguzi za ufanisi, utambuzi, mazingira na maalum mbali ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha.

Kimsingi, taarifa hii imeniwezesha kutoa maoni huru kwa Bunge kuhusiana na matumizi sahihi na uwajibikaji, uwazi na uadilifu

katikamatumizi ya rasilimali za umma kwenye maeneo ya usimamizi wa Mipango miji, Usimamizi wa makisio na usambazaji wa dawa na vifaa tiba muhimu na Usimamizi wa ukarabati wa majengo ya Serikali

Vile vile, nimeweza kutoa matokeo ya mapendekezo yaliyotolewa kwa ripoti tano za ukaguzi wa ufanisi za miaka ya nyuma kwenye maeneo ya Usimamizi wa Udhibiti wa athari za Mafuriko kwa Serikali kuu, Mikoa na Serikali za Mitaa uliofanyika kwa kutumia mafuriko yaliyowahi kutokea Babati (2007); Usimamizi wa Utoaji wa Huduma ya Afya ya Msingi, ukaguzi uliofanyika kwenye vituo vya afya (2009); Programu za Ukaguzi wa Shule za Sekondari nchini (2009); Usimamizi wa Udhibiti wa Taka Ngumu nchini na Usimamizi wa Ujenzi wa barabara (2010).

Lengo kuu la kufanya kaguzi hizi ilikuwa ni kuangalia kama rasilimali zilizotengwa zimetumika kwa ufanisi kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge kwenye maeneo yaliyotajwa.

Ni vizuri kufahamu kwamba wakati ofisi yangu inafanya ukaguzi na kutoa taarifa ya utendaji wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma kulingana na sheria na taratibu zilizopo, ni wajibu wa Maafisa masuuli kuhakikishamapendekezo niliyoyatoa yanatekelezwa kikamilifu.

Ni matarajio ya Bunge kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ataandaa taarifa za fedha kuhusu usimamizi wa rasilimali za umma katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya umma kuhusiana na tija na ufanisi kwenye utekelezaji waprogramu mbalimbali za Serikali. Ofisi yangu inachangia kwa kutoa mapendekezo ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma. Kwa jinsi hiyo, Serikali kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Ofisi yangu kwa pamoja zina mchango mkubwa wa kutoa kwa Bunge katika kujenga imani kwa Umma katika usimamizi wa rasilimali za umma. Ingawa majukumu yanatofautiana, matarajio ya usimamizi bora kwa rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya wabunge na Umma kwa ujumla, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya mapitio ya njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta ya Umma. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga na kuyapa kipaumbele maeneomuhimu yanayochangia maendeleo ya sekta ya umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa rasilimali za umma, tunaendelea kujadili masuala yanayoathiri utawala/uongozi katika sekta ya umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa fedha na masuala ya utawala bora.

Napenda kutambua mchango wa wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa juhudi kubwa walizofanya katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi na mishaharaduni na wakati mwingine kufanya kazi kwenye maeneo yasiyofikikakirahisi.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kutokana na jukumu lake la usimamizi wa rasilimali za Umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo nitafurahi kupata mapendekezo ya jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu hii kwa siku zijazo.

Prof. Mussa Juma Assad
Mdhibiti Na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Dar es Salaam.
26 Machi, 2015

SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kutimiza wajibu wangu wa Kikatiba wa kutoa taarifa hii ya ukaguzi wa ufanisi na maalum. Napenda kumshukuru kila mfanyakazi katika ofisi yangu kwa jitihada zao ambazo zimeniwezesha kutimiza matakwa ya katiba ya kutoa ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi. Nalazimika kuishukuru familia yangu na familia za wafanyakazi katika Ofisi yangu kwa uvumilivu wao walioonyesha wakati wakipindi chote cha uandaaji wa taarifa hii.

Napenda kuishukuru Serikali na Bunge letu Tukufu kwa kuendelea kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

Vile vile, shukrani za pekee ziende kwa wafadhili hasa Ofisi yaTaifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO), Serikali ya Sweden kupitia Wakala wa Kimataifa wa Maendeleo wa Sweden (SIDA), Serikali ya Ujerumani kupitia GIZ, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa la Marekani (USAID),Idara yaMaendeleo ya Kimataifa (DFID), Benki ya Dunia kupitia mradi wa "the Public Financial Management Reform Programme (PFMRP)" na wote waliotutakia mema ambao walichangia kwa njia moja au nyingine kwa nia ya kuleta mabadiliko katika ofisi yangu. Mchango wao katika kuendelezauwezo wa wafanyakazi kiujuzi, kimfumo wa teknologia ya mawasiliano na nyenzo mbalimbali vimechangia kwa kiasi kikubwa kufikia malengo tuliyojiwekea.

Hali kadhalika, ninapenda kuwashukuru wadau wengine wote ikiwa ni pamoja na maafisa Masuuli wa Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, Ujenzi,Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakala wa Majengo Tanzania na Bohari Kuu ya Madawa kwa ushirikiano walioutoa na kutupatia taarifa muhimu zilizohitajika wakati wa uandaaji wa ripoti za ukaguzi ambazo ni chanzo cha ripoti hii ya ujumla.

Shukrani za kipekee ziende kwa jamii ya wanataaluma na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka Vyuo vikuu vya Dar es Salaam,Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Ardhi, wataalamu wa kujitegemea na maafisa wastaafu wa serikali kwa michango yao ambayo iliboresha ripoti za ukaguzi wa ufanisi kupitia ukosoaji na uhakiki walioufanya katika rasimu za ripoti hizo.

Napenda pia kuishukuru Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC) ambayo ripoti hii pamoja na ripoti binafsi zitafikishwa kwa ajili ya uchunguzi, majadiliano na kutoa maelezo yake.

Mwisho, napenda kuwashukuru Maafisa Masuuli wote na watumishi wote wa Umma katika Tanzania nzima, bila kusahau mchango wa walipa kodi ambao ripoti hii tunaitoa kwao. Mwenyezi Mungu awabariki wote kama mnavyojitoa katika kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma nchini.

MUHTASARI

Ukaguzi wa Ufanisi unalenga kuboresha uwajibikaji na ufanisi wa taasisi za umma. Pia unatoa tathmini ya msingi na madhubuti kuhusiana na namna ambavyo taasisi zilizokaguliwa zinatumia rasilimali katika kutimiza majukumu yao kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Kifungu namba 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi wa Ufanisi.

Ripoti hii ya jumla inaainisha mapungufu yaliyobainika, hitimisho na mapendekezo kwa ripoti zote tatu za ukaguzi zilizofanyika kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ambazo zinahusiana na Usimamizi wa mipango miji, Usimamizi wa makisio na usambazaji wa dawa na vifaa tiba muhimu na Usimamizi wa Ukarabati wa majengo ya Serikali. Pia inatoa taarifa za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwenye ripoti tano za ukaguzi wa ufanisi ambazo ziliwasilishwa Bungeni katika kipindi cha mwaka 2007 mpaka 2010. Ripoti hizo ni za: Usimamizi wa Udhibiti wa Athari za Mafuriko kwa Serikali kuu, Mikoa na Serikali za Mitaa uliofanyika kwa kutathmini mafuriko yaliyotokea Babati (2007); Usimamizi wa Utoaji wa Huduma ya Afya ya Msingi, ukaguzi uliofanyika kwenye Vituo vya afya (2009); Programuza Ukaguzi wa Shule za Sekondari nchini Tanzania (2009); Usimamizi wa Udhibiti wa Taka Ngumu Nchini (2009) na Usimamizi wa Ujenzi wa Bara bara (2010).

Kwa ujumla ripoti hii ina lengo la kuwasaidia wabunge, serikali, vyombo vya habari, Umma na wadau wengine kuweza kufanya maamuzi ilikuongeza uwekevu, tija na ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za serikali. Aidha, ripoti hii ya majumuisho hailengi kuwa mbadala wa ripoti tatu ambazo zimefanyika kwa mwaka 2014. Kwa mantiki hii basi wasomaji wanashauriwa kusoma ripoti za Ukaguzi husikaili kuweza kupata undani wa kilichokaguliwa.

Ukaguzi wa Ufanisi katika eneo la Usimamizi wa Mipango Miji umefanyika ili kuweza kutoa tathmini kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wanasimamia upangaji wa miji nchini kwa kupitia mifumo ya mipango miji.Halmashauri saba zilichaguliwa pamoja na Mamlaka ya Uendelezaji wa Miji wa Dodoma. Vile vile, Ukaguzi wa Ufanisi kuhusiana na Ukarabati wa Majengo ya Serikali ulifanya tathmini kuona kama ukarabati wa majengo ya Serikali unafanyika kikamilifu kulingana na kanuni na taratibu zilizopo. Wakaguliwa wakuu ni Mamlaka ya Majengo Tanzania. Ukaguzi wa Usimamizi wa makisio na usambazaji wa dawa na vifaa tiba muhimu umelenga kwenye makisio na

usambazaji; utengenezaji na ufikishwaji wa oda sambamba na ufuatiliaji na tathmini wasambazaji wa madawa na vifaa tiba muhimu. Wakaguliwa wakuu walikuwa ni Bohari kuu ya Madawa na na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mapungufu yaliyobainika kwenye kaguzi hizo tatu ambayo yanahitaji kuboreshwa na Serikali ni haya yafuatayo: uandaaji dhaifu wa mipango, uratibu duni miongoni mwa wadau, ufuatiliaji na tathmini hafifu na uwepo wa vyanzo vya fedha visivyo aminika kwa shughuli zilizopangwa.

Katika ukaguzi wa Mipango Miji ilibainika kuwa, jumla ya miji 148 (80%) ilikuwa inaendelezwa bila kuwa na mipango kabambe inayotoa muongozo wa shughuli zote za uendelezaji wa ardhi mijini. Aidha, miji 96 (65%) kati ya miji 148 haijawahi kuandaa mipango kabambe toka ianzishwe.

Vilevile, ukaguzi kuhusiana na ukarabati wa majengo ya serikali umebaini kukosekana kwa viwango vya taratibu za ukarabati wa majengo ya Serikali ambavyo vilikuwa vinatumiwa na Wakala wa Majengo nchini (TBA). Katika mikoa sita iliyotembelewa, hakuna maboresho yeyote yaliyo fanyika kwenye viwango wala miongozo ya matengenezo ya majengo ya Serikali. Pia ukaguzi uligundua kuwa kiwango kikubwa cha matengenezo yanayofanyika bila kuwekwa kwenye mipango kwani ni miradi 272 (19%) tu ndiyo ambayo ilitekelezwa baada ya kuwa imeingizwa kwenye mipango. Pia hakuna utafiti uliofanyika kwenye jengo lolote lile katika mikoa hii iliyotembelewa kama muongozo wa matengenezo unavyoelekeza. Ukaguzi ulibaini mapungufu kadhaa katika kufuata mipango ya kazi iliyopo, utekelezaji wa mikakati, iliyopo na kufikia lengo lililowekwa la matengenezo ya majengo ya serikali kimkoa. Hii ni kwa kuwa katika mikoa yote sita iliyotembelewa na timu ya ukaguzi hakukuwa na mipango mikakati ya ukarabati, wakati mikoa mingine miwili haikuwana mipango kazi kabisa.

Kwa upande mwingine ripoti ya ukaguzi kuhusiana na usimamizi wa makisio na usambazaji wa dawa na vifaa tiba muhimu umebaini kuwa, Halmashauri za wilaya hazitoi kipaumbele katika suala la kuandaa mipango ya shughuli za makisio. Suala hili linafanywa kama shughuli inayojitegemea na haihusishwi na uandaaji wa mipango ya kina ya afya ya Halmashauri za Wilaya. Vilevile, Halmashauri za Wilaya hazifanyi makisio ya dawa. Makisio haya

yanatolewa katika ngazi ya Mfamasia wa Wilaya bila ya kuzihusisha ngazi za chini.Vilevile, kumekuwana vigezoduni ambavyo vimehusishwa kwenye makisio yanayofanywa ya dawa.

Mapungufu katika uratibu miongoni mwa wadau muhimu pia yameainishwa katika ripoti zote tatu. Ukaguzi wa usimamizi wa mipango miji umebaini kukosekana kwa uratibu kwa kuwa mamlaka hizo zinaandaa mipango kabambe bila kushirikisha taasisi muhimu za utoaji huduma kwa jamii kama vile Shirika la Simu nchini, Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka, Shirika la Umeme na Wakala wa usimamizi wa barabara nchini. Sambamba na hilo, ukaguzi wa ukarabati wa majengo ya serikali umeonyesha kuwa baadhi ya mikakati ya ukarabati wa majengo ya serikali haikuwa inaratibiwa vizuri.

Ufuatiliaji mdogo pia umebainika kwenye ripoti zote tatu za ukaguzi zilizofanyika. Kuhusu ukaguzi wa usimamizi wa mipango miji ilibainika kuwa, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendelo ya Makazi haifanyi ufuatiliaji vizuri kwenye shughuli za mipango miji kwa kuwa haikuweka viashiria vya ufuatiliaji vilivyoandaliwa ili kupima utekelezaji wa lengo lililokusudiwa na shughuli iliyofanyika. Vile vile TAMISEMI haifuatilii kikamilifu shughuli za mipango miji haswa baada ya kubaini kuwa zile Halmashauri zilizotembelewa hazitambui uwepo na kazi zinazofanywa na Idara ya Uendelezaji wa Miji iliyopo TAMISEMI.

Ukaguzi wa ufanisi kuhusiana na ukarabati wa Majengo ya Serikali umebaini kuwa, Wizara ya Ujenzi kama wasimamizi wakuu wa Wakala wa Majengo nchini, haijaweza kufuatilia kikamilifu na kufanya tathmini kuhusiana na shughuli za ukarabati wa majengo ya Serikali. hii ilitokana na kukosekana kwa mpango unaoangalia vihatarishi kwa lengo la kufanyia tathmini; hakukuwa na tathmini ambayo ilihusisha taratibu za Wakala wa Majengo kwenye ofisi zake za mikoani; hakukuwa na mfumo unaoonyesha idadi ya majengo yaliyopo; na hakukuwa na tathmini za kuonyesha kama hatua za marekebisho zinafanyika.

Vile vile ukaguzi kuhusiana na usimamizi wa makisio na usambazaji wa dawa na vifaa tiba muhimu umebaini kuwa, kuna mapungufu kwenye ufuatiliaji, kwa kuwa mipango kazi ya shughuli za kitengo cha kifamasia haiainishi njia za msingi za ufuatiliaji wa usambazaji wa madawa na vifaa tiba muhimu. Ni viashiria vichache tu vilivyowekwa kwa ajili ya ufuatiliaji.

Upatikanaji wa fedha usio madhubuti kwa shughuli ambazo zimepangwa ni miongoni mwa mapungufu yaliyobainika. Katika ukaguzi wa usimamizi wa mipango miji ilibainika kuwa, kulikuwa na mapungufu ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za mipango miji katika Halmashauri za wilaya. Halmashauri hizo zinategemea fedha zinazotengwa na Serikali kwenye vyanzo vingine vya pesa (OC), vyanzo vya fedha vya ndani na asilimia 30 ya kodi ya ardhi. Ilibainika pia kuwa asilimia 30 inayotokana na kodi ya ardhi haisimamiwi vizuri. Pia vyanzo vya ndani kwa Halmashauri nyingi sio toshelevu kwa usimamizi wa shughuli za mipango miji.

Ukaguzi wa ufanisi kuhusiana na usimamizi wa Ukarabati wa Majengo ya Serikali umebainisha kuwa kuna kiwango kidogo cha bajeti kinachotengwa kwa ajili ya shughuli za Ukarabati wa Majengo ya Serikali ikilinganishwa na bajeti nzima ya Wakala wa Majengo (TBA). Katika kipindi cha miaka mitatu iliyotazamwa kwenye ukaguzi huu ilibainika kuwa, bajeti iliyotengwa kwa shughuli za ukarabati haikuwahi kuzidi asilimia 0.5 kwa mwaka. Vile vile, ukaguzi wa ufanisi kuhusiana na usimamizi wa makisio na usambazaji wa dawa na vifaa tiba muhimu umebaini kuwa, upatikanaji wa fedha kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii sio madhubuti na hauna mpangilio. Serikali imekuwa ikitoa fedha ambayo ni pungufu kwa asilimia 10 ya fedha zote zinazohitajika katika awamu 8 kati ya 12 kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Kwa upande wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa, jumla ya mapendekezo 110 yalitolewa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwenye ripoti tano za Ukaguzi wa Ufanisi zilizowasilishwa Bungeni kati ya mwaka 2007 na 2010. Katika mapendekezo hayo, 49 yalitekelezwa kikamilifu, 42 yalitekelezwa kwa kiasi na 17 hayakutekelezwa kabisa.

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyopitaya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusiana na udhibiti wa Athari za mafuriko. Katika ukaguzi huu jumla ya mapendekezo 19 yalitolewa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, Tawala za Mikoa, Halmashauri ya Wilaya ya Babati na Mamlaka ya Usimamizi wa Miradi ya Barabara Mkoa wa Manyara. Mapendekezo 10 kati ya 19 yalitekelezwa kikamilifu; 6 yalitekelezwa kwa kiasi na 3 hayakutekelezwa kabisa.

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyopita kuhusiana na Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Tiba ya Afya ya Msingi ulibaini kuwa, mapendekezo 20 yalitolewa kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa

Jamii, TAMISEMI na halmashauri. Pendekezo moja kati ya 20 halikutekelezwa kabisa, mapendekezo 10 yalitekelezwa kwa kiasi na 9 yalitekelezwa kikamilifu.

Kwa upande mwingine, ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusiana na Programu ya Ukaguzi kwa Shule za Sekondari nchini unaonyesha kuwa mapendekezo 12 yalitolewa kwa idara ya ukaguzi mashuleni. Mapendekezo 6 kati ya 12 yalitekelezwa kikamilifu, 5 yalitekelezwa kwa kiasi tu na 1 halikutekelezwa kabisa.

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa taka ngumu kwenye miji mikuu umebainisha kuwa mapendekezo 39 yalitolewa kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Shirika la Viwango nchini na Halmashauri za Wilaya. Kati ya mapendekezo hayo 39, 11 yalitekelezwa kikamilifu, 16 yalitekelezwa kwa kiasi tu na 12 hayakutekelezwa kabisa.

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Ujenzi wa Barabara nchini umeonyesha kuwa, Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Usimamizi wa Barabara nchini wameweza kwa kiasi kikubwa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa. Kati ya mapendekezo 20, mapendekezo 2 hayakutekelezwa, wakati 5 yalitekelezwa kwa kiasi na yanahitaji uangalizi wa karibu.

Kwa kuhitimisha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itaendelea kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ambayo yalitekelezwa kwa kiasi tu na yale ambayo hayakutekelezwa kabisa. Ripoti ya ufuatiliaji itaandaliwa na kuwasilishwa bungeni mwakani.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Ukaguzi

Ukaguzi wa Ufanisi ni muhimu kwani unalenga kuboresha uwajibikaji na utendaji wa taasisi za Serikali ili wananchi wapate huduma za Serikali zenye Thamani ya fedha iliyotumika. Vigezo kadhaa hutumika wakati wa uchaguzi wa maeneo yanayotazamwa wakati wa Ukaguzi wa ufanisi na maalumu. Miongoni mwa hayo hujumuisha malalamiko kutoka kwa jamii na umuhimu wa eneo linaloangaliwa na sababu za kijamii na kiuchumi.

Ukaguzi wa ufanisi una lengo la kufanya tathmini ya kiwango ambacho mkaguliwa ametumia rasilimali zake katika kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Ukaguzi wa ufanisi una tathmini kama shughuli, mipango au miradi inayohusisha rasilimali za umma katika Wizara, Idara, Serikali za Mitaa na Mashirika yote ya umma imesimamiwa kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Uwekevu, tija na ufanisi unaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

Uwekevu - kupunguza gharama ya rasilimali zinazotumika katika shughuli kwa kuzingatia ubora sahihi.

Tija - uhusiano kati ya matokeo, katika suala la bidhaa, huduma, na rasilimali zilizotumika kuzalishia.

Ufanisi - kiwango ambacho malengo yamefikiwa na uhusiano kati ya malengo yaliyokusudiwa na matokeo halisi katika shughuli husika.

1.2 Mamlaka ya Kukagua

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kisheria ya kufanya Ukaguzi wa Ufanisi kupitia Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.

Kifungu cha 28 cha Sheria hii kinasema “Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa lengo la kuthibitisha uwekevu, tija na ufanisi katika matumizi ya fedha au rasilimali za taasisi ya umma, anaweza kukagua, kuchunguza na kutoa ripoti, kadiri atakavyoona inafaa, juu ya:

(a) Matumizi ya fedha na rasilimali za umma katika wizara, idara, mamlaka za mitaa na mamlaka nyingine za serikali;
(b) Utekelezaji wa majukumu ya maafisa masuuli, wakuu wa idara na wakuu wa taasisi mbalimbali za umma;
(c) Utekelezaji wa matakwa ya sheria ya mazingira, kanuni na sera ya ndani ya mazingira na viwango.

Ukaguzi wa ufanisi unalenga kuangalia kama malengo ya awali yaliyowekwa yamefanikiwa. Kisha unaangalia kama uwekevu, tija na ufanisi vimezingatiwa. Mapendekezo yanatolewa kwa ajili ya kuboresha maeneo yaliyoonekana kuwa na mapungufu.

Ukaguzi unafanyika kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi wa ufanisi. Viwango hivyo vinataka, timu ya ukaguzi kupanga na kutekeleza ukaguzi ili kupata ushahidi wa kutosha ambao utakuwa kigezo cha kuripoti mapungufu yaliyoonekana na kutoa hitimisho kwa kuzingatia lengo la ukaguzi husika.

1.3 Madhumuni ya Ripoti

Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu waheshimiwa wabunge, vyombo vya habari, Umma pamoja na wadau wengine ili waweze kutoa maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija na ufanisi katika shughuli za serikali.

Ripoti hii haikusudii kuwa mbadala wa ripoti tatu za Ukaguzi wa Ufanisi ambazo zimefupishwa katika sura zinazofuata. Ili kuweza kupata uelewa wa kina wa mada mahsusi zilizozungumzwa katika ripoti hii, msomaji anashauriwa kusoma ripoti binafsi zilizokamilika. Ripoti hizo ni za kaguzi za Ufanisi katika maeneo yafuatayo:

- Mipango Miji;
- Makisio ya Mahitaji na Usambazaji wa Dawa na Vifaa Tiba Muhimu; na
- Ukarabati wa Majengo ya Serikali.

Ifuatayo ni orodha ya ripoti tano zilizokwisha wasilishwa Bungeni ambazo utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa umefuatiliwa, ripoti hizo ni:

- Kudhibiti na Kupunguza Athari za Mafuriko kwa Serikali Kuu, Mikoa na Mitaa kwa (2007)
- Utoaji wa Huduma ya Afya ya Msingi: Vituo vya Afya (2009)
- Programu ya Ukaguzi kwa Shule za Sekondari nchini (2009)

- Usimamizi wa Udhibiti wa Taka Ngumu katika Miji Mikuu na Mikoa nchini (2009)
- Ujenzi wa Barabara nchini (2010)

1.4 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu

Wizara, Idara na Wakala mbalimbali za Serikali zilizokaguliwa zilipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao juu ya matokeo ya ukaguzi na kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika rasimu ya taarifa hii.

1.5 Muundo wa Ripoti

Ripoti hii ya jumla imeundwa katika sura nane kama ifuatavyo:

Sura ya kwanza inatoa utangulizi kuhusu sehemu ya kaguzi ya ufanisi, mamlaka ya ukaguzi, madhumuni ya ripoti ya jumla, viwango vinavyotumika na mchakato wa uthibitisho wa takwimu.

Sura ya pili na ya tatu zimeandaliwa kama muhtasari wa ripoti tatu. Muhtasari huu umeandikwa katika mtiririko wa nini kilichochunguzwa, sababu za kuchunguza, nini kilichoonekana, hitimisho na mapendekezo yaliyotolewa kwa Afisa Masuuli. Sura ya Pili imelenga kuelezea kwa ufupi kaguzi zilizofanyika; Sura ya Tatu inajumuisha madhaifu yanayofanana kama yalivyoonekana katika kaguzi hizo tatu.

Sura ya nne hadi ya nane zinalenga kufuatilia hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi yaliyotolewa katika kaguzi zilizotangulia.

SURA YA PILI

MAELEZO MAFUPI YA KAGUZI ZILIZOFANYIKA NA UFUATILIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAGUZI

2.1 Utangulizi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya kaguzi tatu za ufanisi ambazo ni Usimamizi wa Mipango Miji, Usimamizi wa Ukarabati wa majengo ya Serikali na Makisio ya Mahitaji na Usambazaji wa Dawa na Vifaa Tiba muhimu.

Dhumuni kuu la kaguzi hizo tatu zilizofanyika ilikuwa ni kuangalia kama taasisi husika zilizingatia tija na ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Maelezo mafupi kuhusiana na kaguzi zilizofanywa ni kama ifuatavyo:

2.2 Usimamizi wa Mipango Miji nchini

Kwa sasa, idadi ya watu wanaoishi katika maeneo ya mijini kwa upande wa Tanzania Bara imeongezeka kutoka asilimia 5.7 mwaka 1967 hadi asilimia 29.1 mwaka 2012 ikiambatana na kiwango cha ukuaji wa asilimia 5.2 (NBS 2012). Kiwango cha ukuaji wa miji kimekuwa ni kikubwa kuliko uwezo wa mamlaka husika kutoa huduma za viwanja vilivyopangwa kwa makazi na shughuli za maendeleo ya miji. Jiji la Dar es Salaam linakadiriwa kuwa na nyumba zipatazo 400,000 kati ya 500,000 zilizoendelezwa katika maeneo yasiyopangiliwa au makazi yasiyo rasmi ambayo hayajapimwa[1]. Hali hii ni sawa pia katika miji mingine mikubwa kama Mwanza na Arusha ambayo kwa kiasi kikubwa imetokana na asilimia 88 ya waendelezaji katika maeneo ya mijini kupata viwanja kutoka katika masoko ya ardhi yasiyo rasmi. Maeneo haya yanahusishwa na kiwango dhaifu cha huduma za msingi za jamii, msongamano, ukosefu wa usalama wa makazi pamoja na hali duni ya usafi wa mazingira.

Serikali imechukua hatua kadhaa katika kukabiliana na kuongezeka kwa matatizo ya mipango miji. Hatua hizo ni pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya 2007; uanzishwaji wa Idara ya Uendelezaji Miji ndani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya

[1]Ripoti ya mradi wa kuhuisha maeneo yasiyopangwa iliyoandaliwa na Wizara ya Ardhi , Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2013-Imepatikana toka tovuti ya Ardhi.go.tz kwa mwezi wa Aprili,2014

Makazi, TAMISEMI na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na uanzishwaji wa miradi mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Baadhi ya Miradi hiyo ni mpango wa kukabiliana na matokeo hasi kama huduma dhaifu za jamii, msongamano, ukosefu wa usalama na hali duni ya usafi wa mazingira inayotokana na ukuaji wa haraka wa miji. Nyingine ni Programu ya Uimarishaji wa Serikali za Miji na Mitaa, Programu ya Miji ya Mfano na Programu ya Kimkakati ya Udhibiti wa Kurasimisha Makazi yasiyo rasmi.

Licha ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali suala la mipango miji limeendelea kuwa tatizo na hivyo kusababisha ukuaji mkubwa wa makazi yasiyopangiliwa katika miji mingi nchini.

Mipango Miji inasimamiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia divisheni ya Mipango ya Ardhi na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupitia divisheni ya Uendelezaji wa Miji. Shughuli za Mipango Miji zinasimamiwa kwa mujibu wa Sera ya Kitaifa ya Maendeleo ya Watu na Makazi ya mwaka 2000, Sera ya Kitaifa ya Ardhi ya mwaka 1995, Sera ya Kitaifa ya Mazingira ya mwaka 1997; Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007 na Sheria ya Ardhi Na.4 Kifungu 113 cha mwaka 1999.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliamua kufanya ukaguzi wa ufanisi katika eneo la mipango miji ili kuchunguza kama Wizara ya Ardhi na TAMISEMI zinasimamia mipango miji kwa tija.

Ukaguzi ulilenga kuangalia namna Wizara ya Ardhi na TAMISEMI zinavyosimamia mipango miji nchini kupitia mifumo iliyopo. Ukaguzi huu ulilenga pia kuangalia uendelezaji wa mipango miji, mikakati na utekelezaji wa mipango yake pamoja na ufuatiliaji na tathmini za utekelezaji wa mipango na mikakati ya mipango miji.

Ukaguzi huu ulifanyika kwa kuangalia kipindi cha miaka mitatu ya fedha kuanzia Julai, 2010 mpaka Juni, 2013 ili kubainisha mwenendo wa utendaji kwa kipindi husika. Vivyo hivyo ukaguzi huu ulilenga kuangalia utekelezaji wa Sheria ya Mipango Miji ya 2007 iliyoanza kutumika kuanzia 2010.

Mamlaka saba za Serikali za Mitaa zilichaguliwa kama sampuli za ukaguzi. Mamlaka hizo ni; Halmashauri za Majiji ya Dar es Salaam na Mbeya, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Hlmasahuri za Miji

ya Babati na Kahama pamoja na Halmashauri za Wilaya ya Newala na Kigoma. Uchaguzi wa mamlaka hizo za serikali za mitaa ulifanywa kwa kuzingatia kundi la mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini ambazo ni Majiji, Manispaa, Wilaya na Miji pamoja na uwakilishi wa kijiografia kwa nchi.

Ukaguzi huu pia ulijumuisha Mamlaka ya Uendelezaji wa Mji wa Dodoma (CDA) katika manispaa ya Dodoma, kwa kuwa ni mamlaka pekee huru ya ustawishaji yenye mamlaka ya kutoa huduma za mipango miji. Kwa hiyo, CDA ilichaguliwa kwa lengo la kuonyesha ulinganisho wa kiutendaji baina ya mamlaka mbalimbali za mipango miji.

Usimamizi wa Ukarabati wa Majengo ya Serikali

Majengo ya serikali yamekuwa hayafanyiwi ukarabati wa mara kwa mara. Hii imefanya kuwepo kwa mazingira yasiyo salama ya sehemu za kazi/makazi kwa wafanyakazi wa serikali hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya majengo haya yamejengwa zaidi ya miaka 80 iliyopita. Ukarabati yakinifu wa majengo ni muhimu kwa kuwa unayaweka majengo katika hali yake ya awali kwa manufaa ya wakazi na watumiaji wake. Lengo mahsusi la ukarabati wa majengo ni kuliweka jengo katika hali yake ya mwanzo wa matumizi wakati likihifadhiwa kulingana na sehemu husika, thamani yake ya uwekezaji, na kuwa na muonekano mzuri ili liweze kutumika kwa ufanisi kulingana na malengo yaliyokusudiwa. Hata hivyo kutokana na hali kuendelea kuwa mbaya kwa baadhi ya majengo ya serikali, Wizara, Idara na Wakala za Serikali zimeanza kujihusisha katika ukarabati wa majengo wanayoyatumia, kazi ambazo sio wajibu wao wa msingi. Matumizi ya Wizara, Idara na Wakala za serikali katika ujenzi na ukarabati wa majengo yameongezeka katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kutoka shilingi Trillioni 1.429 mwaka wa fedha 2010/2011 hadi shilingi Trillion 2.260 katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Ukarabati wa majengo ya serikali unasimamiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA). Wakala wa Majengo ya Serikali iliundwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 na inafanya kazi kama mamlaka inayojitegemea chini ya Wizara ya Ujenzi. Majukumu na wajibu wa Wakala wa Majengo ni; Ukarabati wa majengo ya serikali na utoaji wa ushauri wa kitaalamu wa majengo kwa Serikali kwa mambo yote yahusianayo na kazi za

majengo. Wizara ya Ujenzi ina jukumu la kusimamia kwa ujumla shughuli za Wakala wa Majengo ya Serikali na kutoa miongozo kwa utendaji wa Wakala wa Majengo kulingana na sera husika. Wizara ya Ujenzi pia ina jukumu la kutoa fedha na rasilimali nyingine muhimu kwa shughuli za Wakala wa Majengo zinazohusu ukarabati wa majengo ya serikali.

Lengo la Ukaguzi

Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo ukarabati wa majengo ya serikali unafanywa kwa kiwango kinachotakiwa. Malengo mahsusi ya ukaguzi yalikuwa ni kuangalia iwapo Wakala wa Majengo nchini :

- anafanya shughuli za ukarabati wa majengo kwa kiwango stahili;
- ana miongozo na nyaraka zinazotakiwa kwa mipango yenye tija ya ukarabati wa majengo ya serikali;
- ana mifumo ya ndani ya usimamizi na ufuatiliaji wa ukarabati wa majengo ya serikali yenye ufanisi na kuhakikisha kwamba malengo na makusudio yanafikiwa; na
- ukaguzi ulilenga kuangalia pia kama Wizara ya Ujenzi inasimamia na kutathmini kwa kiwango cha kutosha utendaji wa Wakala wa Majengo katika ukarabati wa majengo ya Serikali .

Mambo yaliyochunguzwa katika Ukaguzi yaliangazia mipango, utendaji, ufuatiliaji na utathmini wa kazi za ukarabati kwa Wakala wa Majengo na Wizara ya Ujenzi.

Mkaguliwa mkuu alikuwa ni Wakala wa Majengo ya Serikali, iliyopo chini ya Wizara ya Ujenzi. Ukusanyaji wa taarifa ulifanyika Makao Makuu ya Wakala wa Majengo na Ofisi zake za Mikoa. Taarifa zilizokusanywa pia kutoka Wizara ya Ujenzi na Kurugenzi ya Majengo kama mdau muhimu katika usimamizi wa shughuli za ukarabati wa majengo ya serikali nchini Tanzania.

Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia kipindi cha miaka mitatu ya fedha kuanzia 2010/11, 2011/12 na 2012/13 ili kubainisha mwenendo wa utendaji kwa kipindi husika.

2.4 Usimamizi wa Makisio na Usambazaji wa Dawa na Vifaa Tiba Muhimu

Upungufu wa dawa na vifaa tiba muhimu katika vituo vingi vya afya vya umma ni tatizo kubwa nchini. Tatizo hili limeendelea kuwepo licha ya mageuzi kadhaa yaliyofanywa na Serikali. Mapitio ya hivi karibuni ya Mlolongo wa Usambazaji wa Madawa nchini unaonyesha kwamba madawa na vifaa tiba muhimu vinakosekana katika vituo vya afya. Vivyo hivyo, katika taarifa iliyotolewa na Shirika la Afya Duniani mwaka 2014 inaonyesha kwamba, wastani wa upatikanaji wa dawa muhimu kwa ujumla katika nchi ya Tanzania katika vituo vya afya vya serikali ni asilimia 23.4 tu, wakati wastani wa upatikanaji katika vituo binafsi vya afya ukiwa ni asilimia 47.9. Aidha, ripoti iliyotolewa na Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii juu ya mapitio ya uchambuzi wa muhula wa katikati wa ufanisi wa Mpango Mkakati wa Tatu wa Kitaifa wa Sekta ya Afya wa 2009-2015, inaonyesha kwamba, upatikanaji wa madawa 14 ambayo yanatumika kama viashiria vya kupima uwepo wa dawa katika vituo vya afya kwa ujumla ni mdogo.

Makisio na Usambazaji wa Dawa na Vifaa Tiba Muhimu nchini unasimamiwa na Sheria ya Bohari ya Dawa Na 13 ya mwaka 1993 na Sera ya Afya ya Taifa ya mwaka 2003. Inaongozwa pia na Mkakati wa Kitaifa wa Tatu wa Sekta ya Afya (HSSP III) wa Julai 2009 hadi June 2015 na Mfumo Jumuishi wa Ugavi wa Dawa.

Bohari Kuu ya Dawa imepewa mamlaka ya kusimamia usambazaji wa madawa na vifaa tiba muhimu vilivyoruhusiwa kutumiwa na vituo vya afya vya umma hapa nchini. Kati ya majukumu yake makubwa ni: kukuza, kudumisha, kusimamia ufanisi na mfumo wa gharama nafuu wa manunuzi, uhifadhi na usambazaji; ufuatiliaji wa mahitaji yao na usambazaji na kuchukua hatua zinazohitajika ni: kuhakikisha upatikanaji wake kwa wakati muafaka. Wizara ya Afya ina jukumu kubwa la kufuatilia na kutathmini utendaji wa Bohari Kuu ya madawa katika kukadiria mahitaji na kusambaza dawa na vifaa tiba muhimu ikiwa na lengo la kuimarisha upatikanaji wake katika vituo vya afya vya umma.

Lengo la Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa ni kuangalia iwapo Bohari Kuu ya Dawa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zinachukua hatua

stahiki zitakazopelekea kupatikanaji kwa dawa na vifaa tiba muhimu kwa wakati katika vituo vya afya nchini. Ukaguzi ulilenga kuangalia iwapo:

- Bohari Kuu ya madawa inahakikisha kuwa ukadiriaji wa mahitaji ya dawa na vifaa tiba muhimu unafanywa kwa kuzingatia ufanisi;
- Bohari Kuu ya Madawa inasambaza kwa ufanisi madawa na vifaa tiba ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wake kwa wakati; na
- Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inasimamia kwa ufanisi upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya.

Ukaguzi ulijikita zaidi kwenye makisio ya mahitaji, uandaaji wa mahitaji, na usambazaji wa dawa na vifaa tiba, pamoja na tathmini na ufuatiliaji wa mfumo wa ugavi wa dawa na vifaa tiba muhimu. Wakaguliwa wakuu walikuwa ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia kitengo cha Huduma za Madawa pamoja na Bohari Kuu ya Madawa.

Vile vile Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia vituo vya afya na zahanati vilihusishwa kwa kuwa ni shehemu ya mfumo wa Afya ya Msingi inayotoa wigo mpana wa huduma za afya katika jamii.

Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka mitatu ya fedha kuanzia mwaka 2010/2011 hadi 2012/2013.

2.5 Kufuatilia Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mapendekezo ya kaguzi za Ufanisi ni hatua muhimu ili kuhakiki kama mapendekezo yaliyotolewa awali yamefanyiwa kazi na kwamba utoaji wa huduma husika umekuwa bora zaidi. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu imefuatilia na kutathmini kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za ufanisi kwa ripoti tano zilizotolewa. Ripoti hizi ziliwasilishwa Bungeni na kutolewa kwa umma na kisha Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu ikafanya mahojiano na Maafisa Masuuli husika. Hizi ni Kaguzi za Ufanisi katika:

- Kuzuia na Kudhibiti Athari za Mafuriko ya mwaka 2007;
- Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi nchini ya mwaka 2009;

- **Programu ya Ukaguzi wa Shule za Sekondari Tanzania ya mwaka 2009;**
- **Usimamizi wa Udhibiti wa Taka Ngumu katika Miji Mikubwa na mikoa nchini ya mwaka 2009; na**
- **Usimamizi wa Kazi za Ujenzi wa Barabara nchini ya mwaka 2010.**

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyokuwamo katika ripoti hii, inaonyesha kwa kifupi kuwa jumla ya mapendekezo 110 yalitolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Jedwali namba 2.1 linaonyesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa yakiainishwa kama "yametekelezwa kikamilifu, kwa kiasi na ambayo hayakutekelezwa"

Jedwali 2.1: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi

Ripoti ya Kaguzi ya Ufanisi	Idadi ya Mapendekezo yaliyotekelewa Kikamilifu	Idadi ya Mapendekezo yaliyotekelewa Kiasi	Idadi ya Mapendekezo yasiyotekelezwa	Jumla
Kuzuia na Kudhibiti Athari za Mafuriko	10	6	3	19
Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi nchini	9	10	1	20
Programu ya Ukaguzi wa Shule za Sekondari nchini	6	5	1	12
Usimamizi wa Udhibiti wa Taka Ngumu katika Miji Mikubwa na Mikoa nchini	11	16	12	39
Usimamizi wa Kazi za Ujenzi wa Barabara Tanzania	13	5	2	20
Jumla	**49**	**42**	**19**	**110**

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo inaonyesha kwamba mapendekezo 49 yalifanyiwa kazi kwa kiwango cha kuridhisha; 42 yalifanyiwa kazi kwa kiasi; na 19 hayakufanyiwa kazi kabisa.

Vile vile, tathmini ilifanyika kwa mapendekezo kulingana na makundi yaliyowekwa, lengo ilikuwa ni kutathmini kiwango cha utekelezaji

wa mapendekezo hayo. Tathmini hiyo ni kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali 2.2

Jedwali 2.2: Idadi ya Mapendekezo ambayo Hayajatekelezwa

Makundi ya Mapendekezo	Jumla ya Mapendekezo yaliyotolewa kwa Makundi	Idadi ya Mapendekezo yasiyotekelezwa
Usimamizi wa Mapato	10	5
Mgawanyo wa majukumu	4	3
Mipango	14	3
Usimamizi wa Ufanisi	17	3
Bajeti	8	2
Usimamizi na utekelezaji wa Sheria	3	1
Mgawanyo na Matumizi ya Rasilimali	4	1
Ufuatiliaji, Tathmini na Usimamizi	9	1
Utoaji wa Taarifa na Mawasiliano	10	1

Tathmini ya Jedwali 2.2 inaonyesha kuwa mapendekezo yanayohusu maeneo ya ufanisi wa taasisi za Serikali, kama vile: usimamizi wa mapato, mgawanyo wa majukumu, mipango, usimamizi wa ufanisi, bajeti na usimamizi na utekelezaji wa Sheria. Maeneo mengine ni mgawanyo na matumizi ya rasilimali zilizopo, ufuatiliaji, tathmini na usimamizi wa kazi zilizotolewa na utoaji wa taarifa na mawasiliano ya kazi zilizofanyika. Maeneo haya yote hayakutekelezwa na mengine yalitekelezwa kikamilifu au kwa kiasi.

Hii inaashiria kuwa kushindwa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa ambayo ni muhimu kwa kuboresha ufanisi wa taasisi za Serikali zilizokaguliwa kuna kwamisha kufanya maboresho kwenye huduma zinazotolewa na taasisi za Serikali. Pia inapelekea kushindwa kutoa huduma nzuri kwa umma.

Ufafanuzi zaidi wa matokeo ya ufuatiliaji wa kaguzi za Ufanisi yanatolewa kwenye sura ya nne mpaka ya nane.

SURA YA TATU

MAPUNGUFU YANAYOJIRUDIA KATIKA UTENDAJI WA SERIKALI KAMA YALIVYOAINISHWA KATIKA KAGUZI ZA UFANISI

3.1 Utangulizi

Kulingana na malengo ya ukaguzi na matokeo yaliyoonekana katika kaguzi tatu zilizofanyika kama yalivyoainishwa katika ripoti hii ya jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi, yamebainisha mambo ya msingi yanayohitaji kutiliwa mkazo zaidi ili kuwezesha Serikali kufanya kazi na kusimamia shughuli zake za utoaji huduma kwa ufanisi na tija. Mambo yaliyoonekana kuwa na madhaifu yanayojirudia katika kaguzi zote tatu yanayohusiana mipango, uratibu, ufuatiliaji, tathmini na uwezeshaji wa fedha. Maelezo ya madhaifu haya yameainishwa hapa chini:

3.2 Mipango Isiyotosheleza ili kutimiza malengo husika

Udhaifu katika kuandaa mipango umejitokeza katika kaguzi zote tatu kama inavyoonekana hapa chini:

Mipango Isiyotosheleza Uendelezaji Miji

Halmashauri 96 (65%) kati ya 148 hazijawahi kuandaa au kutengeza Mpango Kabambe tangu kuanzishwa kwake. Ukaguzi ulitathmini ni kwa kiwango gani Mamlaka za Mipango Miji zimeandaa Mipango ya uendelezaji wa Miji yao ili kutoa muongozo sahihi wa maendeleo ya Halmashauri; na iwapo mikakati ya mipango iliyoanzishwa inagusa matatizo yaliyopo kwenye mipango miji nchini Tanzania. Ilijidhihirisha kwamba Halmasahuri 148 (80%) zilikuwa zinafanya kazi bila kuwa na Mipango kabambe ya kuongoza matumizi ya ardhi mijini.

Uwepo wa mipango ya mji madhubuti huongeza ufanisi; hupunguza hatari zinazohusiana na biashara; huwezesha uratibu sahihi; husaidia kuandaa, inatoa mwelekeo sahihi; inaweka udhibiti mzuri; inasaidia kufikia malengo; inahamasisha wafanyakazi na inasaidia katika kufanya maamuzi sahihi ya kuendeleza mji husika.

Mipango dhaifu ni moja ya maeneo yaliyoonekana katika kaguzi zote za ufanisi zilizofanyika ambazo zinahusiana na mipango miji,

ukarabati wa majengo ya serikali na makisio na usambazaji wa madawa na vifaa tiba muhimu. Hili ni kama lilivyoanishwa hapa chini:

Imeonekana katika ukaguzi wa usimamizi wa mipango miji kwamba, mamlaka husika za upangaji wa miji kama vile Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Majiji na CDA hazina au hazihuishi mipango kabambe ya uendelezaji wa miji husika. Mamlaka hizo zina jukumu la kuainisha maeneo ya kupangwa, kuandaa mipango ya uendelezaji mji (Mipango kabambe, kina na ya muda mpito), kusimamia utekelezaji wa mipango iliyoandaliwa, kutekeleza udhibiti wa uendelezaji wa ardhi pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya kuendeleza mipango miji.

Ukaguzi wa ufanisi kwenye Ukarabati wa Majengo ya Serikali unaonyesha kukosekana kwa mipango na miongozo yenye ufanisi kwa shughuli za usimamizi na utekelezaji wa miradi ya ukarabati wa majengo ya Serikali. Hali hii inachangiwa na:

Kukosekana kwa taratibu yakinifu za usimamizi wa ukarabati wa majengo ya Serikali

Ilionekana kwamba hakukuwa na taratibu rasmi zilizokuwa zikifuatwa na Wakala wa Majengo katika kusimamia ukarabati wa majengo ya Serikali.

Kila ofisi ya mkoa ya Wakala wa Majengo nchini ilifuata taratibu zake kwa kadiri ya uzoefu na utaalamu wa watendaji wenye wajibu wa kusimamia kazi zote za ukarabati wa Majengo ya Serikali katika Mikoa yao (Jedwali 3.1).

Jedwali 3.1: Uzingatiaji wa Hatua za Ukarabati wa Majengo katika Mikoa

HATUA ZA MATENGENEZO	MKOA						JUMLA "NDIYO"
	Arusha	Dodoma	Dsm	Mtwara	Mwanza	Tabora	
Utambuzi wa jumla wa vipengele katika jengo	NDIYO	NDIYO	NDIYO	HAPANA	HAPANA	NDIYO	4/6
Mapitio ya Viwango na Miongozo	HAPANA	HAPANA	HAPANA	HAPANA	HAPANA	HAPANA	0/6
Ukaguzi wa Kina na Maandalizi ya ukarabati	NDIYO	HAPANA	NDIYO	HAPANA	HAPANA	NDIYO	3/6
Maamuzi ya Aina ya Ukarabati	NDIYO	NDIYO	NDIYO	HAPANA	HAPANA	NDIYO	4/6
Kuandaa mpango endelevu wa Ukarabati	NDIYO	HAPANA	HAPANA	HAPANA	HAPANA	HAPANA	1/6
JUMLA "NDIYO"	4/5 (1)	2/5 (4)	3/5 (2)	0/5	0/5(5)	3/5 (3)	

Chanzo: Muongozo wa Ukarabati wa Majengo yanayosimamiwa na Wakala wa Majengo.

Jedwali 3.1 linaonyesha orodha ya hatua kama zilivyoainishwa katika muongozo wa ukarabati wa majengo na utekelezaji wake katika mikoa sita iliyotembelewa. Mikoa yote sita iliyotembelewa haikufanya mapitio ya viwango na miongozo katika ukarabati wa majengo. Ni Mkoa mmoja pekee ulioweza kuandaa mpango endelevu wa ukarabati wa majengo wakati mikoa mitano iliyobaki haijawahi kufanya hivyo. Mikoa mingi ilikuwa ikifanya utambuzi wa jumla wa vipengele katika majengo yanayohitaji ukarabati na uamuzi wa aina ya matengenezo yanayopaswa kufanywa.

Wakati wa mahojiano na maafisa wa Wakala wa Majengo katika mikoa iliyotembelewa ilionekana kwamba, hakukuwa na nyaraka zinazotumiwa kama muongozo wa kufuatwa wakati wa utekelezaji wa kazi za ukarabati. Wengi wa maafisa hao walisema kwamba hawatengenezi mipango endelevu ya ukarabati wa majengo.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kwamba mikoa ya Mtwara na Mwanza haikufuata hatua hizo zilizoainishwa kwenye Jedwali 3.1 wakati ikifanya ukarabati wa nyumba za Serikali. Wakati huo huo, mkoa wa Dodoma ukitekeleza hatua mbili tu kati ya hizo. Pia ilibainika kuwa hakukuwa na hatua rasmi zilizowekwa kwa ujumla katika mikoa yote ili kutoa muongozo wakati wa kufanya ukarabati wa majengo ya Serikali.

Kiwango kikubwa cha ukarabati usiopangwa kwa majengo ya serikali

Idadi kubwa ya miradi ya ukarabati wa majengo ya Serikali uliofanywa na Wakala wa Majengo katika ofisi za mikoa bila kupangwa na ilitekelezwa kama miradi ya dharura Tazama Jedwali 3.2.

Jedwali 3.2: Ukarabati uliopangwa na ambao Haukupangwa (2010/11 hadi 2012/13)

MKOA	IDADI YA MIRADI YA UKARABATI	IDADI YA MIRADI YA UKARABATI ISIYOPANGWA
Arusha	16	16
Dar es Salaam	738	466
Dodoma	684	684
Mtwara	3	3
Mwanza	6	6
Tabora	0	0
JUMLA	1447	1175(81%)

Chanzo: *Majalada ya nyumba katika mikoa (2010-2013)*

Jedwali 3.2 linaonyesha kwamba idadi kubwa ya miradi ya ukarabati wa majengo iliyofanywa na Wakala wa Majengo haikupangwa. Jedwali linaonyesha kwamba ni miradi 272 pekee (19%) ndiyo iliyotekelezwa ikiwa sehemu ya miradi iliyopangwa.

Hakuna utaratibu wa kiufanisi wa kupata mahitaji ya ukarabati

Ingawa Wakala wa Majengo imetoa muongozo na namna ya kufanya utafiti wa hali ya majengo, muongozo huo haufuatwi na wahusika wa utekelezaji wa shughuli za ukarabati katika mikoa. Kupitia mahojiano yaliyofanywa na mameneja wa Wakala wa Majengo

katika mikoa iliyotembelewa na timu ya ukaguzi. Hali hii ilitokana na kutokusambazwa kwa muongozo huo katika mikoa husika na ilibainika katika mikoa yote sita ya ofisi za Wakala wa Majengo kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali 3.3.

Jedwali 3.3: Tathmini na hali za majengo zilizotakiwa na idadi halisi ya tathmini zilizofanyika mwaka wa fedha 2012/2013

Mikoa	Idadi ya Nyumba zinazohitaji Tafiti Hali	Idadi ya Tafiti Hali zilizofanyika
Arusha	96	0
Dar es Salaam	291	0
Dodoma	472	0
Mtwara	119	0
Mwanza	253	0
Tabora	47	0

Chanzo: *Ripoti za Mwaka za Utekelezaji katika mikoa (2012/2013)*

Jedwali 3.3 inaonyesha kwamba hakukuwa na tathmini zilizofanyika katika majengo yote yaliyopo katika mikoa sita kama inavyotakiwa katika muongozo wa ukarabati majengo ya Serikali. Mikoa ilikuwa na idadi tofauti ya majengo yanayohitaji tathmini; hata hivyo hakuna tathmini ambayo umefanyika. Kulingana na mahojiano na mameneja wa mikoa husika, hali hii ilitokana na ukosefu wa fedha za kugharamia kazi hiyo ya tathmini ya hali ya uchakavu wa majengo licha ya kwamba shughuli hii ilijumuishwa katika mpango mkakati wao wa mwaka.

Mipango isiyojitosheleza katika ngazi ya utekelezaji

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pia iliona madhaifu mbalimbali katika uzingatiaji wa mipango kazi, utekelezaji wa mikakati na kufanikiwa kwa malengo yaliyowekwa katika ukarabati wa majengo ya Serikali kwenye mikoa hiyo sita iliyotembelewa na timu ya ukaguzi (Jedwali 3.4).

Jedwali 3.4: Mipango inayoandaliwa katika ngazi ya mikoa kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa shughuli za ukarabati wa majengo

MKOA	MIPANGO YA MWAKA YA MKOA	MIPANGO YA KAZI
Arusha	HAKUNA	HAKUNA
Dar es Salaam	IPO	HAKUNA
Dodoma	IPO	HAKUNA
Mtwara	IPO	HAKUNA
Mwanza	IPO	HAKUNA
Tabora	IPO	HAKUNA

Chanzo: *Ripoti za Utekelezaji za Mkoa*

Jedwali 3.4 linaonyesha kwamba mikoa mitano kati ya sita ina mipango kazi ya mwaka ya kimkoa. Hata hivyo hakuna mkoa ambao ulikuwa na mipango ya shughuli za ukarabati inayoonyesha rasilimali zinazohitajika. Vile vile kati ya mikoa hiyo sita mikoa ya Arusha na Tabora haikuwa na mipango ya kazi ya mwaka wala mipango ya shughuli za ukarabati. Mipango hiyo ni muhimu kwenye utekelezaji wa miradi ya ukarabati wa majengo kwa kuwa zinaainisha namna kazi za ukarabati wa majengo zitakavyotekelezwa na kudhibiti matumizi ya muda na rasilimali katika ukarabati wa majengo. Kutokuwepo mipango kazi hiyo kunakoashiria kukosekana kwa tija katika utekelezaji wa kazi za ukarabati zinazofanywa na Wakala wa Majengo nchini.

Ukaguzi wa ufanisi katika ukadiriaji wa mahitaji na usambazaji wa dawa na vifaa tiba muhimu umeainisha madhaifu yafuatayo:

Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoweka kipaumbele mipango ya shughuli za makisio ya mahitaji

Ukokotoaji wa makisio ya mahitaji ya dawa na vifaa tiba muhimu unafanyika kama shughuli inayojitegemea na bila kushirikishwa kwenye hatua muhimu ya uandaaji wa Mpango wa Kina wa Afya wa Halmashauri ambao mara nyingi unafuata hatua zinazofanana za upangaji na ukisiaji wa mahitaji ya dawa na vifaa tiba muhimu. Moja

kati ya sababu za kutotumia fursa ya mipango ya kina ya Halmashauri ya Wilaya ni kuwa miongozo ya Afya haikugusia mambo ya ukadiriaji wa mahitaji kama Bohari Kuu ya Madawa inavyoelekezwa.

Muundo wa Mipango ya Kina ilitoa muongozo wa namna vituo vya afya vinavyoweza kuandaa bajeti zao kwa ajili ya mahitaji yao ya dawa na vifaa tiba muhimu kwa kuzingatia matumizi yaliyopita. Hivyo makisio ya mahitaji katika Halmashauri ya wilaya yalikuwa yanafanywa na wafamasia wa wilaya wakisaidiwa na maafisa afya waandamizi wa vituo vya afya bila kujadiliwa na uongozi wa kamati ya afya ya wilaya kama ilivyofanyika katika utengenezaji wa mipango ya afya.

Halmashauri Kutokufanya makisio ya mahitaji kwa kiwango cha kutosha

Wastani wa asilimia 50 wa ripoti za makisio ya mahitaji ya dawa na vifaa tiba muhimu kutoka mamlaka za Serikali za mitaa hazikupelekwa kwenye Ofisi za Kanda za Bohari Kuu ya Madawa za kanda. Jedwali 3.5 linaonyesha kiwango cha uwasilishaji wa ripoti hizo kutoka mamlaka za serikali za mitaa kwenda ofisi za kanda za Bohari Kuu ya Madawa katika miaka mitatu ya fedha 2010/11 hadi 2012/13.

Zahanati na Vituo vya Afya katika ngazi ya msingi hazifanyi kabisa makisio ya mahitaji ya dawa na vifaa tiba muhimu. Makisio yanaanzia katika ngazi ya mfamasia wa wilaya ambako taarifa za mahitaji yao zinakusanywa kupitia fomu za matumizi na taarifa zinakokotolewa.

Jedwali 3.5: Uwasilishaji wa ripoti za Makisio ya dawa na vifaa tiba ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda ofisi za kanda za Bohari Kuu ya Madawa kwa kipindi cha miaka mitatu ya fedha 2010-2013.

Kanda	Idadi ya ripoti zinazohitajika	Idadi halisi ya ripoti zilizowasilishwa	Asilimia ya ripoti zilizowasilishwa
Dar es salaam	30	3	10
Tanga	24	6	25
Mwanza	111	111	100
Tabora	30	30	100
Dodoma	33	0	0
Mtwara	42	0	0
Iringa	33	0	0
JUMLA KUU	303	150	50

Chanzo: Mahojiano na Mameneja wa Kanda Zilizotembelewa

Mamlaka za serikali za mitaa zinazohudumiwa na kanda za Mwanza na Tabora ziliwasilisha ripoti zao kama inavyotakiwa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohudumiwa na kanda za Tanga na Dar es Salaam hawakuwasilisha kadiri inavyotakiwa. Aidha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohudumiwa na Kanda za Dodoma, Mtwara na Iringa hazikuwasilisha ripoti yoyote. Ilionekana pia kwamba kulikuwa hakuna mfumo yakinifu kwa Bohari Kuu ya Madawa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu njia sahihi na yenye usanifu ufanisi wa kupata taarifa sahihi za matumizi ya dawa na vifaa tiba muhimu kutoka mamlaka za Serikali za Mitaa. Hii imesababisha baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa kuchelewa kuwasilisha au kutowasilisha kabisa taarifa hizo.

Vigezo Vichache kutumika wakati wa kufanya makisio

Baadhi ya vigezo vikuu vinavyotumiwa na Bohari Kuu ya Madawa wakati wa ukadiriaji wa makisio ya mahitaji ni pamoja na takwimu za huduma inayotolewa katika sekta ya afya, taarifa za maradhi, idadi ya watu na utumiaji wa dawa na makadirio ya utumiaji wa dawa. Hata hivyo, Bohari Kuu ya Madawa imekuwa ikitumia taarifa za mauzo kukokotoa viwango vya makisio ili kukadiria matumizi kwa mwaka unaofuata.[2] Matumizi ya taarifa za mauzo kutoka katika ofisi

[2] Bohari Kuu ya Dawa: Muongozo wa Uhakiki Ubora sehemu ya 4.1

za kanda za Bohari Kuu ya Madawa yamesababisha kuwa na makadirio ya juu au ya chini ya viwango vya makisio halisi ya mahitaji ya dawa. Hii ni kwa sababu makadirio hayo yanafanyika kwa kuzingatia mauzo yaliyofanywa katika mwaka uliopita bila kuzingatia madawa ambayo hayakupatikana wakati wa uagizaji na hivyo kushindwa kupelekwa katika vituo vya afya. Hii ilipelekea kuwa na viwango visivyo sahihi wakati kulinganisha viwango vilivyokisiwa na manunuzi au mauzo. Kama inavyonyeshwa katika Jedwali 3.6. Jumla ya dawa 15 zilichunguzwa. Hata hivyo kulikuwa na kukosekana kwa taarifa kwa dawa moja na hivyo uchambuzi ulifanyika kwa kuzingatia dawa 14.

Jedwali 3.6: Mlinganisho wa manunuzi sambamba na makisio yake kwa madawa 15 kwa miaka 2010-2013

Kundi	2010/2011	2011/2012	2012/2013	JUMLA
Wakati ambao makisio yalikuwa madogo kuliko manunuzi	4	5	0	9 (21%)
Wakati ambao makisio yalikuwa makubwa kuliko manunuzi	10	9	14	33 (79%)
JUMLA	14	14	14	42

Chanzo: Ripoti za makisio na manunuzi kutoka Ofisi za Bohari Kuu ya Madawa (2010-2013)

Kama ilivyoainishwa katika Jedwali 3.6 kati ya kesi[3] 42 zilizochunguzwa, kesi 33 (79%) zilikuwa na makisio ya dawa makubwa kuliko manunuzi yake na kesi 9 (21%) zilikuwa na kiwango cha makisio cha chini kuliko manunuzi.

Ukaguzi huu pia ulilinganisha viwango vilivyokisiwa na vile vya mauzo katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha 2010-2013 kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 3.7.

[3] Kesi za manunuzi ni wakati ambao mlinganisho ulifanywa kati ya kiwango kilichokisiwa na kiwango sambamba nacho kilichonunuliwa kwa kila aina moja husika ya dawa katika idadi ya dawa 15.

Jedwali 3.7: Mauzo yaliyofanyika kulinganisha na Makisio yake kwa dawa 15 katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha (2010/11-2012/13

Kundi	2010/2011	2011/2012	2012/2013	JUMLA
Wakati ambao makisu yalikuwa madogo kuliko mauzo	2	12	2	16
Wakati ambao makisio yalikuwa makubwa kuliko mauzo	12	2	12	26
JUMLA	14	14	14	42

Chanzo: Ripoti za Makisio na Mauzo kutoka Bohari Kuu ya Dawa 2010-2013

Jedwali 3.7 linaonyesha kwamba katika miaka miwili ya fedha 2010/11 na 2012/2013 idadi kubwa ya madawa yaliuzwa chini ya kiwango ikilinganisha na makisio yake. Kati ya kesi 42, ni kesi 26 (62%) zilionyesha kuwa na makisio makubwa kulinganisha na mauzo yake huku 38% zikionyesha kuwa na makisio madogo kuliko mauzo yake katika miaka mitatu. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilichunguza kiasi tofauti cha kesi ambazo kiwango cha makisio kilitofautiana na mauzo kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali 3.7

Ukaguzi pia ulichunguza uagizaji, uandaaji, na upelekaji wa oda za dawa na vifaa tiba muhimu katika ngazi tofauti kama inavyoonyeshwa hapa:

Kutopatikana kwa baadhi ya dawa na kusababisha kuwa na idadi kubwa ya oda za dawa

Wastani wa idadi ya oda za dawa yaliyofanywa na kila kanda kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12 ilikuwa ni 100. Hii ni sawa na oda 76 zaidi ya kiwango kinachotakiwa ambacho ni oda 24 tu kwa mwaka. Ilidhihirika kwamba kulikuwa na ongezeko la dawa zinazokosekana maghalani katika Bohari za Kanda na Bohari Kuu ya Madawa iliyopelekea kuwa na idadi kubwa ya oda zinazoletwa toka katika Vituo vya Afya na Hospitali za Mikoa na Wilaya. Kielelezo 3.1 kinaonyesha mlinganisho kati ya idadi ya oda zinazotakiwa na idadi halisi zilizofanyika kila kanda.



Kielelezo 3.1: Idadi ya oda za mahitaji na kiwango halisi cha oda zilizofanywa na kanda kwenda Bohari Kuu ya Madawa (2011/2012-2012/2013).

Kielelezo 3.1 kinaonyesha kwamba Bohari za Kanda zimekuwa zikitoa Oda nyingi za dawa kuliko kiwango ambacho kinatakiwa kwenda Bohari Kuu.

Muda mrefu wa kuandaa na Kupeleka Oda ya dawa kati ya Bohari Kuu na Bohari za Kanda

Jumla ya oda 216[4] zilizochaguliwa na timu ya ukaguzi ili kuweza kupata wastani[5] wa muda wa kuandaa na kusafirisha dawa na vifaa tiba muhimu kwa kulinganisha na muda uliowekwa wa siku 14 kwa ofisi za Bohari za Kanda kufanya kazi hiyo. Kielelezo 3.2 kinaonyesha matokeo ya ulinganisho huo.

[4] Agizo 1 kwa kila mwezi kupata jumla ya oda 12 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka 3 kwa kanda

[5] Ukokotoaji wa wastani wa muda wa kuandaa na kusafirisha oda ulipatikana kwa kujumlisha muda wote uliotumika kuandaa na kusafirisha maagizo yote 12 kwa kila kanda na kugawanya jumla kwa idadi ya maagizo 12



Kielelezo 3.2: Mlinganisho kati ya muda rasmi wa kuandaa na kupeleka oda za dawa na muda halisi uliotumika kuandaa oda hizo kusafirisha kutoka Bohari Kuu kwenda Bohari za Kanda

Kielelezo 3.2 kinaonyesha kwamba idadi kubwa ya oda za dawa zilisambazwa katika kanda husika nje ya muda unaotakiwa. Kati ya kesi 18[6] zilizochunguzwa ni 7 tu (39%) zilizofanyika ndani ya muda rasmi wa siku 14 au chini ya hapo wakati 11(61%) zilicheleweshwa kwenda katika Kanda.

Katika mwaka 2011/2012, oda kutoka makao makuu ya Bohari Kuu ya Madawa kwenda katika kanda zilichukua wastani wa siku 15 kutoka siku ya kuwasilisha oda mpaka kupatikana kwake. Kwa mwaka 2012/2013 oda zilichukua wastani wa zaidi ya siku 46 kuandaliwa na kupelekwa katika kanda husika. Kanda ya Tanga ilikuwa na kiwango kikubwa zaidi cha ucheleweshaji ambapo kwa wastani oda zao ziliandaliwa kwa muda wa siku 71, ikimaanisha kwamba oda zao zilichelewa kwa siku 57.

[6] Kesi moja inawakilisha mwaka mmoja wa fedha kwa kanda na kesi tatu kwa kila kanda kwa kanda sita.

Uchambuzi wa "muda wa kuandaa oda" na "muda wa kupeleka" ili kuweza kutambua ni nini kinasababisha ucheleweshaji kutoka kuwasilishwa kwa oda kwenda Bohari Kuu ya Madawa mpaka inapopokelewa katika kanda husika imeainishwa katika Kielelezo 3.3



Kielelezo 3.3: Mlinganisho kati ya muda wa kuandaa na kupeleka oda za dawa kati ya Bohari Kuu ya Madawa na zile za Kanda (2010-2013)

Kielelezo 3.3 kinaonyesha kwamba kati ya oda 18 zilizochunguzwa, 11 (61%) zilichukua muda mrefu kuziandaa kuliko kuzipeleka, na oda 7 (39%) muda wa kuzisafirisha ulizidi ule wa kuzitayarissha. Hii ina maana kwamba oda kutoka Bohari Kuu zinazopelekwa katika kanda zilichukua muda mrefu zaidi kwenye kuandaa kuliko kusafirisha. Kupitia mahojiano yaliyofanywa na maafisa wa Bohari Kuu ya Madawa, muda mrefu zaidi wa kuandaa mahitaji ulitokana na kubadilishwa kwa mfumo wa ndani wa mawasiliano kutoka ule wa zamani wa ORION kwenda mpya wa EPICOR 9. Kipindi hicho vipengele vingi vya mfumo huo havikufanya kazi kwa ufanisi.

Muda mrefu zaidi wa kuandaa oda ulionekana katika kanda ya Tanga ambapo ilichukua wastani wa zaidi ya siku 66 kuandaa oda moja kwenda Bohari Kuu ya Madawa katika mwaka wa fedha

2012/13. Kanda za Iringa na Mtwara zilichukua muda mfupi zaidi katika miaka ya fedha 2010/11 na 2011/12 kwani oda zake ziliandaliwa kwa wastani wa siku 1 tu. Ilionekana pia kwamba oda kutoka kanda ya Dodoma zilichukua muda mrefu zaidi kuandaliwa katika Bohari Kuu ya Madawa kwa wastani wa siku 32 kwa kipindi cha miaka mitatu ya fedha 2010-2013. Kwa ujumla ilichukua muda mfupi zaidi kupeleka oda kuliko kuziandaa oda za kutoka mkoa wa Tabora zilipelekwa haraka zaidi kwa wastani wa siku moja tu katika mwaka wa fedha 2010/11.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pia ilifanya uchambuzi kuonyesha kwa ujumla uwiano wa oda kwa kila kundi katika Bohari Kuu ya Madawa Kielelezo 3.4 kinaonyesha uwiano wa oda katika Bohari Kuu ya Madawa kwa kuzingatia muda uliochukua kuanzia pale oda inapoandaliwa na kusafirishwa kwenda katika kanda husika.



Kielelezo 3.4: Uwiano wa idadi ya oda kulingana na muda uliochukua kuandaliwa na kupelekwa kutoka Bohari Kuu kwenda Bohari za Kanda

Kielelezo 3.4 kinaonyesha kwamba zaidi ya nusu ya oda (54%) zilizopokelewa katika Bohari Kuu ziliandaliwa na kusafirishwa kwa muda wa zaidi ya siku 14. Asilimia 46 ndio ziliandaliwa na kusafirishwa ndani ya muda rasmi wa siku 14.

Upelekaji wa oda nje ya muda kutokana na kuandaliwa kwa muda mrefu zaidi

Wastani wa muda wa kuandaa na kusafirisha oda za dawa uliotumiwa na Kanda tano kwa kuzingatia idadi ya oda ziliyofanywa na vituo vya afya chini ya Mfumo Jumuishi wa Ugavi ni kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 3.8

Jedwali 3.8: Upelekaji wa Oda kwenda katika vituo vya Afya kutoka katika kanda tano zilizotembelewa 2012/2013.

KANDA	Idadi ya Maagizo yaliyochunguzwa	Uwiano wa maagizo yaliyocheleweshwa (%)	Wastani wa Kuchelewa (siku)
MWANZA	32	91	30
TANGA	28	100	25
DODOMA	32	40	5
MTWARA	28	14	3
IRINGA	28	100	44
WASTANI		69	21

Chanzo: Rejesta za oda, vitabu vya Stoo za Vituo vya Afya, ankara za mauzo, leja za MTUHA.

Jedwali linaonyesha kwamba kuna uwiano mkuwa wa kiwango cha oda ambazo zinapelekwa nje ya muda uliopangwa. Kwa wastani katika kanda tano zilizotembelewa, asilimia 69 ya oda zilizopokelewa kutoka vituo vya afya hazikupelekwa kwa wakati huku asilimia 31 ya oda zikipelekwa kwa wakati. Oda zote kutoka katika kanda ya Tanga na Iringa hazikupelekwa kwa wakati kwenda vituo vya afya. Wastani wa ucheleweshwaji wa oda za dawa katika mikoa yote mitano ulikuwa ni siku 21.

3.3 Uratibu hafifu wa wadau muhimu

Ripoti zote za uchambuzi wa kaguzi za ufanisi zilizotolewa zimeonyesha madhaifu katika uratibu wa wadau muhimu katika ripoti zote. Kwa mfano, mfumo wa kusimamia mipango miji hujumuisha wadau mbalimbali kama vile : Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Mamlaka ya Uendelezaji Miji. Nyingine ni Wakala za Huduma, Mashirika ya Umma, Taasisi zisizo za Kiserikali pamoja na watu binafsi wakiwemo wamiliki wa ardhi.

Kuna mapungufu katika kuhusisha wakala/taasisi za serikali zilizopewa jukumu la kutoa huduma muhimu kama vile maji, umeme na barabara wakati wa kuandaa mipango kabambe ya kuendeleza miji, licha ya kuwa taasisi hizi zina wajibu wa kuchangia wakati wa utekelezaji wa mipango hiyo.

Ukaguzi ulibaini kwamba sababu kubwa ya ushiriki mdogo wa wadau ni kukosekana kwa uratibu mzuri wa uandaaji na utekelezaji wa mipango miji baina ya Mamlaka za Mipango Miji na Taasisi mbali mbali nchini. Mamlaka za mipango miji ziliandaa mipango miji yao bila ya kuzishirikisha tasisi mbalimbali ambazo zinawajibu wa kutoa huduma za msingi kwa jamii. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilibaini pia utendaji kazi wa taasisi hizo kama vile Shirika la Simu, Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka,Shirika la Umeme na Wakala wa Barabara nchini ulitegemea uwepo wa mpango miji mzuri kwani kuna kutegemeana baina yao haswa katika uwekaji na ukarabati wa miundo mbinu ya utoaji huduma. Hata hivyo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilibaini kwamba taasisi hizo zilifanya shughuli zake kila moja peke yake na hii ilitokana na kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa mipango miji.

Ukaguzi wa ufanisi wa ukarabati wa majengo ya Serikali ulibaini kwamba mikakati kuhusu ukarabati wa majengo ya Serikali katika Mipango Mkakati ya Wakala wa Majengo ya mwaka 2007-2012 na ule wa 2012-2017 haikuweka bayana namna ambavyo uratibu wa rasilimali zilizopo na upatikanaji wa wataalamu pamoja na wadau husika utakaofanyika katika eneo hili la ukarabati wa majengo.

Kwa mfano, lengo namba 3 la Wakala wa Majengo katika Mpango mkakati wake wa 2012-2017 ni "*kuhakikisho kwamba mali za Serikali zinakarabatiwa na kutumika kulingana na kanuni za majengo ya Serikali".* Hata hivyo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilibaini kwamba kanuni hizo za majengo ya serikali zilizoainishwa katika lengo hilo hazikuwepo. Hivyo Wakala wa Majengo walikuwa wakipanga kukarabati majengo ya serikali kwa kutumia kanuni wakati hakukuwa na nyaraka zozote zile ambazo zilikuwa na kanuni hizo.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pia ilibaini kwamba baadhi ya mikakati kuhusu ukarabati wa majengo ya Serikali haikuratibiwa vya kutosha. Lengo la 6 katika Mpango Mkakati wa Wakala wa Majengo wa mwaka 2012-2017 linanuia kuandaa na kutekeleza miongozo ya ukarabati wa majengo 40 yanayotumiwa na Wizara, Idara, Wakala zote za Serikali na Serikali za Mitaa ifikapo tarehe 30 Juni 2012.

Hata hivyo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilibaini kwamba hakukuwa na mpango mmoja unaofahamika kati ya Wakala wa Majengo na Wizara, Idara, Wakala za Serikali na Serikali za Mitaa kama wadau wakuu wa kazi za ukarabati wa majengo. Wakala wa Majengo alipanga kuandaa na kutekeleza miongozo ya matengenezo kwa Wizara, Idara na Wakala za Serikali bila makubaliano yoyote yale baina yao kuhusu utekelezaji wa shughuli za ukarabati wa majengo.

Taasisi hizo za Serikali ama walikuwa na idara zao binafsi za usimamizi wa mali zisizohamishika au vitengo vinavyojitegemea vilivyohusika na mambo ya ukarabati wa majengo yaliyopo chini yao au yale wanayoyatumia kwa kipindi hicho.

3.4 Ufuatiliaji na utathmini

Ufuatiliaji na tathmini hafifu zisizotosheleza ni udhaifu mwingine mkubwa ambao umejirudia katika ripoti zote tatu zilizowasilishwa kama ilivyoelezwa katika ripoti hii ya jumla.

Ufuatiliaji na tathmini usioridhisha umebainika katika ukaguzi wa usimamizi wa mipango miji.

Ukaguzi wa ufanisi ulichunguza ni kwa kiasi gani Wizara ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinafuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya mipango miji nchini.

Katika Wizara ya Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilionekana kwamba ufuatiliaji ulikuwa ukifanywa kwa kila kipindi cha robo mwaka kupitia ripoti zilizowasilishwa baada ya ziara mbali mbali zilizofanywa na watendaji wa Wizara katika Halmashauri za Wilaya nchini. Divisheni ya Mipango ya Ardhi na Vijiji kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Maendeleo ya Ardhi hufanya ufuatiliaji wa shughuli za mipango miji na vijiji kwa nchi nzima. Hata hivyo hakuna viashiria vya ufuatiliaji, vigezo au makabrasha yaliyotengenezwa kupima matokeo yaliyokusudiwa. Matokeo yake, ripoti za ufuatiliaji

zilizokuwa zikitolewa zilikuwa zikionyesha changamoto chache ambazo Mamlaka za Mipango Miji zinakabiliana nazo, badala ya kuonyesha jinsi gani malengo au madhumuni yaliyowekwa na divisheni yamefikiwa kama ilivyotakiwa na miongozo ya uandaaji wa mipango ya uendelezaji wa miji nchini.

Katika Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilionekana kwamba ufuatiliaji ulikuwa ukifanywa kwa mamlaka za serikali za mitaa kupitia ziara mbali mbali zinazofanywa na kupitia ripoti za mwaka. Hata hivyo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilibaini kwamba, baadhi ya mamlaka za mipango miji hazikujua uwepo wa Divisheni ya Mipango Miji chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na majukumu ya Divisheni hiyo. Hii inaonyesha kwamba utendaji kazi wao kwa kuangalia mipango miji haukuwa ukifuatiliwa. Katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, timu za Usimamizi za Wilaya zilitakiwa kufuatilia na kutoa ripoti ya utekelezaji wa mipango ya uendelezaji miji kwa kila robo mwaka, kwa kuhakikisha kwamba Kamati za wataalamu kwa kushirikiana na ofisi za kata zinafuatilia utekelezaji wa mipango ya kina iliyopitishwa.

Lakini ilibainika kwamba Mamlaka za Upangaji Miji zilizotembelewa hazikutoa ripoti kuhusu utekelezaji wa miradi ya mipango miji yao kwa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha Divisheni ya Mipango Miji na Ardhi haikufuatilia hali ya utekelezaji wa mipango hiyo.Hakukuwa na tathmini zozote za nusu mwaka au mwisho wa mwaka zilizofanywa na Mamlaka za Mipango Miji kuhusu kiwango cha utekelezaji wa Mipango ya uendelezaji wa miji chini ya mamlaka zao.

Ufuatiliaji wa mamlaka za mipango miji unaofanywa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi haukuzingatia viashiria vya utendaji. Hata pale ambapo ufuatiliaji ukifanywa kwa kushirikiana baina ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hiyo na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hakukuwa na mrejesho wowote uliotolewa kwa mamlaka husika za mipango miji.

Katika ukaguzi wa ufanisi wa Usimamizi wa Ukarabati wa Majengo ya Serikali ilibainika kwamba Wizara ya Ujenzi kama msimamizi mkuu wa shughuli za Wakala wa Majengo haijafuatilia na kutathmini

kikamilifu ukarabati wa majengo ya serikali. Matokeo yake, dhamira ya Wakala wa Majengo ya kutoa huduma bora ya makazi na ofisi kwa watendaji wa Serikali katika ngazi haijafikiwa.

Madhaifu yameonekana katika mipango na utekelezaji wa ufuatiliaji na tathmini kama ifuatavyo:

i) **Hakuna mipango inayozingatia viashiria hatarishi katika kutathmini utendaji wa Wakala wa Majengo kwa mambo yahusuyo ukarabati wa majengo ya serikali;**
ii) **Hakuna tathmini, zenye kuangalia ufanisi wa programu za ukarabati wa majengo ya Serikali, Idadi na ujuzi wa wafanyakazi, utoshelezi wa zana na vitendea kazi vingine na kiwango cha ujuzi wa mafundi waliopo kwenye ofisi husika;**
iii) **Hakukuwa na ushahidi wa mawasiliano ya matokeo ya tathmini ya utendaji wa Wakala wa Majengo;**
iv) **Hakukuwa na mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu za majengo ya Serikali ili kusaidia kuboresha usimamizi na kuandaa mipango mingine ya maendeleo ; na**
v) **Hakuna sera ya ukarabati wa majengo iliyosambazwa kwa taasisi na watumiaji wa majengo ya serikali ili kuwa na mfumo mmoja wa ukarabati wa majengo ya serikali nchi nzima.**

Ukaguzi wa ufanisi katika Ukisiaji na Usambazaji wa Dawa na Vifaa Tiba Muhimu ulibaini kwamba, Kitengo cha Huduma za Madawa cha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hakina mpango wa kina wa kufuatilia usambazaji wa na utendaji mfumo mzima wa ugavi wa dawa na vifaa tiba muhimu kwa nchi nzima. Pia viashiria vichache vilivyowekwa na kutumika kufuatilia upatikanaji wa dawa muhimu kama inavyotajwa katika Mkakati wa Kitaifa wa III wa Sekta ya Afya havijafanyiwa kazi na hivyo haviwezi kuchangia kuboresha upatikanaji wa dawa nchini. Tatizo hili linakuzwa na ukosefu wa miongozo ya kufuatilia na kusambaza Madawa na Vifaa Tiba Muhimu.

Ufuatiliaji wa shughuli za usambazaji ndani ya Bohari Kuu ya Madawa haujafanywa kwa kiwango cha kutosha kutokana na idadi ndogo ya viashiria katika kupima tija wakati wa usambazaji; kutokuwepo kwa miongozo yenye kutoa muelekeo wa kufuatilia utendaji wa shughuli za usambazaji; na kukosekana kwa mipango ya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Bohari Kuu ya Madawa

katika shughuli hizo za usambazaji wa madawa na vifaa tiba muhimu .

3.5 Upatikanaji wa fedha usiotegemewa wa shughuli zilizopangwa

Katika ukaguzi wa Usimamizi wa Mipango Miji ilibainika kwamba fedha zilizotolewa chini ya kiasi kinachohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za mipango miji kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uchambuzi wa matumizi katika kipindi cha nusu mwaka unaonyesha kuwa, Halmashauri zilitegemea matumizi mengineyo, vyanzo binafsi, na asilimia 30 ya kodi za ardhi kama vyanzo vya mapato ili kuendeshea shughuli za mipango miji. Taarifa za matumizi ya Halmashauri hizo na mahojiano yaliyofanywa na maafisa wa Halmashauri hizo yalionyesha kwamba, huduma nyingi za ardhi zinatolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa isipokuwa zile tu za usajili wa hati za umiliki wa ardhi ambao unaofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hata hivyo, Wizara hiyo inachukua asilimia 70 ya kiasi cha kodi ya ardhi kinachokusanywa, na mara nyingi haikurudisha asilimia 30 ya kodi ya ardhi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kama utaratibu unavyotaka.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilibaini pia kuwa hata pale ambapo asilimia 30 ya kodi iliporudishwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, haikupelekwa kwa wakati. Ilichukua zaidi ya miezi 6 kabla fedha hizo hazijatumwa. Hii iliathiri utekelezaji wa kazi za mipango miji na pia ni kinyume cha muongozo wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi unaotaka Wizara hii kutoa asilimia 30 ya kodi ya ardhi kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili yakutekeleza shughuli za mipango miji. Jambo hili lilionekana katika mamlaka zote za upangaji wa miji ambazo zilitembelewa na timu ya ukaguzi. Hata hivyo wakati wa ukaguzi ilibainika kwamba, toka mwaka 2012 hakuna ripoti za robo mwaka ambazo zimetumwa kwenda Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye kuainisha matumizi ya asilimia 30 ya kodi ya ardhi kama muongozo wa Wizara unavyotaka.

Kadhalika ilionekana kwamba vyanzo binafsi vya mapato kwa mamlaka nyingi za Upangaji wa Miji havikutosha kugharamia mahitaji ya msingi ya uendeshaji, uandaaji na utekelezaji wa mipango miji iliyoandaliwa. Hata hivyo, kuanzia mwaka wa fedha

2012/13 kiasi kinachotengwa kwa matumizi mengineyo kiliongezeka kutoka shilingi milioni 5.4 hadi shilingi milioni 12 kwa mwaka.

Ukaguzi wa ufanisi katika Usimamizi wa Ukarabati wa Majengo ya Serikali ulibaini kuwapo kwa kiwango kidogo cha bajeti inayotengwa kwa ajili ya shughuli za ukarabati wa majengo ya Serikali. Ukaguzi ulichambua bajeti ilivyotengwa kwa ajili ya kazi za ukarabati majengo ya Serikali na kubaini kwamba ni kiasi kidogo sana kinachotengwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya serikali ikilinganishwa na bajeti nzima ya Wakala wa Majengo (Jedwali 3.9).

Jedwali 3.9: Kiasi cha bajeti kinachotengwa (Matumizi tarajiwa) kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya serikali.

Mwaka wa fedha	Bajeti ya Jumla ya Shirika (Shilingi Bilioni)	Bajeti inayotengwa kwa shughuli za ukarabati (Shilingi Milioni)	Asilimia ya bajeti ya ukarabati kati ya bajeti kuu
2010/2011	67	267	0.4
2011/2012	55	300	0.5
2012/2013	73	300	0.4

Chanzo: *Mipango kazi ya Wakala wa Majengo (2010-2013)*

Jedwali 3.9 linaonyesha kwamba katika kipindi cha miaka mitatu, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo haikuzidi asilimia 0.5 ya bajeti kuu ya Wakala wa Majengo. Zaidi ya asilimia 25 ya kipato cha Wakala wa Majengo kinachotokana na vyanzo binafsi kinapatikana kutokana na makusanyo ya kodi za upangishaji. Hata hivyo bajeti inayotengwa kwa ajili ya shughuli za ukarabati imekuwa ndogo kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 3.9. Mahojiano na Maafisa wa Ofisi za Wakala zilizoko mikoani na kutoka Kurugenzi ya Usimamizi wa mali zisizohamishika waliopo Makao Makuu ya Wakala wa Majengo yalieleza kwamba, fedha zinazotengwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo zilikuwa hazitoshelezi ukilinganisha na hali halisi ya majengo yaliyopo.

Uchambuzi wa kiwango cha utoaji fedha kwa shughuli za ukarabati wa majengo ulivyofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ulibaini kupungua kwa ruzuku ya Serikali kutoka Wizara ya Ujenzi kwa ajili ya shughuli za ujenzi na ukarabati pamoja na kodi za upangaji zinazodaiwa kwa Wizara, Idara na Wakala za Serikali kulivyoathiri

kiwango cha bajeti inayotengwa kwa ajili ya shughuli za ukarabati wa majengo. Kwa mfano ilibainika kwamba, ruzuku ya serikali kwa ujenzi na ukarabati wa majengo ya serikali ilipungua kutoka shilingi bilioni 2.2 kwa mwaka 2006/2007 mpaka kutokutengwa kwa fedha yeyote mnamo mwaka 2013/14.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilibaini pia kwamba, kiasi cha fedha ambacho Wizara ya Ujenzi imekuwa ikitoa kimekuwa chini ya wastani kwa kipindi cha miaka minne iliyopita na hali hii imechangia kupungua kwa fedha inayotengwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Serikali. Kiasi kinachotolewa na Wizara ya Ujenzi kimekuwa chini ya wastani kwa miaka minne kuanzia 2010/11 – 2013/14 kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo 3.5



Kielelezo 3.5: Mwenendo wa ruzuku ya Serikali kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya serikali kwa kipindi cha miaka ya fedha 2006/2007 hadi 2013/2014

Ukaguzi wa ufanisi katika ukadiriaji wa mahitaji wa mahitaji na Usambazaji wa Dawa na Vifaa Tiba Muhimu ulibaini uwepo wa mtiririko usio ridhisha (kinyume na ilivyopangwa) wa fedha kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa ajili ya ununuzi wa dawa za vituo vya afya vya Serikali. Serikali ilitoa fedha chini ya asilimia 10 ya fedha zote zilizohitajika katika mikupuo 8 kati ya 12 katika mwaka wa fedha 2012/13 kama ilivyoonyeshwa katika **Kielelezo 3.6**



Kielelezo 3.6: Kiwango cha fedha zilizotolewa katika kila mkupuo kutoka Wizara ya Afya mwaka 2012/13 kwa manunuzi ya dawa na vifaa tiba muhimu

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilibaini mtiririko usio eleweka (kinyume na mpango wao wa awali) wa utoaji wa fedha kwa ajili ya manunuzi ya dawa na vifaa tiba. Kielelezo 3.6 hapo juu kinaonyesha kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Bohari Kuu ya Madawa hazikupata fedha za manunuzi ya dawa na vifaa tiba kwa wakati unaotakiwa.

Uchunguzi wa mwenendo kati ya Mtaji wa Biashara na deni la serikali kwa Bohari Kuu ya Madawa (2008-2013) ni kama ilivyoonyeshwa katika Kielelezo namba 3.7



Kielelezo 3.7: Mtaji wa Biashara wa Bohari Kuu ya Madawa dhidi ya Deni la Serikali

Kielelezo 3.7 kinaonyesha kupungua kwa mtaji wa biashara wa Bohari Kuu ya Madawa kwa zaidi la zaidi ya asilimia 69 katika kipindi cha miaka 5, kutoka shilingi bilioni 81 mwaka 2008 hadi shilingi bilioni 25 mwaka 2013. Kutetereka huko kwa mtaji wa Bohari Kuu ya Madawa ni matokeo ya kuongezeka kwa deni la Serikali. Deni ambalo serikali inadaiwa limeongezeka zaidi ya mara 4 katika kipindi cha miaka 6, kutoka shilingi bilioni 14 mwaka 2008 hadi shilingi bilioni 69 mwaka 2014.

3.6 Hitimisho la jumla kwa madhaifu yanayojirudia

Uchambuzi wa mambo yanayojirudia kama yalivyoonekana katika ripoti tatu za ufanisi zilizofanyika zinahitimisha kwamba, baadhi ya madhumuni ya serikali hayatafikiwa kutokana na madhaifu yaliyobainika wakati wa kaguzi hizo. Madhaifu yaliyobainika ni pamoja na mipango hafifu ya kuongoza maendeleo ya miji/ madhaifu katika uwasilishaji oda, uandaaji, usafirishaji wa oda za dawa na vifaa tiba muhimu; uratibu usioridhisha wa wadau wakuu, ufuatiliaji na utathmini, na mtiririko na upatikanaji hafifu wa fedha kwa shughuli zinazopangwa zinaleta athari katika kufikia uwekevu, tija na ufanisi katika programu za serikali, miradi na shughuli nyinginezo.

3.7 Mapendekezo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu

Uchambuzi huo hapo juu na hitimisho la jumla linatufanya tutoe mapendekezo yafuatayo kwa ajili ya kuboresha hali ya baadae katika utendaji wa shughuli za Serikali:

3.7.1 Mipango na Bajeti

Ofisi ya Waziri Mkuu inatakiwa kuhakikisha kwamba taasisi zote za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zinafanya yafuatayo ili kuboresha mipango na bajeti za shughuli za Serikali:

- shughuli zote muhimu zinatambulika na mpango kazi wa kina unaandaliwa;
- uchambuzi wa vihatarishi unazingatiwa wakati wa upangaji ili kuelekeza rasilimali katika namna ambayo inazingatia uwekevu, tija na ufanisi; na
- mgawanyo wa rasilimali unafanywa kwa kuzingatia mahitaji ya msingi, vipaumbele na vihatarishi vilivyomo.

3.7.2 Uratibu kati ya wadau muhimu

Ofisi ya Waziri Mkuu inatakiwa kuhakikisha kwamba taasisi zote za Serikali Kuu na za Mitaa zinafanya yafuatayo linapokuja suala la uratibu kati ya wadau muhimu wakati wa utekelezaji wa programu za serikali:

- kuna mfumo wenye ufanisi wa kutathmini utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Serikali; na
- unawekwa mfumo na madhubuti wa kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya idara, divisheni katika ngazi ya taasisi ili kuboresha ufanisi wake.

3.7.3 Mgawanyo wa Rasilimali

Ofisi ya Waziri Mkuu inatakiwa kuhakikisha kwamba taasisi zote za Serikali Kuu na za Mitaa zinafanya yafuatayo kuhusu suala la mgawanyo wa rasilimali:

- kuna mifumo inayoeleweka na iliyo wazi katika kukusanya na kugawa rasilimali kwa shughuli na sekta mbalimbali za serikali; na
- mgawanyo wa rasilimali unafanywa kwa kuzingatia vipaumbele na vihatarishi vilivyowekwa.

3.7.4 Ufuatiliaji, Utathmini na taarifa za utekelezaji

Ofisi ya Waziri Mkuu inatakiwa kuhakikisha kwamba taasisi zote za Serikali Kuu na za Mitaa zinafanya yafuatayo kuhusu suala la ufuatiliaji, tathmini na uandaaji wa taarifa za utekelezaji:

- **kuhakikisha kwamba taasisi zote za serikali zimeandaa viashiria vikuu vya utendaji na vipimo vya kutathmini utendaji wao;**
- **kufuatilia na kutathmini mara kwa mara utendaji wa taasisi zote za Serikali nchini ili kuhakikisha kwamba mipango ya ufuatiliaji na tathmini iliyowekwa inatekelezwa kwa usahihi na ripoti za utekelezaji zinatolewa kama ilivyopangwa; na**
- **kuweka mfumo yakinifu maalum wa kina na rasmi wa kitaifa kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa shughuli/programu za Serikali katika ngazi ya taifa.**

SURA YA NNE

KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA KATIKA RIPOTI YA UFANISI YA KUZUIA NA KUDHIBITI ATHARI ZA MAFURIKO

4.1 Usuli wa Ukaguzi

Ripoti ya ufanisi inayohusu kuzuia na kukabiliana na athari za mafuriko katika ngazi ya Serikali Kuu na Mitaa nchini kufuatia mafuriko yaliyowahi kutokea Babati iliwasilishwa Bungeni mnamo mwezi wa saba mwaka 2007. Wakaguliwa wakuu walikuwa Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa, Ofisi ya Katibu Tawala wa mkoa wa Manyara, na Halmashauri ya Mji na Wilaya ya Babati.

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini jinsi Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa, Ofisi ya mkoa wa Manyara , Halmashauri za Mji na Wilaya ya Babati na Wakala wa Barabara nchini walivyotekeleza sheria, kanuni, taratibu za kimkakati katika usimamizi wa kupunguza na kuzuia athari za mafuriko.

Ukaguzi ulilenga matukio ya mafuriko yaliyotokea tangu mwezi Januari, 1990 hadi Desemba, 2005 katika mji wa Babati. Ukaguzi ulizingatia majukumu yanayotakiwa kutekelezwa na Mkuu wa Idara ya Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu na Maafisa wengine wa ngazi za chini ikijumuisha maofisa wa ofisi ya Mkoa wa Manyara na Halmashauri ya Wilaya ya Babati katika suala zima la kuzuia na kukabiliana na athari za mafuriko. Ukaguzi uliangalia zaidi usimamizi na utunzaji wa miundombinu ya kuzuia na kukabiliana na athari za mafuriko katika mji wa Babati.

Katika ukaguzi huo ilibainika kuwa, kulikuwa na uwezekano wa kuendelea kuwepo hatari zitokanazo na mafuriko na hivyo zinahitajika njia muafaka za kujikinga zaidi na mafuriko yanayoweza kutokea. Hii inatokana na uhaba na ubovu wa miundombinu ya kupitisha maji katika mji wa Babati, uwepo wa makazi ya watu katika maeneo hatarishi, kutokufanya ukarabati wa miundombinu iliyopo katika barabara ya Minjingu-Dodoma na kutokujiandaa kwa wahusika wanaosimamia masuala ya maafa. Pamoja na mafuriko kujirudia katika maeneo ya Babati na maeneo mengine ya nchi kwa zaidi ya miaka kumi, ukaguzi ulibaini kuwa

Ofisi ya Waziri Mkuu-Idara ya Maafa haijaandaa rejesta (mfumo wa kuhifadhia kumbukumbu) ambayo ingetumika katika kuandaa mipango mikakati ya kuzuia na kukabiliana na athari za mafuriko nchini.

Hivyo ukaguzi ulihitimishwa kuwa, Tawala za Mkoa, Halmashauri ya mji na Wilaya ya Babati hazijachukua tahadhari za kutosha za kuiweka miundombinu ya kuzuia na kukabiliana na athari za mafuriko.

4.2 Matokeo ya ufuatiliaji ya utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa

4.2.1 Matokeo ya jumla ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa

Kwa ujumla mapendekezo 10 kati ya 19 yalitekelezwa kikamilifu, mapendekezo 6 yalitekelezwa kwa kiasi na mapendekezo 3 hayakutekelezwa kabisa. Hii inajionyesha katika Kilelezo namba 4.1



Kielelezo 4.1: Utekelezaji wa jumla wa mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi

Ukaguzi ulithibitisha kuwa Wakala wa Barabara nchini imetekeleza mipango yake ili kuzuia mafuriko Babati. Hata hivyo kuna mapendekezo ambayo hayajafanyiwa kazi na Idara ya Maafa katika ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Tawala na Mkoa wa Manyara, na Halmashauri ya Mji na Wilaya ya Babati (**Jedwali 4.1**).

Jedwali 4.1: Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi kwa taasisi moja moja zilizokaguliwa

Na	Taasisi iliyokaguliwa	Mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu	Mapendekezo yaliyotekelezwa kwa kiasi	Mapendekezo ambayo hayakutekelezwa	Jumla
1	Ofisi ya Waziri Mkuu-Idara ya Maafa	0	3	1	4
2	Ofisi ya Katibu Tawala za Mkoa-Manyara	2	1	0	3
3	Halmashauri ya Mji/Wilaya Babati	3	2	2	7
4	Wakala wa Barabara	5	0	0	5
	Jumla	**10**	**6**	**3**	**19**

***Chanzo**: Taarifa kutoka kwenye taasisi husika na uchambuzi uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, 2015*

Jedwari 4.1, linaonyesha mapendekezo 3 ambayo hayakutekelezwa, mapendekezo 6 yaliyotekelezwa kwa kiasi na mapendekezo 10i yaliyotekelezwa kikamilifu.

4.2.2 Mapendekezo ambayo hayakutekelezwa

Pendekezo 3.2: Kuweka Mpango Kabambe unaozingatia vigezo hatarishi

Wakati ukaguzi ulipofanyika mwaka 2007, ilibainika kuwa mpango kabambe wa mji wa Babati haukulipa kipaumbele suala la mafuriko yaliyokuwa yakitokea mara kwa mara katika mji wa Babati. Baadhi

ya makazi na biashara yapo katika uwanda wa chini ambao hukumbwa na mafuriko ya mara kwa mara. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipendekeza kwamba kuwepo na mpango kabambe wa mji wa Babati, utakaochambua na kutenga maeneo hatarishi wakati wa kuandaa maeneo ya makazi na biashara. Wakati wa ufuatiliaji na kutathmini utekelezaji wa pendekezo hili, ilibainika kuwa pendekezo hili halikufanyiwa kazi. Ilibainika pia kuwa Mpango Kabambe na ule wa mpito haujafanyiwa mapitio ili kujumuisha mapendekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Pendekezo *4.1:* Kujumuisha suala la usimamizi wa maafa katika bajeti

Wakati wa ukaguzi huo mnamo mwaka 2007 ilibainika kuwa, Halmashauri za Mji na Wilaya ya Babati hazikutenga bajeti kwa ajili ya usimamizi wa maafa/mafuriko japokuwa Halimashauri hizo zinakumbwa na tatizo kubwa la mafuriko kwa miaka mingi. Kwahiyo, ilipendekezwa kuwa Serikali za Mitaa ziingize masuala ya usimamizi wa maafa na mafuriko katika bajeti zao za mwaka. Hadi sasa Halmashauri hizo hazijatekeleza.

***Pendekezo 8.2:* Uandaliwe mpango mkakati kwa ajili ya kukabiliana na mafuriko**

Ripoti ya ukaguzi ilipendekeza kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa iandae mpango mkakati wa kukabiliana na mafuriko. Katika kutekeleza pendekezo hili Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa ilipanga kuweka miundombinu ya teknolojia kwa ajili ya hali ya hewa, tabia nchi, maji na ufuatiliaji wa miundombinu ya mazingira. Taarifa za hali ya hewa na tabia nchi zimejumuishwa katika mipango ya maendeleo na mifumo ya upashanaji wa taarifa za tahadhari. Wakati wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa pendekezo hili, ofisi ilibaini kuwa pendekezo hili halikufanyiwa kazi, japo kuna mradi wa kuimarisha upashanaji wa habari za hali ya hewa na mifumo ya tahadhari nchini ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa. Jitihada zimefanywa pia ili kutekeleza pendekezo hili ambalo linataka kuwepo kwa mikakati kwa ajili ya kupambana na kuzuia mafuriko .

Uchambuzi zaidi wa mapendekezo kwa kila kundi na tabaka unaonyeshwa katika Jedwali 4.2:

Jedwali 4.2: Idadi ya mapendekezo ya aina mbali mbali ambayo hayajatekelezwa

Mapendekezo	Jumla ya mapendekezo	Idadi ya mapendekezo ambayo hayakutekelezwa
Mipango	7	2
Maamuzi	2	0
Maendeleo	3	0
Bajeti	3	1
Ufuatiliaji na Tathmini	2	0
Uhusishaji jamii	2	0

Uchambuzi katika Jedwali 4.2 unaonyesha kwamba mapendekezo kuhusu bajeti na mipango kwa ajili ya kuzuia na kupambana na athari za mafuriko Babati hayajafanyiwa kazi japo baadhi yalitekelezwa kikamilifu au kwa kiasi fulani.

Hii inaonyesha kuwa bajeti na mipango ya mafuriko bado ni hafifu na jitihada za kuboresha eneo hilo bado zinahitajika.

4.2.3 Mapendekezo ambayo yametekelezwa kwa kiasi

***Pendekezo 2.2**: kupandwa mimea inayohifadhi udongo ili kuzuia mmomonyoko*

Ukaguzi umebaini kuwa mmomonyoko wa udongo uliotokea katika maeneo ya Kigogoni yanasababisha kuongezeka kwa tope katika ziwa Babati. Ripoti ilipendekeza kuwa Halmashauri ya Mji wa Babati itangaze maeneo hayo ya kingo ya Kigongoni na maeneo mengine yenye maporomoko kuwa hayaruhusiwi kwa kilimo, ufugaji, utengenezaji wa matofali na yanahitaji kupandwa idadi kubwa ya miti na mimea mingine ya kuzuia mmomonyoko wa udongo. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa pendekezo hili umebaini kuwa kuna mabango ya matangazo ya zuio yakionyesha kuwa eneo hilo

limezuiliwa kufanya shughuli za kilimo na ufugaji. Lakini, miti kwa ajili ya kuhifadhi udongo bado haijapandwa.

Pendekezo 4.2: **Halmashauri zinatakiwa kuhakikisha kuwa asasi za kiraia na wataalamu walioko wanatekeleza majukumu yao**

Wakati wa ukaguzi, ilidhihirika kuwa asasi za kiraia na wataalamu walioko hawatekelezi majukumu yao katika miradi ya kuzuia mafuriko. Ilipendekezwa kuwa Halmashauri za Mji na Wilaya ya Babati zihakikishe kuwa asasi za kiraia na wataalamu walioko wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa pendekezo hili, umebaini kuwa Halmashauri ya Mji wa Babati imekuwa ikitoa elimu kwa wadau wa mazingira na wakazi wanaozunguka ziwa Babati. Ufugaji, kilimo na utengenezaji wa matofali umezuiliwa ipasavyo. Hata hivyo, hakuna ushahidi wowote unaoonyesha jinsi wataalamu katika ngazi ya wilaya, kata, mtaa na kijiji wanavyotekeleza programu za kuzuia mafuriko.

***Pendekezo 8.1*: Idara ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu iboreshe utaratibu wa ufuatiliaji wa shughuli za Maafa**

Ripoti ya ukaguzi imebaini kuwa baada ya kuwapatia watendaji wa Halmashauri za Wilaya mafunzo, Idara ya Maafa ya Ofisi ya Waziri Mkuu haijafanya tathmini na ufuatiliaji kuangalia uendelezaji wa mipango ya Halmashauri mbali mbali nchini katika kusimamia maafa na tahadhari zingine za mazingira, ambapo washiriki walitakiwa kuandaa na kutekeleza. Ripoti ilipendekeza kuwa, Idara ya Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu ifanye ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini yanaonyesha ufanisi katika kuzuia na kukabiliana naathari za mafuriko. Kutokana na ushahidi uliowasilishwa, mwongozo unaotumika kwa ajili ya mafunzo umeshaandaliwa na unatakiwa kuanza kutumika kwenye mafunzo mbalimbali. Pamoja na ukweli kwamba mafunzo ni suala endelevu, Mamlaka 13 tu kati ya 168 nchini ndizo zimeweza kuandaa mipango ya dharura kama sehemu ya mafanikio yatokanayo na mafunzo yaliyotolewa na Idara ya Maafa. Kwa ujumla Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa hazijapata mafunzo na hazijaandaa mipango ya dharura ya kukabiliana na maafa.

***Pendekezo 8.3*: Kuanzishwa kwa mpango wa kuzuia mafuriko na kuratibu juhudi za pamoja**

Ukaguzi ulipendekeza Idara ya Maafa iliyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuratibu utafiti dhidi ya mafuriko, kuanzisha mpango wa kuzuia mafuriko, kufanya mapitio na kuratibu jitihada za kuzuia mafuriko yanayotokea mara kwa mara.

Idara ya Maafa na wadau mbali mbali wa masuala ya maafa wanapaswa kuelewa kuwa jamii ipo kwenye hali hatarishi ya maafa na inahitaji kuweka mifumo imara na endelevu kuweza kujiandaa kukabiliana na maafa . Utafiti wa awali unalenga kuangalia namna tarifa zinavyopelekwa kwa jamii kuhusu kuchukua tahadhari kabla na baada ya dharura/maafa kutokea.

Aidha, baadhi ya njia zilizotajwa za kujikinga na kuzuia maafa kama vile: mipango ya uokoaji kwa wahanga wa Mabwepande – Dar es Salaam; Magole Kilosa; na Dakawa Mvomero ilikuwa ni njia za kujikinga baada ya maafa kuwa yametokea na hazikuwa za kujikinga kabla maafa hayajatokea kama ilivyopendekezwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Pendekezo 8.4*: *Kuanzisha mfumo wa uandikishaji kwa ajili ya uchambuzi na hatua za kujikinga

Ukaguzi ulibaini kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Idara ya Maafa haina njia madhubuti za kuweka kumbukumbu na kufanya uchambuzi wa kujikinga na athari za mafuriko katika maeneo yote yaliyo hatarishi ya kukumbwa na mafuriko nchini. Ili kukabiliana na upungufu huu ilipendekezwa kuwa Idara ya Maafa iandae mfumo madhubuti wa utunzaji wa kumbukumbu kwa nchi nzima, ambamo matukio yote ya mafuriko yatakuwa yanaorodheshwa na kufanyiwa uchambuzi wa njia za kujikinga na athari za mafuriko. Mfumo huo wa uandikishaji na utunzaji wa kumbukumbu utakuwa ni muongozo wa kuandaa mkakati wa kujikinga na mafuriko. Ufuatiliaji uliofanywa kuhusiana na utekelezaji wa pendekezo hili umebaini kuwa japokuwa kuna miongozo na sheria zilizoanzishwa, hakuna rejista iliyoandaliwa ili kutunza kumbu kumbu za mafuriko yaliyotokea na kufanyiwa uchambuzi wa kina ambao ungeiwezesha Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa kuweza kutambua kama mafuriko katika maeneo husika mara moja au unajirudia. Kutokana na kukosekana kwa taarifa hizo inakuwa vigumu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa kuchukua hatua madhubuti za kujikinga na maafa nchini.

4.2.1 Mapendekezo Yaliyotekelezwa kikamilifu

Uchambuzi uliofanywa wakati wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa, ilibainika kuwa mapendekezo 12 yaliyoonyeshwa hapa chini yalitekelezwa kikamilifu:

Pendekezo 1: Vikinga Majani

Ili kuweza kudhibiti vizuizi vya uotaji wa majani, kufanya shughuli za kilimo na ufugaji pembezoni mwa Ziwa Babati, ilipendekezwa kuwa Halmashauri ya Mji na Wilaya ya Babati ifanye maboresho katika maeneo haya yote mawili. Ufuatiliaji uliofanyika ili kuona utekelezaji wa pendekezo hili umebaini kuwa majani ambayo yangeweza kuzuia utiririshaji wa maji kuelekea mto Kigongo yamefyekwa vizuri. Hii ina maanisha kuwa pendekezo hili limetekelezwa kikamilifu.

Pendekezo 2: Kingo za Mto na Maporomoko ya Kutengenezwa

Pendekezo 2.1: Ilipendekezwa kuwa, kwa kuzingatia uwekezaji uliofanywa hapo awali kwenye kingo za mto, na uhitaji wa kuzuia uharibifu zaidi unaotokana na mmomonyoko wa udongo, Mkoa wa Manyara na Halmashauri ya Wilaya ya Babati ilipaswa kutafuta ushauri kwa wataalam wa kuzuia mmomonyoko wa udongo kama njia ya tahadhari. Pendekezo hili limetekelezwa kikamilifu kwa kuwa, mifereji iliyotengenezwa yenye kingo imara ni ya kudumu na inazuia ongezeko la kina. Pia agizo la kuzuia shughuli za kilimo na ufugaji katika eneo hilo limetolewa na miti imepandwa.

Pendekezo 3.1: Upangaji wa Makazi na Sehemu za Biashara kwa mji wa Babati

Ukaguzi ulipendekeza kuwa maafisa wa mipango miji katika Halmashauri ya Mji wa Babati wanapaswa kuzingatia suala la athari zitokanazo na mafuriko wanapogawa viwanja vya makazi biashara na matumizi mengine. Jitihada zinapaswa zifanyike kuhakikisha kuwa njia za kujikinga zinatekelezwa katika maeneo ambayo yapo hatarini kukumbwa na mafuriko. Pendekezo hili limetekelezwa kikamilifu kwa kuwa kwenye michoro ya maafisa mipango miji inazingatia maeneo ambayo ni hatarishi kwa mafuriko. Hata hivyo mipango ya muda mfupi ya matumizi ya ardhi haijafanyiwa maboresho ili kuweza kujumuisha namna ya kukabiliana na mafuriko.

Pendekezo 4: Mipango ya awali ya maafa na fedha kwa ajili ya usimamizi wa mafuriko

Ilipendekezwa kuwa Mamlaka ya Mkoa na Wilaya zijumuishwe suala la usimamizi wa mafuriko/majanga katika bajeti zao za mwaka; na kuhakikisha kuwa asasi za kijamii na maafisa wa Serikali katika ngazi mbalimbali wanatimiza wajibu wao kwenye programu za kuzuia mafuriko.

Wakati wa ufuatiliaji wa pendekezo hili ilibainika kuwa shughuli zinazohusiana na usimamizi wa maafa zimejumuishwa kwenye mpango wa muda mfupi wa matumizi ya Halmashauri ya Wilaya ya Babati. Pia ilionekana kuwa Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara ilipokea fedha kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa maafa.

Pendekezo 5: Kingo ya Kigongoni

Pendekezo 5.1: Pendekezo hili liliitaka Halmashauri ya Mji wa Babati na Wakala wa Barabara Mkoa wa Manyara kupunguza athari za mafuriko kwa kubadilisha makaravati madogo na kuweka makubwa zaidi na pia kuimarisha kingo zake katika eneo la Kigongoni. Pendekezo hili limetekelezwa kikamilifu.

Pendekezo 5.2: Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa makaravati katika kingo za Kigongoni hayakuwa mazuri kiasi cha kuruhusu maji ya kutosha kutiririka ili kuzuia mafuriko katika ziwa Babati lililopo katika Halmashauri ya Mji wa Babati. Ripoti ya ukaguzi ilipendekeza kuwa Wakala wa Bara bara nchini itengeneze makaravati katika kingo za Kigongoni ambayo yataboresha mtiririko wa maji ili kuzuia mafuriko kupitia Ziwa Babati. Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa pendekezo hili ilibainika kuwa, makaravati mapya yenye umbo la boxi yametengenezwa katika eneo la Kigongoni (**Picha 4.1**)

Picha 4.1: Makaravati yaliyoboreshwa katika Eneo la Kigongoni

Chanzo: *Wakala wa Bara bara nchini, 2014*

Pendekezo 6.1: Daraja la Kiongozi:

Pendekezo liliitaka Wakala wa Barabara kuhakikisha kuwa kazi za matengezo zinafanyika mapema ili kuepuka kufungwa kwa barabara kunakotokana na uharibifu mkubwa unaosababishwa na mafuriko; na kushauriana na wakandarasi wa madaraja wenye uzoefu wakati wanapofanyia ukarabati wa madaraja ili kuhakikisha kuwa kingo za madaraja hayo zinajengwa kwa ubora wa hali ya juu na yenye ukubwa wa kuweza kupitisha maji ya kutosha.

Ufuatiliaji uliofanywa kuhusiana na utekelezaji wa pendekezo hili unaonyesha kuwa, pendekezo hili limetekelezwa.

Picha 4.2: Daraja la Kiongozi

Chanzo: *Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, 2014*

Pendekezo 7: Usanifu wa matengenezo wa barabara ya Arusha – Dodoma

Ilipendekezwa kuwa Wakala wa Barabara itumie uzoefu uliopata kutoka kwenye mafuriko ya awali ili waweze kuitaarifu kikamilifu Kampuni ya Washauri elekezi ambao wanafanya usanifu wa matengenezo ya barabara ya Singida Babati - Minjingu.

Wakati wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa pendekezo hili, ilibainika kuwa waliweza kumfahamisha Mshauri elekezi aliefanya maboresho ya usanifu wa mradi wa barabara ya Singida – Babati – Minjingu ambae ni M/s Carl Bro wa Denmark ili kuweza kuchukua tahadhari ya tatizo la mafuriko katika Mji wa Babati ambalo limekuwa likisababishwa na kujaa kwa Ziwa Babati. Uboreshaji huo ulijumuisha Ujenzi wa makaravati makubwa ya kupitisha maji kwa wingi zaidi pindi Ziwa Babati linapofurika. Ujenzi huu ulifanyika katika eneo la Kigongoni. Vile vile ulijumuisha upandishaji wa tuta la barabara zilizojengwa katika Mji wa Babati na pia mfumo mzuri wa mifereji ya kutiririsha maji kipindi chote cha mvua.

4.3 Hitimisho na Matarajio

Ofisi ya Ukaguzi itaendelea kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ambayo hayakutekelezwa na yale yaliyotekelezwa kwa kiasi ili kuhakikisha kuwa yametekelezwa kikamilifu.

4.3.1 Mapendekezo Kwa Halmashauri ya Mji wa Babati

1. **Kutangaza kuwa eneo kutoka kingo za Kigongoni mpaka mwisho wa korongo la maporomoko ya maji limezuiwa kwa shughuli za kilimo, ufugaji, utengenezaji wa matofali nk, na**

pia kupanda idadi kubwa ya miti na aina nyingine ya uoto unaozuia mmomonyoko wa udongo (Pendekezo 3.2 kwenye ripoti husika, Uk 51);

2. Kuweka mpango kabambe wa Halmashauri ya Mji wa Babati ili kukabiliana na viashiria vyote hatarishi wakati wa kupanga maeneo ya makazi na biashara (Pendekezo 6.2 la kwenye ripoti husika ukurasa 52);
3. Kujumuisha shughuli za kukabiliana na mafuriko katika bajeti zao za mwaka (Pendekezo 4.2 la kwenye ripoti husika , Ukurasa 53); na
4. Mamlaka za Mkoa wa Manyara na Halmashauri ya Mji wa Babati kuhakikisha kuwa asasi za kiraia na maafisa husika wa mambo ya maafa katika ngazi zote wanatimiza majukumu yao katika utekelezaji wa programu za kukabiliana na mafuriko (Pendekezo 4.2 ya ripoti husika, ukurasa 53).

4.3.2 Pendekezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara

Katibu Tawala wa Mkoa ahakikishe kuwa asasi za kijamii na maofisa husika katika ngazi mbalimbali wanatimiza majuku yao katika utekelezaji wa programu za kukabiliana na mafuriko.

Mapendekezo kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa

Ofisi ya Waziri Mkuu Idara ya Maafa inapaswa:

1. Kuandaa mpango kazi kuhusiana na mafuriko (Pendekezo 8.2 kwenye ripoti husika , ukurasa 53);
2. Kufuatilia ili kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa kwenye Halmashauri za Wilaya yanakuwa na manufaa na ujuzi uliopatikana unatumika kwenye shughuli za kukabiliana na kujikinga na mafuriko (Pendekezo 8.1 ya ripoti husika , ukurasa 53);
3. Kufanya jitihada na kuratibu tafiti zinazohusiana na mafuriko, kuandaa mipango ya kujikinga na mafuriko, na kufanya maboresho ya mara kwa mara na kuratibu njia za kukabiliana na mafuriko (pendekezo 8.3 la kwenye ripoti husika , ukurasa 53); na
4. Kuhakikisha kuwa kwa haraka iwezekanavyo mfumo wa uandikishaji na utunzaji wa kumbukumbu za mafuriko nchini, ambapo matukio ya mafuriko yatakuwa yanaorodheshwa na kufanyiwa uchambuzi wa kina kama vile athari za mafuriko katika maeneo yaliyo hatarishi na ambayo ni muhimu

kiuchumi. Mfumo huo wa kumbukumbu utakuwa ni msingi wa kuandaa mkakati wa kujikinga na kukabiliana na mafuriko nchini (Pendekezo 8.4 la kwenye ripoti husika, ukurasa 53).

SURA YA TANO

KUFUALIA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU UTOAJI WA HUDUMA YA AFYA YA MSINGI

5.1 Usuli wa Ukaguzi

Taarifa ya Ukaguzi wa ufanisi kuhusiana na Usimamizi wa Huduma za Afya ya Msingi katika vituo vya afya iliwasilishwa Bungeni mwezi April 2009. Wakaguliwa wakuu walikuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

Kusudi la ukaguzi ni kuchunguza kama vituo vya afya vinasimamiwa kwa ufanisi na kama utendaji wake unapimwa na kuzingatiwa kwenye utengaji wa rasilimali zilizopo. Lengo lilikuwa ni kupata nafasi ya kuboresha usimamizi na ufanisi wa huduma katika vituo vya afya kwa jamii.

Ilibainika kuwa TAMISEMI ni mmiliki wa vituo vya huduma ya afya ya msingi na Wizara ya Afya kama Wizara mama ndiyo kwa kiasi kikubwa inatimiza majukumu ya kusambaza rasilimali kwa vituo vya afya.

Ukaguzi umebaini matatizo kadhaa yanayohusiana na utendaji wa vituo vya afya. Mapungufu hayo yanahusisha: Ukosekanaji wa maarifa katika ngazi ya kitaifa kuhusu namna gani vituo vya afya vinafanya kazi vizuri, na pia rasilimali zilizopo hazikuwa zinasambazwa na kutumika vizuri. Kadhalika kulikuwa na dalili za mapungufu kwenye usimamizi na ufuatiliaji katika ngazi mbalimbali za kiutawala.

5.2 Hali ya Ujumla ya Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa

Kwa ujumla utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa unaonyesha kuwa pendekezo moja (1) kati ya 20 halikutekelezwa kabisa, mapendekezo 10 yalitekelezwa kwa kiasi tu na mapendekezo 9 yalitekelezwa kikamilifu. Kielelezo 5.1 kinaonesha hali ya utekelezwaji wa mapendekezo yaliyotolewa.



Kielelezo 5.1: Asilimia ya Utekelezwaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa kwa TAMISEMI na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

Tathmini ilifanyika ili kuweza kuhakiki kiwango cha utekelezaji wa jumla wa mapendekezo yaliyotolewa kwa Wizara husika, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Kielelezo 5.2 kinaonyesha hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa Wizara husika, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.



Kilelezo 5.2: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo katika Ngazi ya Wizara, Tawala za Mikoa na Halmashauri

5.3 Utekelezaji wa Pendekezo Moja moja

5.3.1 Mapendekezo ambayo Hayakutekelezwa

Pendekezo 1: Bohari kuu ya Madawa kuandaa na kutoa taarifa za uwajibikaji kwa kila robo ya mwaka

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii haijatekeleza jukumu lake la kuhakikisha kuwa Bohari Kuu ya Madawa inaandaa na kutoa taarifa za Uwajibikaji kwa kila robo mwaka kwa Halmashauri zote. Wizara hiyo pia haijasisitiza umuhimu wa kuboresha suala la uwajibikaji kwa Bohari kuu ya Madawa zinapotoa huduma kwa Halmashauri.

Tathmini zaidi ya mapendekezo yaliyotolewa kwa mgawanyo wa makundi mbalimbali ilifanyiaka kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali 5.1:

Jedwali 5.1: Idadi ya mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kwa kila kundi

Makundi ya Mapendekezo	Jumla ya Mapendekezo yaliyotolewa kwa Makundi	Idadi ya Mapendekezo yasiyotekelezwa
Uandaaji wa mipango	3	-
Bujeti	3	-
Kujenga uwezo	2	-
Ufuatiliaji na tathmini	1	-
Usimamizi wa utendaji	2	-
Utoaji wa huduma	1	-
Utoaji taarifa	6	1
Ugatuaji	2	-

Jedwali 5.1 linaonyesha kuwa pendekezo moja linalohusiana na utoaji wa taarifa halikutekelezwa. Mapendekezo mengine yalikuwa yametekelezwa kwa kiasi au kwa ukamilifu.Hii inaonyesha kuwa maboresho yanahitajika katika eneo la utoaji wa taarifa za utendaji kwa vituo vya afya kuhusiana na utoaji wa huduma za afya ya msingi nchini.

5.3.2 Mapendekezo ambayo yametekelezwa kwa Kiasi

Kati ya mapendekezo yote yaliyotolewa, mapendekezo saba (7) yalitekelezwa kwa kiasi tu, hii inamaanisha kuwa bado mambo mengine kuhusiana na pendekezo hili hayajakamilika. Ifuatayo ni tathmini ya hali ya utekelezaji wa kila pendekezo kati ya mapendekezo 7 yaliyotekelezwa kiasi:

Pendekezo 2: Utengaji wa madawa muhimu, vifaa , vifaa tiba na fedha

Wiara ya Afya Na Ustawi WA Jamii inapaswa kutenga madawa muhimu, vifaa, vifaa tiba na fedha

Wakati wa ufuatiliaji ili kutathmini kiwango cha utekelezaji wa pendekezo hili, ilibainika kuwa , hali ya sasa kwa vituo vya afya hairidhishi. Hii ni kwa sababu viashiria 3 vilivyowekwa ambavyo ni idadi ya wanaohudhuria vituo vya afya,Idadi ya wahudumu waliopo na muda wa kusubiria huduma hutumika kwa nadra.Ni mara chache idadi ya watu wanaohudhuria vituo vya afya inalinganishwa na rasilimali zilizopo kama vile wahudumu wa afya na muda wa kusubiria kupatiwa huduma. Hali halisi ya mgawanyo wa rasilimali kwa sasa ni kama ifuatavyo:

- hospitali za rufaa za mikoa zinapata madawa muhimu, vifaa , vifaa tiba na fedha kulingana na idadi ya vitanda vilivyopo;
- hospitali za wilaya zinapatiwa fedha na rasilimali zingine kulingana na idadi ya wakazi katika wilaya; na
- hospitali maalumu za kitaifa zinapatiwa fedha na rasilimali zingine kulingana na idadi ya huduma zinazotolewa.

Kwa mantiki hii, suala la wingi wa kazi limeshughulikiwa isipokuwa suala la muda wa kusubiria na mlolongo wa kushughulikia wagonjwa halijafanyiwa kazi na Wizara ya Afya haijaonyesha ni kwa namna gani watashughulikia suala hili.

Ilibainika kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ipo katika mchakato wa kurekebisha hali iliyopo ya sasa, kwa sasa inakusanya takwimu toka vituo vya afya ili kupata njia ya kuboresha hali hii.

Pendekezo 3: Utoaji wa madawa muhimu kwa kiasi cha kutosha
Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ihakikishe vituo vya afya vinapatiwa na kusambaziwa madawa ya kutosha na Bohari kuu ya Madawa kulingana na uhitaji wao.

Licha ya kupokea miongozo, na uboreshwaji wa utengaji wa bajeti, vituo vya afya vinakabiliwa na upungufu wa madawa na vifaa tiba. Taarifa toka vituo vya afya zinaonyesha kuwa hili tatizo bado lipo. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inapaswa kutafuta namna ya kuboresha huduma kwenye vituo vya afya nchini.

Pendekezo 4: Tathmini ya taarifa zinazoandaliwa ilenge masuala ya kiutendaji

TAMISEMI ihakikishe kuwa tathmini ya taarifa za fedha na zile za masuala husika ya huduma ya afya ya msingi yanalipa umuhimu suala la ufanisi wa kiutendaji ili kuleta mabadiliko chanya kwa kuwezesha vituo vya afya kutumia ipasavyo misaada yote ya kifedha na ya kitaalamu.

Mpaka sasa ilibainika kuwa TAMISEMI imeanzisha mfumo wa upangaji kwa ujumla (Plan Rep) wa kutathmini utendaji, ambao umeleta maboresho kwa ngazi zote kutoka mkoa hadi Wizara. Ingawa mfumo huu wa upangaji (Plan Rep) umeanza kutumika lakini TAMISEMI na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zimeshindwa kuunganisha mfumo wa EPICOR na Plan Rep na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo yake.

Pendekezo 5: Utengaji wa rasilimali kwa vituo vya afya ulingane na utendaji kazi

Wakurugenzi wa halmashauri walitakiwa kuhakikisha kuwa utengaji wa rasilimali katika vituo vya afya unalinganishwa na utendaji. Kutekeleza hili, halmashauri kwa kushirikiana na timu za usimamizi wa masuala ya afya walitakiwa kuanzisha vigezo vya kiufanisi vinavyolingana na utendaji wa kituo husika cha afya.

Ilibainika kuwa TAMISEMI imeanzisha mradi wa majaribio uitwao malipo kulingana na utendaji kuanzia mwaka wa fedha 2012/13 kwa mkoa wa Pwani.Mradi huu ulilenga kuongeza uwajibikaji miongoni mwa wafanyakazi na utengaji mzuri wa rasilimali kulingana na uhitaji.

Licha ya kuanzishwa kwa mradi huu wa majaribio, bado kuna changamoto kuhusu na usambazaji wa rasilimali na uwajibikaji katika kazi zilizotekelezwa. Kushughulikia suala hili Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilianzisha mfumo wa uwezeshwaji kifedha kulingana na matokeo ya kiutendaji ambao utatekelezwa pamoja na mradi wa malipo kulingana na utendaji (P4P) ili kuhakikisha

kunakuwa na ufanisi zaidi katika usambazaji wa rasilimali na uwajibikaji wa shughuli kwa mwaka wa fedha ujao 2015/16.

Pendekezo 6: Kuchangia uboreshaji wa huduma katika vituo vya afya – usambazaji mzuri wa vifaa tiba

Ilipendekezwa kuwa , afisa tabibu wa wilaya na timu yake pamoja na timu ya usimamizi wa afya ya Halmashauri kuchangia uboreshaji wa shughuli katika vituo vya afya kwa kuimarisha na kuhakikisha kuwa kuna usambazaji mzuri wa madawa na vifaa tiba muhimu kwa vituo vya afya.

TAMISEMI imeanzisha mfumo wa utoaji wa taarifa wa usimamizi wa vifaa (ILS) ili kuhakikisha kuwa maombi yanayotoka kwenye vituo vya afya yanapata kibali toka kwenye ngazi ya halmashauri na vifaa kusambazwa moja kwa moja kwenye vituo vya afya. Licha ya kuanzishwa kwa ILS, bado vituo vya afya havipokei madawa na vifaa tiba muhimu kwa wakati na kwa kiwango kinachohitajika.

Pendekezo 7: Kuchangia uboreshaji wa shughuli katika vituo vya afya – ugawaji mzuri wa vifaa tiba

Ilipendekezwa kuwa, afisa tabibu wa wilaya na timu yake pamoja na timu ya usimamizi wa afya ya Halmashauri kuchangia uboreshaji wa huduma katika vituo vya afya kwa kuimarisha na kuhakikisha kuwa mgawanyo wa wafanyakazi, madawa, fedha na rasilimali nyingine katika vituo mbali mbali vya afya unafanyika kwa kuzingatia viashiria vya ufanisi kama nguvu kazi na muda wa kusubiria huduma.

Majaribio ya mradi wa P4P umeweza kuhamasisha ubadilishanaji wa wafanyakazi na mgawanyo wa rasilimali nyingine.Hata hivyo, pamoja na jitihada za kuanzisha mradi wa P4P bado kuna changamoto za ugawaji wa rasilimali katika vituo vya afya mbalimbali kulingana na viashiria vya ufanisi.

Pendekezo 8: Ugatuaji wa fedha za vituo vya afya

Ilipendekezwa kuwa, afisa tabibu wa wilaya pamoja na timu yake (CHMT) wawe wanachangia katika uboreshaji wa shughuli kwenye vituo vya afya kwa kuimarisha na kuhakikisha kuwa vituo vya afya vinamiliki na kufanya maamuzi ya fedha wenyewe. Hii ni pamoja na

kuhakikisha kwamba kila kituo cha afya kinakuwa na akaunti yake na fedha za dharura.

TAMISEMI imetoa maelekezo mwaka 2011 kwa halmashauri zote kufunga akaunti ndogo ndogo na kufungua akaunti sita tu. Agizo hili halikufanyika na ndipo mwaka 2013 halmashauri zilielekezwa tena kufungua hizi akaunti.Kwa sasa ni Halmashauri chache tu ndizo zimefungua akaunti hizi.

Pendekezo 9: Kuimarisha na Kuwezesha Usimamizi wa Kifedha

Ilipendekezwa kuwa , afisa tabibu wa Wilaya pamoja na timu yake ya usimamizi wa afya ya Wilaya wana wajibu wa kuchangia uboreshaji wa shughuli za afya katika vituo vya afya kwa kuimarisha na kuwezesha uwepo wa vitendea kazi na kuweka kumbukumbu na usimamizi wa rasilimali za afya.

Hivi karibuni kamati za afya zimeanza kuwezeshwa kupitia mafunzo yatolewayo na mradi wa kujenga uwezo kwenye shughuli za afya (BHSP) katika eneo la usimamizi wa fedha.

Pendekezo10: Kuhuisha mfumo wa taarifa wa usimamizi wa afya

Wizara ya afya ilitakiwa kuhakikisha kuwa mfumo wa taarifa wa usimamizi wa shughuli za afya unahuishwa ili kuboresha uwajibikaji

Wizara kwa sasa imeanzisha mfumo mpya wa kukusanya na kuweka taarifa. Kiwango cha utoaji wa taarifa kwa sasa kimeboreshwa kufikia 84%. Wizara inapaswa kuendelea kuhuisha mfumo huu kwa kuhakikisha kuwa kiwango cha utoaji wa taarifa kwa mwezi kinafikia asilimia 100.

Pendekezo 11: Kuimarisha timu za usimamizi za mkoa

Ilipendekezwa kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuimarisha timu za Mikoa za usimamizi wa masuala ya afya ili ziweze kutimiza majukumu yao ya kusimamia timu za Wilaya na kutathmini taarifa zao za maendeleo kabla ya kuzipeleka TAMISEMI na Wizara ya Afya na Usatwi wa Jamii.

Shughuli za kujenga uwezo zinaendelea kwenye halmashauri na ngazi mbalimbali. Awamu ya kwanza na ya pili ya kujenga uwezo kwa timu za mikoa za usimamizi wa afya zilizofanyika mwaka (2008 –

2011) na (2011 – 2014) zikijumuisha maeneo ya usimamizi na ufuatiliaji .

Pendekezo 12: Kuimarisha mifumo ya udhibiti – usambazaji sahihi

Mifumo ya udhibiti wa bajeti ya vituo vya afya inahitaji kuboreshwa kwa kuhakikisha usambazwaji wa madawa na vifaa tiba kwenye vituo vya afya, kuhakikisha vituo vya afya vinakuwa na fedha za dharura, na kufungua akaunti zao.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeanzisha mfumo wa taarifa wa usimamizi wa vifaa vya afya (ILS) ili kuhakikisha kuwa maombi yanayotoka kwenye vituo vya afya, yanapata kibali toka ngazi za wilaya na vifaa vinapelekwa moja kwa moja vituoni. Pia baadhi ya halmashauri zimefungua akaunti kwa vituo vya afya na zimekuwa zikishirikisha ukomo wa bajeti zao.

Pendekezo 13: Kuimarisha mfumo wa udhibiti – utengaji wa rasilimali

Mfumo wa kudhibiti bajeti kwa vituo vya afya unahitaji kuimarishwa kwa kubadilisha wafanyakazi vituo vyao vya kazi, madawa, fedha na rasilimali nyingine kwa vituo vya afya mbalimbali kulingana na viashiria vya utendaji kama nguvu kazi na muda wa kusubiria kupata huduma.

Ilibainika kuwa, TAMISEMI ipo kwenye majaribio ya mradi wa malipo kulingana na utendaji ambao umeweza kuhamasisha kubadilishana kwa wafanyakazi na mgawanyo wa rasilimali nyingine. Kadhalika, mfumo wa afya muhimu wa kitaifa unaingizwa kwenye muongozo wa nne wa mpango wa kina wa afya wa wilaya. Kwa sasamradi huo upo kwenye hatua ya utekelezaji kama inavyooneshwa kwenye mipango ya muda mfupi ya matumizi kwa Halmashauri zilizofuatiliwa wakati wa ufuatiliaji uliofanywa kwa kila robo mwaka.

5.3.3 Mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu

Uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ambayo yalitekelezwa kwa ukamilifu na Wizara ya Afya na ustawi wa Jamii na TAMISEMI yamefafanuliwa hapa chini:

Pendekezo 14: Taratibu za utoaji wa pesa

TAMISEMI imehakikisha kuwa utaratibu wa kutoa fedha kwa kuzingatia muda unafuatwa. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pia

imeandaa mfumo wa wazi unaowezesha kubaini pesa zilizotengwa kwenye Vituo vya Afya, shughuli zinazotegemewa kufanywa, kiwango cha huduma na malengo. Miongozo imetolewa kwa timu za usimamizi wa afya kwa ngazi ya mkoa, halmashauri na vituo vya afya ili kuhakikisha kuwa ukaguzi wa usimamizi unafanywa kwa wakati na kwa ufanisi.

Pendekezo 15: Uandaaji wa taarifa za kina kwa kila robo mwaka

Ilibainika kuwa timu za usimamizi wa afya za mkoa zinaandaa mipango ya afya na kujumuisha Halmashauri zote kila baada ya siku 30 baada ya robo mwaka. Nakala zinatumwa TAMISEMI na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Wizara ya Afya na TAMISEMI kila robo mwaka zinazipitia taarifa hizo na kutengeneza Mpango wa Kina wa Afya wa Wilaya unaohusisha masuala ya fedha na utaalamu kwa lengo la kufanya maamuzi.

Pendekezo 16: Kuimarisha mfumo wa udhibiti wa bajeti

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeimarisha mfumo wa udhibiti wa bajeti ya vituo vya afya kwa kuvipatia makadirio ya ukomo wa bajeti ya mwaka. Pia wameboresha mfuko wa maendeleo wa halmashauri za mitaa (LGDG) kwa kuweka kigezo cha uwazi na ushirikishanaji wa taarifa ili halmashauri ziweze kupata pesa za maendeleo.

Pendekezo 17: Kuimarisha ukusanyaji wa taarifa, uchambuzi na mfumo wa utoaji wa taarifa

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na TAMISEMI zimeweza kusimamia na Kuimarishaji ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za vituo vya afya na mfumo wa utoaji wa taarifa. Hii ni kulingana na mfumo wa usimamizi wa taarifa za afya ulioanzishwa ambao kwa sasa unafanya kazi kwenye Halmashauri zote. Pia mfumo huu umeunganishwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Uchambuzi wa utekelezaji wa mapendekezo kwa kila Wizara husika umeonyeshwa kwenye Kielelezo 5.2

5.4 Hitimisho na Matarajio

Kulingana na hali halisi ya utekelezaji, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali imeamua kuendelea kufanya ufuatiliaji na kutoa taarifa kwa bunge tena mwaka ujao. Hii ni kwa kuwa asilimia 50 ya mapendekezo yaliyotolewa yametekelezwa kwa kiasi tu lakini inaonekana wahusika wanaendelea kufanyia maboresho.

Mwaka ujao ufuatiliaji utazingatia hasa mapendekezo yafuatayo:

5.4.1 Mapendekezo yaliyotolewa kwa wizara ya afya na ustawi wa jamii

1. ***Ugawaji wa vifaa tiba muhimu***

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inapaswa kutenga dawa, vifaa tiba muhimu, vitendea kazi na fedha kwa kuzingatia viashiria vya ufanisi kama vile nguvu kazi katika vituo vya afya na muda wa kusubiria wa wagonjwa na ule wa kupatiwa huduma.

2. ***Kuhakikisha inatoa dawa na vifaa tiba za kutosha***

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inapaswa kuhakikisha kuwa vituo vya afya vinapatiwa dawa na vifaa tiba vya kutosha toka bohari kuu kulingana na maombi yao.

3. ***Kuhuisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Shughuli za Afya***

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inapaswa kuhakikisha kuwa mfumo wa usimamizi wa taarifa za afya unahuishwa ili kuondoa mapengo kulingana na utendaji.

4. ***Taarifa za Uwajibikaji zinaandaliwa na kutolewa***

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inapaswa kuhakikisha kwamba Bohari Kuu ya Madawa inaandaa na kutoa taarifa za uwajibikaji za robo mwaka kwa kila Halmashauri. Taarifa hiyo pia inapaswa kujumuishwa kwenye taarifa za robo mwaka za utekelezaji za Halmashauri.

5.4.2 Mapendekezo yaliyotolewa kwa TAMISEMI

1. ***Kuingiza masuala ya ufanisi kwenye taarifa***

TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kuwa thathmini ya taarifa za kifedha na za kitaalamu zinasisitiza masuala ya utendaji ili kuhamasisha mabadiliko chanya kwa kuwezesha vituo vya afya msaada wa kitaalamu na kifedha.

5.4.3 Mapendekezo kwa Serikali za Mitaa / Halmashauri

1. ***Mgawanyo wa rasilimali kulingana na ufanisi***

Wakurugenzi wa Halmashauri wanapaswa kuhakikisha kuwa mgawanyo wa rasilimali katika vituo vya afya unazingatia ufanisi. Kutekeleza hili Halmashauri kwa kupitia timu yake ya usimamizi inapaswa kuandaa vigezo vinavyohusiana na ufanisi kwa vituo husika

2. ***Kuchangia uboreshwaji wa shughuli***

Afisa Tabibu wa Wilaya na timu ya wilaya ya usimamizi wa masuala ya afya zinahitaji kuchangia uboreshaji wa kazi mbalimbali zinazofanyika katika vituo vya afya. Ili kufanikisha hili, timu zinapaswa kuimarisha na kuhakikisha mambo yafuatayo:

- **usambazaji sahihi wa vifaa tiba na dawa muhimu kwa vituo vya afya;**
- **mgawanyo wa wafanyakazi, dawa, fedha na rasilimali nyingine kwa vituo mbalimbali vya afya mbalimbali kulingana na viashiria vya ufanisi kama nguvu kazi na muda wa kusubiria huduma;**
- **kuhakikisha kuwa kila kituo kinakuwa na akaunti yake na fedha za matumizi madogo madogo kwa kiwango maalum;**
- **kujenga uwezo kwa wasimamizi wa vituo vya afya ili waweze kuweka vizuri kumbukumbu na udhibiti wa fedha na rasilimali nyingine katika vituo vyao vya afya; na**
- **kuwezesha vituo vya afya kuweka kumbukumbu na kusimamia wa rasilimali za afya.**

SURA YA SITA

KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU PROGRAMU YA UKAGUZI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TANZANIA

6.1 Usuli wa Ukaguzi

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Programu ya Ukaguzi kwa Shule za Sekondari nchini iliwasilishwa Bungeni mwezi Agosti mwaka 2009. Mkaguliwa alikuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kupitia idara ya ukaguzi mashuleni.

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini kama idara ya ukaguzi mashuleni inatekeleza kikamilifu nia yake ya kuimarisha ubora wa mafunzo kwenye shule za sekondari.

Ukaguzi ulilenga masomo ya sayansi na hisabati na kuangalia kama ukaguzi katika shule za sekondari unasaidia kutatua tatizo la ufaulu duni wa wanafunzi kwenye masomo ya sayansi na hisabati kwa shule za sekondari.

Ilibainika kuwa hakuna vipaumbele yakinifu kuhusu ufaulu duni wa wanafunzi kwenye masomo ya sayansi na hisabati kwenye mpango wa utekelezaji wa mwaka, mpango wa ukaguzi mashuleni na pia kwenye miongozo iliyotolewa kwa wakaguzi wa shule. Kati ya vipengele 148 vya ukaguzi, ni vipengele 16 tu ndivyo vinavyohusiana na masuala ya ufaulu duni wa wanafunzi. Ukaguzi wetu ulibaini kuwa mamlaka yaliyopo ya kuwasiliana kuhusiana na matokeo ya ukaguzi hayatumiwi ipasavyo ili kuweza kukabiliana na tatizo la ufaulu mdogo wa wanafunzi.

Licha ya kuwa sheria ya elimu[7] imeagiza taarifa za ukaguzi mashuleni kutumwa kwa Afisa elimu mkuu wa Wizara ya Elimu, usambazaji wa taarifa hizo ungeweza kupanuka ili kuwafikia wadau wengine kama vile wakuu wa shule na wakuu wa halmashauri.

Kadhalika, ukaguzi ulibaini kuwa hakuna mzunguko wa kufuatilia tathmini kwa kaguzi zinazofanyika. Ufuatiliaji huu ni muhimu kwenye

[7] Sheria ya Elimu No 25 ya Mwaka 1978

mfumo wa mafunzo hasa wakati wa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa kuhusu ufanisi wa shule.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ilibaini kuwa, suala la ufaulu duni kwenye masomo ya sayansi na hisabati kwa wanafunzi wa shule za sekondari halijumuishwi na kupewa kipaumbele kwenye miongozo na mipango ya utekelezaji ya ukaguzi wa shule. Pia matokeo ya ukaguzi katika shule hayawasilishwi ipasavyo kwa wadau.Aidha ufuatiliaji na tathmini havifanyiki mara kwa mara kuona utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na wakaguzi wa shule.

6.2 Utekelezaji wa Mapendekezo

Kwa ujumla, mapendekezo 12 yalitolewa na ofisi ya Taifa ya ukaguzi.Katika mapendekezo hayo, idara ya ukaguzi mashuleni imeweza kutekeleza mapendekezo 6 kikamilifu, 5 kwa kiasi na moja halikutekelezwa kabisa.

Kielelezo 6.1 kinaonyesha hali ya ujumla ya utekelezaji wa mapendekezo yote 12.



Kielelezo 6.1: Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Ukaguzi katika Shule za Sekondari nchini.

6.2.1 Mapendekezo ambayo Hayajatekelezwa

Mfumo wa Nyongeza wa Mafunzo

Kama ilivyoelezewa kwenye kipengele 6.2 hapo juu, pendekezo moja (1) kati ya 12 yaliyotolewa halikutekelezwa (Rejea

kiambatanisho 3). Ukaguzi ulibaini kuwa suala la ufaulu duni kwa wanafunzi halipewi kipaumbele kwa sababu halipo kwenye miongozo inayotolewa kwa wakaguzi wala kwenye mipango ya utekelezaji ya mwaka. Kwa hiyo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ulipendekeza kuwa shule ziwe na mifumo itakayoonyesha uhitaji wa mafunzo ya ziada kwa wanafunzi wasiofanya vizuri.

Masomo ya Ziada

Ili kuweza kuwajibika kwenye pendekezo lililotolewa, masomo ya ziada yalipaswa kufanywa na walimu katika shule baada ya muda wa masomo na siku za jumamosi. Hata hivyo, masomo ya ziada kwa sasa hayafanyiki kikamilifu na hakuna ufuatiliaji wowote unaofanywa na idara ya ukaguzi mashuleni toka wizarani. Sababu iliyotolewa ni kuwa, masomo ya ziada yalikuwa yanafanyika kikamilifu kipindi ambacho wanafunzi waliofeli kidato cha pili hawakuwa wanarudia darasa, kwa hiyo masomo ya ziada yalifanyika kusaidia kuboresha uelewa wa wanafunzi. Kwa sasa yanafanyika kwa kiasi na kwa shule chache.

Wakati wa mahojiano yaliyofanywa kwa maafisa wa juu toka idara ya ukaguzi, ilibainishwa kuwa, idara ya ukaguzi mashuleni itafanya ufuatiliaji kwa kuwa masomo hayo ya ziada ni muhimu sana katika kuongeza uelewa kwa wanafunzi.

Uchambuzi zaidi ulifanywa wa mapendekezo kwa kila mgawanyo wa makundi kama unavyoonyeshwa hapa chini kwenye Jedwali 6.1:

Jedwali 6.1: Idadai ya Mapendekezo Yasiyotekelezwa kwa Mgawanyo

Mgawanyo wa Mapendekezo	Jumla ya Idadi ya Mapendekezo yaliyotolewa kwa mgawanyo	Idadi ya Mapendekezo yasiyotekelezwa
Udhibiti Ubora	1	-
Kujenga Uwezo	1	-
Ufuatiliaji, Tathmini na Usimamizi	2	-
Mgawanyo na utumiaji wa rasilimali	2	-
Usimamizi wa Ufanisi	3	1
Utoaji wa taarifa na mawasiliano	3	-

Jedwali 6.1 linaonesha kuwa pendekezo linalohusiana na usimamizi wa ufanisi katika ukaguzi wa shule halijajafanyiwa kazi wakati mapendekezo mengine aidha yametekelezwa kwa kikamilifu au kwa kiasi tu.

Hii inaonyesha kuwa kutokana na kushindwa kufanya usimamizi wa ufanisi kikamilifu kwa wadau wote wa ukaguzi mashuleni unazuia uwezekano wa kufikia lengo la kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata elimu yenye ubora.

6.2.2 Mapendekezo Yaliyotekelezwa kwa Kiasi

Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa unaonyesha kuwa, mapendekezo 5 kati ya 12 yalitekelezwa kwa kiasi tu (Rejea kiambatisho 3). Jambo kubwa lililojitokeza wakati wa kufanya ukaguzi na sababu ya mapendekezo hayo kutekelezwa kwa kiasi ni kama ilivyoainishwa hapa chini:

Pendekezo 1.2: Marekebisho Muhimu ya Muongozo wa Mafunzo wa Wakaguzi Shuleni

Wizara ya Elimu na mafunzo Stadi inapaswa kuhakikisha kuwa muongozo wa mafunzo kwa wakaguzi shuleni unafanyiwa marekebisho na kuwa na mtazamo wa kulenga kutatua matatizo badala ya mtizamo wa sasa ambao una maelezo ya kina

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali imebaini kuwa hakukuwa na kipaumbele kilichowekwa au muongozo kwa mipango ya mwaka ya utekelezaji wa kaguzi za shule wenye lengo la kutatua tatizo la ufaulu duni kwenye masomo ya sayansi na hisabati kwa shule za sekondari. Pendekezo lililotolewa ni kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo Stadi kuhakikisha kuwa muongozo wa mafunzo kwa wakaguzi shuleni unafanyiwa marekebisho ili kuweza kutatua matatizo ya ufaulu duni.

Utekelezaji uliokuwa unatakiwa ni kurekebisha muongozo wa ukaguzi kwa miaka ya fedha 2010/2011 na 2014/2015. Marekebisho yaliweza kufanyika mwaka 2010/2011 lakini kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 marekebisho hayajafanyika kutokana na ucheleweshaji wa kutoa fedha.

Pendekezo 2.2: Kuipatia Idara ya Ukaguzi vifaa na fedha

Wizara ya Elimu inatakiwa ihakikishe kuwa idara ya ukaguzi inawezeshwa kikamilifu kifedha na vifaa vya kazi ili kuweza kuifanya iwe na ufanisi.

Wakati wa kufanya ukaguzi ilibainika kuwa, Idara ya Ukaguzi wa shule haijafanya ufuatiliaji wowote wa ufanisi wa mawasiliano yake, wala hakuna majumuisho ya taarifa yaliyofanywa. Hii ilisababishwa

na ukosekanaji wa rasilimali watu, usafiri, vifaa vy maofisini na nyumba. Ukaguzi ulipendekeza kuwa, Wizara ya Elimu ihakikishe kuwa idara ya Ukaguzi wa shule inawezeshwa kikamilifu na kupatiwa vifaa muhimu ili kuboresha utendaji wake.

Utekelezaji uliofanyika ulikuwa ni kuhakikisha kuwa idara ya ukaguzi inapata pesa za kutosha. Pia kuna mpango unaondelea wa kununua magari 36 ambayo tayari yameshaagizwa. Idara ya ukaguzi wa shule kwa sasa imeweza kuongeza kiwango cha uchangiaji wa ukaguzi unaofanyika kutoka shilingi 500 mpaka shilingi 1000 kwa mwanafunzi kwa mwaka katika vyuo vya ualimu, shule za sekondari na shule za msingi za Serikali na za watu binafsi.

Pendekezo 3.1: Kuandaa njia bora ya kufanya mawasiliano

Idara ya Ukaguzi Shuleni inapaswa kuandaa njia bora ya mawasiliano na wadau husika kuhusiana na matokeo ya ukaguzi uliofanywa katika shule kwa kuandaa taarifa binafsi na zile za pamoja.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali imebaini kuwa hakukuwa na ufuatiliaji na tathmini za mara kwa mara kwa kaguzi za shule zilizofanyika licha ya kuwa ni jambo muhimu linalowezesha kujifunza kwa kupitia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye ukaguzi uliopita. Pendekezo lililotolewa kwa Idara ya Ukaguzi wa shule lilikuwa ni kuandaa mfumo wa mawasiliano ulio bora kwa kuzingatia wadau ili kuandaa taarifa inayotokana na ukaguzi uliofanywa.

Hatua iliyochukuliwa na idara ya ukaguzi ni kuanzisha mfumo wa usimamizi wa utoaji wa taarifa (IMIS) mwaka 2011 na kwa sasa huu mfumo upo kwenye majaribio kwa wilaya 7. Kwa kutumia mfumo huu (IMIS) taarifa na mrejesho zinatumwa kwa wadau wa pande zote husika. Mfumo huu (IMIS) hautumiki katika maeneo mengi kwa kuwa unajaribiwa katika Wilaya 7 tu kati ya Wilaya 168 zilizopo nchini.

Kadhalika, mpaka sasa hakuna tathmini iliyofanyika ili kubaini ubora wa mfumo huu mpya. Hata hivyo mahojiano yaliyofanywa na uongozi wa Wizara ya Elimu yanaonyesha kuwa Wizara inapanga kufanya tathmini kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2015 endapo fedha zitatolewa kwa wakati.

Pendekezo 3.2: Utoaji wa Miongozo ya Mafunzo kwa Vitendo kwa Wadau Wote

Idara ya Ukaguzi shuleni inapaswa kuhakikisha kuwa mapendekezo kwa walimu, wakuu wa shule na wadau wengine wanatoa miongozo ya vitendo zaidi ambayo inaendana na hali iliyoonekana na kujadiliwa kwenye shule zilizokaguliwa.

Kuhusu kukosekana kwa ufuatiliaji wa mara kwa mara na tathmini kwa kaguzi zilizofanyika, idara ya ukaguzi wa shule walitakiwa kuhakikisha kuwa mapendekezo kwa walimu, wakuu wa shule na wadau wengine yanatoa muongozo wa vitendo unaolingana na hali halisi iliyobainika na kujadiliwa kwa shule zulizokaguliwa.

Mkakati uliowekwa ulikuwa ni kuwahimiza wamiliki wa shule na wakuu wa shule kutoa mrejesho kwa mkaguzi mkuu wa kanda kuhusu namna walivyofanyia kazi mapungufu yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi. Wakati wa ufuatiliaji, ilibainika kuwa pendekezo hili limetekelezwa kwa kiasi tu kwa kuwa mrejesho unatolewa kwa baadhi ya shule zilizokaguliwa. Sababu iliyotolewa kuhusu shule nyingine kutokutoa mrejesho ilikuwa ni uzembe wa baadhi ya wamiliki na wakuu wa shule. Kadhalika, idara ya ukaguzi shuleni imebainisha kuwa wanafanya mpango wa kuanza kufanya ufuatiliaji kwa shule ambazo hazitoi mrejesho kwa wakati.

Pendekezo 4.6: Kuhamasisha Ufanisi kwenye Kaguzi za Shule

Idara ya ukaguzi inapaswa kuhakikisha kuwa uongezekaji wa idadi za shule za sekondari una uwiano na idadi ya wakaguzi kwa ili kuongeza ufanisi kwenye kaguzi za shule za sekondari.

Katika suala hilohilo la kukosekana kwa ufuatiliaji wa tathmini za kaguzi zilizofanyika mara kwa mara, Idara ya Ukaguzi shuleni ilishauriwa kuhakikisha kuwa ongezeko la idadi za shule za sekondari unawiana na idadi ya wakaguzi kama inavyoonyeshwa kwenye viwango ili kuboresha ufanisi kwenye kaguzi zinazofanyika katika shule za sekondari.

Mpango uliowekwa na idara ya ukaguzi shuleni ilikuwa ni kuajiri wakaguzi zaidi. Walimu 217 wameshajiunga na idara ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Kuna maombi 309 yanasubiri usaili na walimu watakao chaguliwa watajiunga na Idara ya Ukaguzi. Kwa sasa wanahitajika wakaguzi 502.

Aidha, suala la kuongeza wakaguzi zaidi ni zoezi endelevu kwa kuwa wengine wanastaafu, wenkawenda kufanya kazi maeneo mengine na/au wengine wanafariki.

6.2.3 Mapendekezo Yaliyotekelezwa kikamilifu

Kama ilivyoonyeshwa kwenye Kielelezo 6.1, mapendekezo ambayo yametekelezwa kikamilifu ni 6 kati ya 12 (50%). Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali imeridhishwa na utekelezaji huo na vithibitisho vimeonekana. Aidha, mapendekezo yote hayo 6 ambayo yametekelezwa kikamilifu yanahitaji kufuatiliwa tena mwakani (**Rejea kiambatisho 3**)

Mapendekezo ambayo yametekelezwa kikamilifu yalikuwa yanashughulikia mambo yafuatayo:

a) kushughulikia ufaulu duni wa wanafunzi kama mtazamo mkuu kwenye muongozo wa mwaka wa idara ya ukaguzi;

b) majumuisho ya taarifa zilizochambuliwa na tathmini zilizofanywa kuhusiana na ufaulu duni wa wanafunzi/ shule;

c) hatua zilizochukuliwa na shule za sekondari kukabiliana na suala la kiwango kikubwa cha wanafunzi kufeli wanafunzi kwenye masomo ya sayansi na hisabati yanaonyeshwa kwa umakini kwenye taarifa za ukaguzi;

d) kuwa na mpangilio wa majadiliano,semina/ mafunzo na walimu wa masomo ya sayansi na hisabati kuhusu na namna ya kuboresha ufundishaji na ufanisi kwenye kufundisha masomo hayo;

e) kuweka mifumo ya ufuatiliaji ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye ukaguzi; na

f) Kuandaa viwango vya uwiano wa wakaguzi au walimu ambavyo vitatumika kama kipimo cha ubora wa elimu nchini.

6.3 Hitimisho na Matarajio

Kwa lengo la kuleta mabadiliko kwenye ukaguzi uliofanyika kuhusiana na Usimamizi wa Ukaguzi wa Shule za Sekondari, utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni wa muhimu sana. Kwa mantiki hii, ufuatiliaji inabidi ufanyike tena mwakani kwa kuwa ni asilimia 50 tu ya mapendekezo yaliyotolewa ndio iliyotekelezwa kikamilifu, asilimia 42 ilitekelezwa kwa kiasi na asilimia 8 haikutekelezwa kabisa. Ufuatiliaji utasaidia kuainisha hali ambayo huenda ikafikiwa kwa yale mapendekezo yaliyotekelezwa kwa kiasi tu na lile ambalo halijatekelezwa kabisa.

SURA YA SABA

KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA UFANISI KUHUSU USIMAMIZI NA UDHIBITI WA TAKA NGUMU KWENYE MIJI MIKUU NA MIKOA NCHINI

7.1 Usuli wa Ukaguzi

Taarifa ya ukaguzi kuhusiana na usimamizi wa taka ngumu katika miji mikuu na mikoa ya Tanzania ilipelekwa bungeni mwezi April mwaka 2009. Wakaguliwa wakuu walikuwa ni Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia idara ya Mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na halmashauri sita zilizochaguliwa ambazo ni Manispaa ya Ilala, Kinondoni na Temeke na miji ya Arusha, Mbeya na Mwanza.

Lengo kubwa la ukaguzi ilikuwa ni kutathmini kama shughuli za usimamizi wa taka ngumu kwa halmashauri zilizochaguliwa nchini Tanzania zinafanywa kwa ufanisi kwa kuzingatia huduma zinazotolewa na watoa huduma, ufuatiliaji wa shughuli za taka ngumu, usimamizi wa ukusanyaji wa ada za huduma ya kuzoa taka taka, usimamizi wa mikataba baina ya wakandarasi na manispaa/jiji na usahihi wa mfumo wa ufuatiliaji wa serikali kuu.

Ukaguzi ulilenga kwenye usimamizi wa shughuli za taka ngumu kwa halmashauri zilizochaguliwa nchini Tanzania.

Ukaguzi ulibaini kuwa, kiwango cha taka ngumu ambacho hakizolewi kutoka kwenye halmashauri kinaongezeka kwa kasi. Katika halmashauri sita zilizokaguliwa kiwango cha taka ngumu ambacho hakikuzolewa kilikuwa ni zaidi ya 50% ya taka zote zinazozalishwa. Ufanisi katika usimamizi wa utoaji wa huduma za taka ngumu kati ya wadau wa kutoa huduma kwenye halmashauri mbali mbali unatofautiana, na mfumo wa sasa wa usimamizi wa taka ngumu ni mbovu kwa kuwa hauna mgawanyo wa majukumu kati ya utoaji wa huduma na ufuatiliaji katika halmashauri/jiji.

Ukaguzi pia ulibaini kuwa halmashauri tano kati ya sita zilizokaguliwa zimebinafsisha huduma za usimamizi wa taka ngumu kwa wakandarasi au Vikundi vya kijamii ambao ndio wanaokusanya taka na ada. Kadhalika, wakandarasi hao, wengi hawana uwezo wa

kukusanya taka ngumu na ada na pia hawana kibali cha kuwalazimisha wakazi kulipa ada ya taka ngumu.

Pia ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na mapungufu kwenye utaratibu wa kuteua wakandarasi /vikundi vya uzoaji taka kwa kuwa wakandarasi wengi au taasisi za kijamii zilizoteuliwa zilikuwa zinafanya kazi chini ya kiwango na wakati mwingine walitelekeza kazi zao baada ya muda mfupi.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ilibaini kuwa, malengo yaliyowekwa la ukusanyaji wa taka ngumu yalikuwa chini ya kiwango. Halmashauri zote zilizokaguliwa zilikuwa zinafanya ukaguzi bila kuwa na muda maalum wa kufanya ukaguzi huo. Hakukuwa na halmashauri hata moja yenye mpango ulioandaliwa wa uchunguzi ambao una vipaumbele na malengo yakinifu. Ni mara chache vikwazo vilikuwa vinawekwa na hakukuwa na viwango wala sera za kitaifa zilizokuwa zimeandaliwa. Serikali kuu pia haikufanya ufuatiliaji wa kutosha na tathmini ya shughuli za taka ngumu.

7.2 Utekelezaji wa Jumla wa mapendekezo yaliyotolewa

Kwa ujumla, mapendekezo 39 yalitolewa na ofisi ya Ukaguzi. Katika mapendekezo hayo; asilimia 28 yalitekelezwa kikamilifu (11 kati 39), asilimia 41 (16 kati 39) yalitekelezwa kwa kiasi na asilimia 31 (12 kati 39) hayakutekelezwa kabisa. Kielelezo 7.1 kinafafanua zaidi.



Kielelezo 7.1: Utekelezaji wa Jumla wa Majumuisho ya mapendekezo ya ukaguzi wa ufanisi Kuhusu usimamizi wa taka ngumu kwenye Miji Tanzania

Kadhalika, kati ya mapendekezo 11 ambayo yalitekelezwa kikamilifu, mapendekezo 2 (sawa na asilimia 18) yalitekelezwa na idara za serikali toka ngazi ya kitaifa. Mapendekezo mengine 9 (sawa na asilimia 82) yalitekelezwa kikamilifu na ngazi za Halmashauri.

Kati ya mapendekezo 16 ambayo yalitekelezwa kwa kiasi, ngazi ya taifa ilitekeleza kwa asilimia 38 na halmashauri ilitekeleza kwa asilimia 62. Vivyo hivyo, mapendekezo yaliyobakia 12 ambayo hayakutekelezwa kabisa, nusu ya mapendekezo hayakutekelezwa na ngazi ya Taifa na nusu hayakutekelezwa na halmashauri (Rejea Kielelezo 7.2)



Kielelezo 7.2: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwa Ngazi ya Taifa na Halmashauri

7.2.1 Mapendekezo ambayo Hayakutekelezwa

Kama ilivyoelekezwa kwenye kipengele 7.2 hapo juu, maendekezo 12 kati ya 39 hayakutekelezwa kabisa (Rejea Kiambatanisho 4). Sababu zilizotolewa kwa kutokutekelezwa na athari zake ni kama inavyoelezewa hapo chini:

Pendekezo 1: Kuandaa ukusanyaji mzuri wa ada za taka Ngumu

TAMISEMI ilitakiwa kuongoza halmashauri katika uandaaji wa mfumo wa usimamizi wa taka ngumu, ambapo ukusanyaji mzuri wa ada za taka ngumu ilikuwa ni jambo la msingi. Ilitakiwa kuziagiza halmashauri hizi kuandaa namna sahihi ya ukusanyaji wa ada za taka ngumu na kuwa na kumbukumbu ya wote wanaotakiwa kulipa ada. Ulipaji wa ada za taka ngumu ulioandaliwa ulitakiwa kuwa na vigezo vifuatavyo: Kiwango sahihi cha kulipa ada; kuzingatia gharama sahihi za uendeshaji shughuli za usimamizi wa taka ngumu na makadirio ya taka ngumu yanayotegemewa kukusanywa.

Kupitia mahojiano yaliyofanywa na uongozi wa Idara ya Uendelezaji miji iliyopo TAMISEMI, ilibainika kuwa halmashauri hazikuandaa mfumo mzuri wa ukusanyaji wa ada za taka ngumu ambao ungekidhi kigezo cha uendeshaji na gharama sahihi za usimamizi wa shughuli za taka ngumu. Sababu kubwa iliyotolewa ilikuwa ni kuchelewa kutolewa kwa fedha. Lakini Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali haikuridhishwa na sababu hii kwa kuwa inaonekana kabisa pendekezo hili halijapewa mkazo licha ya kuwa taarifa ya ukaguzi huu ilipelekwa bungeni mwaka wa fedha 2009. Athari zake ni kuwa, halmashauri hazifahamu kiwango sahihi kinachotakiwa kulipwa kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa taka ngumu na makadirio ya taka ngumu zinazotegemewa kukusanywa.

Pendekezo 2: Utenganishaji wa majukumu yanayohusiana na ukusanyaji wa ada za taka ngumu na utoaji wa huduma ambapo kwa sasa majukumu yote yanafanywa na wakandarasi wa uzoaji wa taka ngumu

TAMISEMI ilitakiwa kutenganisha jukumu la ukusanyaji wa ada za taka ngumu na utoaji wa huduma (ukusanyaji wa taka ngumu. Halmashauri zilitakiwa kuchukua jukumu la ukusanyaji wa ada za taka ngumu na kumlipa mkandarasi na kuliacha jukumu la ukusanyaji wa taka ngumu lifanywe na mkandarasi .

Mahojiano yaliyofanywa na uongozi wa Idara ya Uendelezaji Miji wa TAMISEMI ulibaini kuwa, jitihada zinahitajika ili pendekezo hili liweze kutekelezwa. Hii ni kwa sababu, licha ya shughuli za utekelezaji wa suala hili kupangiwa bajeti, Wizara ya Fedha bado haijatoa pesa za kuweza kusaidia kutekeleza jukumu hili. Kwa sasa kilichofanyika ni uundaji wa kikundi kazi ambacho kilipewa jukumu

la kutoa mapendekezo yatakayotumika kutengeneza muongozo wa usimamizi wa taka ngumu. Kadhalika haijulikani ni lini pendekezo la utenganishaji wa jukumu la ukusanyaji wa ada na utoaji wa huduma litatekelezwa. Kwa sasa yote haya yanafanywa na wakandarasi.

Pendekezo 3: Utenganishwaji wa jukumu linalohusiana na manunuzi, utoaji wa huduma na ufuatiliaji

TAMISEMI ilitakiwa kuhakikisha kuwa kuna na mgawanyo wa majukumu ya tenda za kuteua wakandarasi wa uzoaji wa taka ngumu, utoaji wa huduma na ufuatiliaji katika halmashauri. Majukumu haya yanapaswa kufanywa na watendaji tofauti ili kuweza kuboresha ufanisi na uwajibikaji kwenye shughuli za usimamizi wa uzoaji wa taka ngumu.

Ilibainika kuwa, TAMISEMI haijalipa kipaumbele utekelezaji wa pendekezo hili. Kwa kupitia taarifa mbalimbali na mahojiano yaliyofanywa na uongozi wa TAMISEMI kupitia idara ya Uendelezaji wa Miji ilibainika kuwa, mgawanyo huu haujafanyika. Katika halmashauri maafisa wengi wenye jukumu la utoaji wa huduma za ukusanyaji wa taka ngumu, ndio wanaofanya ufuatiliaji wa ufanisi wa shughuli zinazofanywa na wao wenyewe. Sababu iliyotolewa ni ile ile ya ucheleweshwaji kutolewa kwa fedha ili mgawanyo wa majukumu ukamilike. Hii inaathiri ufanisi wa shughuli za ufuatiliaji kwa kuwa sio sahihi kwa ofisa kujitathmini au kufuatilia shughuli anazofanya yeye mwenyewe.

Pendekezo 5: Kuandaa orodha ya kujifanyia tathmini

TAMISEMI ilitakiwa kutumia taarifa ya ukaguzi wa usimamizi wa taka ngumu uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuandaa orodha au dondoo ambazo zingeziwezesha Halmashauri kujifanyia tathmini na Wizara iweze kupata muelekeo wa kinachoendelea nchini kuhusu usimamizi wa shughuli za taka ngumu.

Wakati ufuatiliaji unafanywa kuhusu na utekelezaji wa pendekezo hili, ilibainika kuwa, TAMISEMI haijatekeleza jukumu hili. Sababu iliyotolewa ilikuwa ni kukosekana kwa mtaalamu wa masuala ya taka ngumu katika kitengo cha Uendelezaji Miji kilichopo TAMISEMI. Sababu hii haijitoshelezi kwa kuwa sheria inaruhusu TAMISEMI kuteua mtaalamu kwa mkataba pale anapohitajika ili aweze

kutekeleza jukumu hilo. Athari za hii hali ni kuwa kwa sasa halmashauri hazijifanyii tathmini na wakati huo huo wizara inakosa taarifa ya nini kinachoendelea nchi nzima.

Pendekezo 10: Ufuatiliaji na tathmini za shughuli za usimamizi wa taka ngumu

TAMISEMI, inapaswa kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za taka ngumu kwa nchi nzima. Pia inatakiwa kuwa na mpango tathmini na ufuatiliaji.

Ufuatiliaji uliofanywa ili kujua utekelezaji wa pendekezo hili ulibaini kuwa, viashiria vya ufuatiliaji kwa shughuli za usimamizi wa taka ngumu havijaingizwa kwenye mpango wa wizara wa ufuatialiaji na tathmini (M&E), na hakuna ushahidi kuwa viashiria hivi vinatumika kwenye ufuatiliaji na tathmini unaofanywa na idara ya Sera na Mipango. Hii inatokana na kukosekana kwa mipango ya kutosha ya kuwezesha kutekeleza pendekezo hili.

Pendekezo 12: Viwango vya usimamizi wa shughuli za taka ngumu

Taasisi ya viwango nchini inapaswa, kwa mujibu wa sheria[8], kuweka viwango vya usimamizi wa taka ngumu ambavyo vinapaswa kufuata na halmashauri zote wanapotimiza majukumu yao ili kuhakikisha kunakuwa na usawa kwenye huduma zitolewazo.

Mapitio ya utekelezaji wa pendekezo lililotolewa kwa taasisi ya viwango (TBS) unaonyesha kuwa, hakuna viwango vilivyoandaliwa na TBS kuhusiana na usimamizi wa shughuli za taka ngumu. Jambo hili linaathiri ubora wa shughuli za usimamizi wa taka ngumu zinazofanywa na halmashauri kwa kuwa hakuna viwango ambavyo vingeweza kusimamia usawa wa utoaji wa huduma hizi.

Pendekezo 14: Kukadiria kiwango cha uzalishwaji wa taka ngumu

Kitengo cha usimamizi wa shughuli za taka ngumu kwenye halmashauri kilipaswa kuandaa mfumo wa taarifa za usimamizi wa taka ngumu ambao utategemewa na Halmashauri kukadiria kiwango cha taka ngumu kinachozalishwa na kukusanywa kwa mwaka.

---

8 Sheria ya usimamizi wa mazingira Na.20 ya mwaka 2004, Pamoja nasheria ya udhibiti wa viwango ya mwaka 1975

Mapitio ya utekelezaji wa pendekezo hili unaonesha kuwa pendekezo hili halijatekelezwa, Mpaka sasa, halmashauri zimeweza kufanya zoezi la tathmini kuhusiana na uhitaji wa kuanzishwa kwa mfumo wa taarifa wa pamoja wa usimamizi wa taka ngumu tu. Pia jitihada zimefanyika kuanzisha mfumo wa taarifa wa kijiografia (GIS) ambao umeunganishwa kwa halmashauri 26 tu kati ya halmashauri 168 zilizopo mpaka sasa na hakuna ufafanuzi wa namna gani mfumo huu utatumika kusaidia kukadiria kiwango cha uzalishaji na ukusanyaji wa taka ngumu kwa kila mwaka. Matokeo ya hali hii, halmashauri 142 ambazo hazijaunganishwa kwenye mfumo huu wa taarifa wa kijiografia (GIS) zinafanya kazi bila kuwa na mfumo wa taarifa wa usimamizi wa taka ngumu ambao ungesaidia kwenye kukadiria kiwango cha taka ngumu kinachozalishwa na kukusanywa.

Pendekezo 21: Ufanyaji wa hesabu sahihi wa kaya, biashara na viwanda katika kila kata

Ili kuboresha ukusanyaji wa taarifa za taka ngumu, idara ya uhasibu kwenye halmashauri inapaswa kuwa na hesabu kamili ya kaya, biashara na viwanda vilivyopo kwenye kila kata, pamoja na taarifa kuhusiana na kiasi gani kila kaya au taasisi kinapaswa kulipa kama ada za shughuli za ukusanyaji wa taka ngumu na kiasi gani kilicholipwa.

Kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanywa na uongozi wa idara ya Uendelezaji Miji ya TAMISEMI ilibainika kuwa, hakuna mfumo wowote ulioanzishwa wa kuhifadhi taarifa zote za kaya, biashara na viwanda katika kila kata. Hivyo basi pendekezo hili halijatekelezwa kabisa. Kadhalika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali imegundua kuwa, TAMISEMI na halmashauri wanajaribu kuhusisha suala hili na utafiti uliofanywa kuhusu na ukusanyaji wa mapato ambao unakadiria kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa shughuli za uzoaji wa taka ngumu. Mapitio ya nyaraka zaidi yaliyofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kuhusiana na taarifa ya utafiti huo wa ukusanyaji wa mapato umebainisha kuwa, hakuna kipengele chochote kinachohusiana na kiasi ambacho kaya au taasisi kinadaiwa au kiasi kilicholipwa.

Pendekezo 22: Kuanzisha mfumo wa mahesabu

Halmashauri zinapaswa kuwa na mfumo thabiti wa hesabu ambao unaweza kuhifadhi taarifa zote zinazohusiana na idadi ya kaya, biashara na viwanda katika kata husika ili kuweza kuwa na orodha ya vyanzo muhimu vya mapato na kuepuka upotevu wa mapato unaofanywa na wakandarasi.

Vivyo hivyo, mapitio ya utekelezaji wa pendekezo hili ulibaini kuwa, pendekezo hili halikutekelezwa kwa sababu mfumo wa hesabu wenye kuweka taarifa zote za kaya, biashara na viwanda katika kila kata haujaandaliwa.

Pendekezo 24: Jukumu la ukusanyaji wa ada za taka ngumu

Halmashauri zinapaswa kuwa na jukumu la kukusanya ada za taka ngumu na kuwalipa wakandarasi. Jukumu la wakandarasi litakuwa ni ukusanyaji wa taka ngumu tu.

Wakati wa kufuatilia utekelezaji wa pendekezo hili, uongozi wa idara ya Uendelezaji Miji ilibainisha kuwa, kwa sasa wadau wa ushauri wanakusanya maoni kuhusiana na suala la kutenganisha majukumu ili jukumu la wakandarasi liwe ni kutoa huduma tu na ukusanyaji wa ada kwa ajili ya shughuli za taka ngumu ufanywe na Halmashauri. Utekelezaji wa suala hili unategemea maoni ya wananchi.

Pendekezo 34: Mgawanyo wa shughuli za utekelezaji na ufuatiliaji

Kitengo cha afya kilichopo kwenye Halmashauri kinapaswa kuhakikisha kuwa kuna mgawanyo wa majukumu kati ya kazi za ufuatiliaji na utoaji wa huduma ndani ya idara ya usimamizi wa taka ngumu.

Ufuatiliaji uliofanywa ili kujua utekelezaji wa jukumu hili umebaini kuwa, TAMISEMI haijalipa suala hili kipaumbele. Mapitio ya taarifa mbalimbali na mahojiano yaliyofanyika yamebaini kuwa mgawanyo wa majukumu haya haujafanyika kwa sababu kwenye halmashauri nyingi bado maafisa ambao wanatekeleza majukumu ya utoaji wa huduma wa kuzoa taka ngumu ndio hao hao wanaofanya ufuatiliaji wa kiufanisi au kiutendaji. Kwa kiwango kikubwa hii imeathiri ubora wa ufuatiliaji unaofanywa kwa kuwa hakuna nafasi ya kujifunza ufanisi wa wadau wengine.

Pendekezo 38: Mgawanyo wa majukumu ya ukusanyaji wa ada za taka ngumu na utoaji wa huduma

Jukumu la kukusanya ada za taka ngumu linapaswa kuwa la Halmashauri na sio la mkandarasi. Idara ya uhasibu inatakiwa kuwajibika kukusanya ada za taka ngumu. Wakandarasi wanapaswa kulipwa ada na halmashauri kwa kusimamia shughuli za uzoaji taka. Ada inayokusanywa inaweza kulinganishwa na mambo mbali mbali kama vile eneo la ukusanyaji taka na kiwango cha taka ngumu kilichokusanywa. Mkandarasi anapaswa kukusanya taka ngumu tu na sio kukusanya ada kwa wananchi.

Mapitio ya nyaraka yaliyofanywa ili kujua kiwango cha utekelezaji wa pendekezo hili, ilibainishwa na uongozi wa idara ya Uendelezwaji wa Miji kuwa, kwa sasa wadau wa ushauri wanakusanya maoni kwa wananchi kuhusiana na jukumu la wakandarasi kuwa ni ukusanyaji wa taka tu na kuachia jukumu la ukusanyaji wa ada kuwa jukumu la halmashauri. Utekelezwaji wa suala hili unategemea na maoni ya wananchi.

Uchambuzi zaidi ulifanyika kuhusiana na mapendekezo yaliyotolewa kulingana na makundi kama unavyoonyeshwa kwenye jedwali 7.1:

Jedwali 7.1:Idadi ya Mapendekezo yasiyotekelezwa kwa makundi

Mkundi ya Mapendekezo	Jumla ya mapendekezo yaliyotolewa kwa makundi	Idadi ya mapendekezo yasiyotekelezwa
Uandaaji wa Mipango	3	1
Ufanyaji wa Maamuzi	1	-
Uandaaji wa bajeti	1	-
Ujengaji wa uwezo	1	-
Ufuatiliaji, Tathmini na Usimamizi	3	1
Utumiaji na mgawanyo wa rasilimali	1	-
Manunuzi na Usimamizi wa mikataba	1	-
Usimamiaji wa ufanisi	10	2
Mgawanyo wa majukumu	3	3
Usimamizi wa mapato	10	5
Usimamizi wa sheria na utekelezaji kwa mujibu wa sheria	3	1
Utoaji wa huduma	1	-
Utoaji wa taarifa na mawasiliano	1	-

Uchambuzi uliofanywa kwenye jedwali 7.1 unaonesha kuwa: mapendekezo kuhusu na usimamizi wa mapato yatokanayo na ukusanyaji wa taka ngumu; mgawanyo wa majukumu ya ukusanyaji wa taka ngumu. Uteuzi wa wakandarasi na ufuatiliaji na tathmini ya huduma inayotolewa; usimamiaji wa utendaji/ufanisi wa watoa huduma sambamba na ule wa watumishi wa halmashauri; uandaaji wa mipango ya utoaji wa huduma za usimamizi wa taka ngumu na usimamiaji wa sheria hazijatekelezwa. Mapendekezo mengine aidha yametekelezwa kikamilifu au kwa kiasi.

Kushindwa kutekelezwa kwa kiasi kikubwa cha mapendekezo yaliyotolewa kunawanyima nafasi wakaguliwa wakuu kuboresha huduma za usimamizi wa shughuli za taka ngumu pamoja na kuwakosesha wananchi huduma.

7.2.2 Mapendekezo yaliyotekelezwa kwa kiasi

Mapendekezo 16 kati ya 39 yalitekelezwa kwa kiasi tu (Rejea kiambatanisho 4). Mapendekezo yaliyotolewa kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Shirika la Viwango nchini na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na sababu na athari za kutekelezwa kwake kwa kiasi tu yameainishwa hapa chini.

Pendekezo 4: Manunuzi yanapaswa kufanyika kulingana na makisio ya gharama na kumchagua mkandarasi anayefaa

TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kuwa, Halmashauri zinachagua mkandarasi wa taka ngumu kwa kufuata kigezo cha makisio ya gharama ya kusimamia shughuli za taka ngumu katika kata husika na kumchagua yule ambae anafaa kulingana na vigezo vinavyoendana na hali halisi katika eneo.

Ufuatiliaji wa pendekezo hili umeonyesha kuwa, licha ya kuundwa kwa bodi ya zabuni kwenye Halmashauri, hakuna ushahidi uliotolewa kuhusiana ni namna gani bodi hizi zinafanya kazi zao za kuteua wakandarasi. Pia barua ya maelekezo iliyopelekwa kwenye halmashauri haijaweza kuonyesha hili.

Pendekezo 7: Matumizi ya mifuko ya plastiki katika kukusanya taka ngumu

Utafutwe uwezekano wa kutumia mifuko ya plastiki ambayo inauwezo wa kukaa kwa muda mzuri na yenye kiwango kizuri kwa ajili ya kukusanya taka ngumu.

Rejea zilizofanywa kuhusu utekelezaji wa pendekezo hili zimebainisha kuwa, pendekezo hili limetekelezwa kwa kiasi tu. Hakuna ushahidi uliotolewa na TAMISEMI, VPO na NEMC kuhusiana na kilichofanyika zaidi ya kuelezea kuwa mkutano wa wadau uliowahusisha TAMISEMI, VPO na NEMC ulifanyika na ulihusu kampeni ya usambazaji wa mpango kazi wa utunzaji wa mazingira wa mwaka 2013 uliojumuisha uzalishaji na matumizi ya mifuko ya plastiki.

Pendekezo 8: Kila Halmashauri inapaswa kujua au kuweza kukadiria kiasi cha mapato kinachoweza kukusanywa kwenye kata.

TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kuwa kila halmashauri inajua au inakadiria kiasi cha mapato yatokanayo na shughuli za taka ngumu ambacho kila mkandarasi au halmashauri ina uwezo wa kukusanya; na kuandaa uhalisia wa kiasi cha taka ngumu kinachozalishwa na kinachopaswa kukusanywa.

Wakati wa ufuatiliaji ili kujua kiwango cha utekelezaji wa pendekezo hili, haukupatikana ushahidi wowote unaoonesha kuwa halmashauri zimeandaa database kwa ajili ya wazalishaji muhimu wa taka ngumu na kiwango cha uzalishaji kwa siku, mwezi na mwaka; na kutumia taarifa hizo kuonyesha uhalisia wa kiwango cha taka ngumu kinachozalishwa na kinachopaswa kukusanywa. Vile vile mapitio ya mikataba inayotolewa kwa wakandarasi na sheria ndogo ndogo za halmashauri yameonesha kuwa, kwenye nakala hizi mbili kuna kipengele cha ada inayotakiwa kukusanywa na makadirio ya mapato yanayotarajiwa kukusanywa. Pia makadirio haya yanapatikana kwenye muongozo wa matumizi wa halmashauri (MTEF).

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inachukulia hali hii kuwa imechangiwa na TAMISEMI kushindwa kufanya ufuatiliaji kwenye Halmashauri ingawa sehemu ya shughuli zao za kila siku. Pia TAMISEMI imeshindwa kutekeleza pendekezo la ukaguzi lililotolewa mwaka

2009. Athari za hii hali ni kuwa TAMISEMI haina picha kamili ya baadhi ya shughuli zinazoendelea kwenye Halmashauri.

Pendekezo 11: Ujengaji wa uwezo na kuwatumia wafanyakazi wazoefu kama mameneja

Ujengaji wa uwezo unapaswa kuwa ni sehemu ya kutekeleza shughuli za usimamizi wa taka ngumu. Pia wafanyakazi wenye uwezo wanapaswa kutumika kwa kazi hii. Suala la elimu kwa jamii linapaswa lisipuuzwe. Halmashauri zinapaswa kuendelea kuelimisha jamii ili iweze kukabiliana na vigezo vinavyotakiwa na kanuni zilizopo.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imepitia taarifa toka TAMISEMI kwa lengo la kutathmini kiwango cha utekelezaji wa pendekezo hili na ikabaini kuwa pendekezo hili limetekelezwa kwa kiasi tu. Mafunzo yamefanyika katika halmashauri 26 ambazo zipo chini ya mradi wa TSCP na ULGSP wakati kwa ujumla kuna halmashauri 168 nchini. Hakuna mpango wowote uliooneshwa wa kuzifikia halmashauri 142 zilizobakia.

Pendekezo la 13: Sera na kanuni kuhusu taka ngumu

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia kitengo cha mazingira na Baraza la Usimamizi wa Mazingira nchini (NEMC) wanatakiwa kuandaa sera na kanuni ili zitumike kwa utekelezaji wa shughuli za taka ngumu nchini.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeandaa kuandaa sera ya usimamizi wa taka ngumu na imezisambaza kwenye mikoa na Halmashauri: Kanuni ya usimamizi wa taka ngumu na taka za mabaki ya binadamu bado zinasubiria kuthibitishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na imepelekwa huko kwa muda mrefu sasa. Lakini Idara ya huduma za kinga haina taarifa zozote kuhusiana na hatua iliyofikiwa ya uthibitishwaji wa kanuni kwa kuwa hakuna ufuatiliaji uliofanywa na idara hiyo. Hali hii inaathiri ufanisi wa shughuli za usimamizi wa taka ngumu nchini.

Kadhalika, VPO imefanikiwa kuandaa kanuni ambazo tayari zinatumika. Hata hivyo, Sera ya Taifa ya Mazingira ambayo itahusisha masuala ya taka ngumu bado haijafanyiwa maboresho licha ya pendekezo hili kutolewa miaka mingi. Sababu iliyotolewa ni

kuwa, kabla ya sera kuthibitishwa inapitia mchakato mrefu sana na hali hii inawalazimu kuendelea kutumia sera ya zamani.

Pendekezo 15: Kuweka viwango vinavyohitajika vya ufanisi na malengo kwa ukusanyaji wa taka ngumu

Kitengo cha usimamizi wa taka ngumu kwenye halmashauri kinapaswa kuandaa viwango vinavyohitajika kwa wakandarasi. Kitengo hiki kinapaswa kuhakikisha kuwa, lengo la taka ngumu zinazopaswa kukusanywa kwa kila kata linaandaliwa na mkandarasi anatakiwa kufuata vigezo hivyo.

Kulingana na mahojiano yaliyofanyika ili kutathmini kiwango cha utekelezaji wa pendekezo hili, ilibainika kuwa sio Halmashauri zote zilizoweka lengo. Hii ni kutokana na sababu mbali mbali kama vile uwezo wa wafanyakazi na ufinyu wa rasilimali. TAMISEMI kwa kupitia miradi yake mbalimbali kama vile TSCP na ULGSP imebainisha kuwa itaendelea kuzijengea uwezo Halmashauri ili kufanikisha lengo hilo. Hali hii hairidhishi kwa kuwa Halmashauri zenyewe zinatakiwa kuandaa tathmini ya uhitaji wa mafunzo kwa wafanyakazi wake. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilitegemea Halmashauri ziwe na wafanyakazi ambao ni wataalamu wa kuandaa vigezo hivyo vya ufanisi, na uwezo wa kuingia mikataba na wadau mbalimbali wenye utaalamu katika suala hili ili kuweza kutimiza jukumu hili. Zaidi ya hapo, taarifa ya ukaguzi huu wa usimamizi wa taka ngumu ilipelekwa bungeni toka mwaka 2009, kwa hiyo ilitegemewa mambo mengi yangekuwa yamefanyika kwa kuwa ni miaka sita sasa toka pendekezo hili lilipotolewa.

Pendekezo 18: Kuboresha mfumo wa kufuatilia ufanisi

Idara ya usimamizi wa taka ngumu ya halmashauri inapaswa kuboresha aina, kiasi na awamu za taarifa inayohitaji ili kuweza kufuatilia ufanisi wa watoa huduma wake. Katika kutekeleza hili, idara ya usimamizi wa taka ngumu inatakiwa kuweka wazi uhitaji wake wa taarifa, ikilinganisha na ukubwa uliowapa watoa huduma kutoa taarifa hizo. Pindi uhitaji wa taarifa utakapokuwa bayana kitengo kinapaswa kuhakikisha kuwa huduma zinatolewa kwa mujibu wa makubaliano.

Licha ya kuwa mipango mikakati ya halmashauri imekuwa ikifanyiwa marekebisho ya mara kwa mara, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

ilibaini kuwa, halmashauri hazijaweza kufanya maboresho kuhusiana na aina, kiasi na awamu ya taarifa muhimu kwa utoaji wa huduma za usimamizi wa taka ngumu. Vile vile, Halmashauri hazijaweza kuhakikisha kuwa taarifa toka kwa wakandarasi zinapelekwa kwenye halmashauri mara kwa mara kama ilivyopangwa. Matokeo ya hali hii ni ufuatiliaji hafifu wa ufanisi kwa shughuli za taka ngumu zinazofanywa na wakandarasi ambazo zinaonekana kufanywa kwa kushtukia tu kwani haziko kwenye mipango.

Pendekezo 19: Hatua sahihi zichukuliwe ili kuweza kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma

Idara ya usimamizi wa taka ngumu katika halmashauri inapaswa kuendelea kuandaa na kuanzisha uwezo wa kujisimamia wenyewe. Hapa kitengo kinatakiwa kuchukua hatua sahihi na kuweka kwenye maandishi maamuzi yanayofanywa ili kuweza kuimarisha na kuboresha ufanisi wa utoaji wa huduma.

Mapitio ya taarifa ya mafunzo yaliyofanywa ili kuweza kubaini kiwango cha utekelezaji wa pendekezo hili ulibaini kuwa uwezo unajengwa kwa lengo la kuboresha ufanisi wa utoaji wa huduma. Lakini suala la kufikia Halmashauri zote halizingatiwi kwani Halmashuri 142 hazijafikiwa na miradi ya TSCP na ULGSP ambayo inawezesha ujengaji wa uwezo.Sambamba na hilo shughuli za na usimamizi wa taka ngumu unaofanywa na miradi ya TSCP na ULGSP sio endelevu kwa kuwa miradi hii ni ya kipindi maalumu kilichoainishwa kwenye mkataba.

Pendekezo 20: Mfumo wa ada za taka ngumu

Halmashauri zinatakiwa kuanzisha mfumo wa ada za usimamizi wa taka ngumu ambao utajumuisha gharama zote za uendeshaji wa shughuli za taka ngumu. Hili litawezeshwa kwa kufanya mchanganuo wa bajeti zake na gharama za usimamizi wa shughuli hizo, na baadae kuainisha vyanzo vyote vya mapato ili waweze kukadiria mapato kamili ya makusanyo yanayopatikana. Pia halmashauri zinatakiwa kufanya utafiti kuhusiana na utayari wa wananchi kulipia gharama za uzoaji wa taka ngumu.

Mapitio yaliyofanywa kwenye taarifa mbalimbali ili kuweza kujua kiasi cha utekelezaji wa pendekezo hili umebainisha kuwa, utafiti wa

utayari wa kulipia gharama za usimamizi wa shughuli za taka ngumu umefanyika kwa baadhi ya Halmashauri, na matokeo ya utafiti huo yalitumika katika kuandaa mipango mikakati. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imepitia taarifa ya utafiti huo na mipango mikakati ya baadhi ya halmashauri na kubaini kuwa zinatekeleza pendekezo hili. Viwango vya utozaji wa ada vipo kwenye maandalizi. Kwa sasa ada zimekuwa zikitozwa na watoa huduma.

Pendekezo 26: Ukusanyaji wa ada za taka ngumu

Halmashauri kwa kushirikiana na idara ya usimamizi wa taka ngumu walitakiwa kuanzisha njia mpya ya ukusanyaji wa ada ya taka ngumu. Halmashauri zilipaswa kufanya mchanganuo wa vyanzo vya mapato na kuainisha vyanzo sahihi ili kuweza kujumuisha asilimia ya kiwango cha cha kuendeshea shughuli za taka ngumu.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliweza kupitia taarifa ya utafiti wa vyanzo vya mapato na kubaini kuwa vyanzo vya mapato vimeainishwa, lakini halmashauri hazijaweza kuanzisha njia mpya za ukusanyaji wa ada za taka ngumu. Uongozi wa TAMISEMI unachukulia suala hili kuwa toshelevu kwa kuwa inalilinganisha na utafiti uliofanyika katika halmashauri kuhusiana na vyanzo vya mapato. Hata hivyo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ilitegemea kukuta mbinu za namna ambavyo halmashauri itaongeza mapato kutoka vyanzo mbalimbali ambavyo kimsingi vinakosekana.

Pendekezo 27: Vigezo vya ufanisi kwa watoa huduma

Kitengo cha usimamizi wa taka ngumu kinapaswa kuandaa viashiria vitakavyotumika kutathmini utekelezaji wa mikataba ya watoa huduma. Viashiria hivi vinapaswa kuainishwa kwenye mikataba na pia ifuatiliwe kikamilifu ili kuhakikisha utoaji mzuri wa huduma. Ufuatiliaji utawezesha kitengo cha usimamizi wa taka ngumu kuweka namna ya uwajibikaji pindi kunapokuwa na kiwango cha chini cha ufanisi.

Kipindi ambacho ufuatiliaji unafanywa kuhusiana na utekelezaji wa pendekezo hili lililotolewa ilibainika kuwa, mikataba inayotolewa kwa watoa huduma inajumuisha pia viashiria ambavyo vinapaswa kufuatwa. Aidha, hakuna ushahidi unaoonesha kuwa viashiria hivyo vya ufanisi vinafuatiliwa na hatua sahihi zitachukuliwa endapo kutakuwa na ufanisi duni.

Pendekezo 28: Uchunguzi kwa watoa huduma

Idara ya usimamizi wa watoa huduma inapaswa kufanya utafiti wa kina na kufuatilia tafiti hizo zinazofanywa. Matokeo na hatua zinazopendekezwa kama matokeo ya tafiti yanapaswa yawekwe kwenye maandishi. Mapendekezo yanayopatikana toka kwenye tafiti zinazofanywa inapaswa yatumike kuimarisha ufanisi wa watoa huduma. Programu ya utafiti inapaswa kufuatilia maeneo hatarishi. Idadi za tafiti zinazofanywa zinapaswa ziendane na maboresho yatokanayo na tafiti hizo.

Mapitio ya taarifa za tafiti zilizotolewa kama ushahidi wa utekelezaji wa pendekezo hili haukuwa na viashiria vya maeneo hatarishi wala haukutokana na maboresho ya tafiti zilizopita.Matokeo yake kwa sasa uchunguzi unaofanyika hauzingatii matokeo ya uchunguzi uliopita.

Pendekezo 30: Kuboresha hatua za manunuzi ya watoa huduma binafsi

Kitengo cha manunuzi kinapaswa kuboresha vigezo vya ufuatiliaji na hatua za manunuzi ya wakandarasi wa taka ngumu ili kuhakikisha kuwa wale wakandarasi wanaokidhi vigezo tu ndio wanapewa mikataba. Tathmini ya kina ya uwezo wa kifedha, vifaa vya mzabuni, nguvu kazi na rasilimali nyingine inapaswa vifanyiwe tathmini nzuri kabla ya kuingia mkataba.

Mapitio yaliyofanywa ili kuweza kubaini hali ya utekelezaji wa pendekezo hili ilibaini kuwa hakuna kilichofanyika kinachoonesha kuwa kuna tathmini ya kina iliyofanyika ya uwezo wa kifedha, vifaa vya mzabuni, idadi ya wafanyakazi na rasilimali nyingine. Hii ni ishara kuwa tathmini ya kina haifanyiki ipasavyo.

Pendekezo 33: Mfumo wa kufuatilia ukiukwaji wa mikataba

Kitengo cha usimamizi wa taka ngumu kinapaswa kuandaa mifumo ya ufuatiliaji wa ukiukwaji wa mikataba inaofanywa na watoa huduma.

Mahojiano na uongozi wa idara ya Uendelezaji Miji na mapitio ya Mipango mikakati kipindi cha ufuatiliaji wa utekelezaji wa pendekezo hili ilibainika kuwa, hakukuwa na mfumo ulianzishwa wa kufuatilia ukiukwaji wa mikataba kutoka kwa wakandarasi.

Mipango mikakati iliyoandaliwa katika halmashauri 26 ambazo zipo chini ya miradi ya TSCP na ULGSP inaonesha nini kifanyike, na viashiria vipi vitumike kwenye ufuatiliaji wa taka ngumu. Jumla ya halmashauri 142 hazikuweza kufikiwa na miradi hii miwili, na shughuli ambazo zinafadhiliwa na miradi hii miwili sio endelevu kwa kuwa hii miradi inafanya kazi kwa kipindi maalum. Matokeo yake, ufuatiliaji wa ukiukwaji unaofanyika unatofautiana kutokana na kukosekana kwa mifumo thabiti.

Pendekezo 35: Kumuhusisha Mtafiti

Idara ya usimamizi wa taka ngumu inaweza ikamuhusisha mtafiti ili aweze kutafiti uzalishaji wa taka ngumu kwa kila kata na kuandaa makadirio yatakayotumika kama sehemu ya tathmini ya ufanisi kwa watoa huduma.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imebaini kuwa pendekezo hili limetekelezwa kwa kiasi tu kwa sababu hakuna ushahidi uliotolewa wa tafiti zilizofanyika kuanzisha kiwango cha uzalishaji taka ngumu kwa kila kata. Hali hii inaathiri usimamizi kwa kuwa kiwango cha uzalishaji wa taka ngumu kwenye kata hakijulikani.

7.2.3 Mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu

Jumla ya mapendekezo 11 ambayo ni sawa na asilimia 28 yalitekelezwa kikamilifu (rejea kiambatanisho 4). Aidha wakaguliwa wakuu ambao wametekeleza mapendekezo haya kwa kikamilifu (TAMISEMI, na Halmashauri) zinahitaji kuhakikisha kuwa hii hali endelevu ili kuweza kuboresha shughuli za usimamizi wa taka ngumu Tanzania.

Mapendekezo ambayo yametekelezwa kikamilifu yalikuwa yanahusisha mambo yafuatayo:

- Kuanzisha mfumo wa utaratibu kwa ajili ya wananchi kulipa ada ya taka ngumu;
- Kutafuta ushauri wa kisheria toka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweza kuona kama wakandarasi wanapaswa kutekeleza adhabu zilizoainishwa kwenye sheria ndogo za miji na manispaa;

- **Kutambua sababu za kuwa na utofauti kwenye utendaji/ufanisi miongoni mwa watoa huduma kwa kuzingatia kiwango, ubora na faida;**
- **Tathmini ya mara kwa mara kuhusiana na ufanisi wa watoa huduma;**
- **Kuweka sababu za kutoweza kukusanya ada za taka ngumu kama zilivyoainishwa kwenye sheria ndogo za halmashauri;**
- **Kutekeleza mikataba kwa kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa ukiukwaji wa mikataba na watoa huduma;**
- **Kusimamia kwa usahihi adhabu dhidi ya wale wanaokiuka taratibu za usimamizi wa taka ngumu;**
- **Kuweka viwango vya ufanisi kwa watoa huduma;**
- **Kuanzisha mfumo wa utoaji taarifa kati ya timu ya usimamizi wa taka ngumu na watoa huduma;**
- **Kuhakikisha kuwa kila mtoa huduma wa taka ngumu ana mfumo mzuri wa kuhakikisha ufuatiliaji wa viwango na ubora ni wa uhakika; na**
- **Kuhakikisha kunafanyika bajeti ya msingi ili kuweza kutambua gharama ya ukusanyaji wa taka ngumu kwenye manispaa ambayo itajumuisha makadirio ya gharama kwa viwango mbalimbali vya asilimia ya taka ngumu zilizokusanywa.**

7.3 Hitimisho na Matarajio

Wakaguliwa katika ukaguzi wa usimamizi wa taka ngumu ambao ni Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jami, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Taasisi ya Viwango Tanzania na Tawala za Serikali za Mitaa wanatakiwa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.Sehemu kubwa ya mapendekezo yaliyotolewa hayakutekelezwa kikamilifu. Ni asilimia 28 ya mapendekezo yaliyotolewa ndio yaliyotekelezwa kikamilifu. Asilimia 41 yametekelezwa kwa kiasi tu na asilimia 31 hayajatekelezwa kabisa.

Kwa hiyo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali itafanya ufuatiliaji tena mwaka ujao ili kuweza kutathmini utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na kujua kama kutakuwa na maboresho.

SURA YA NANE

KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA UFANISI WA USIMAMIZI WA UJENZI WA BARABARA NCHINI

8.1 Usuli wa Ukaguzi

Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi kuhusiana na muda wa, gharama na ubora wa ujenzi wa barabara nchini iliwakilishwa bungeni mnamo mwezi Machi 2010.Wakaguliwa wakuu walikuwa ni Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Bara bara (TANROADS) nchini.

Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini kama Wizara ya ujenzi na Wakala wa barabara nchini zimeweza kuainisha matatizo ya ucheleweshaji, ongezeko la gharama na ubora kwenye barabara nchini na kupunguza matatizo haya kwa kutumia rasilimali zilizopo. Ukaguzi ulilenga hasa kwenye miradi ya ujenzi wa barabara ambayo inasimamiwa na Wakala wa Barabara nchini makao makuu na Wizara ya Ujenzi.

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na ongezeko la muda kwenye miradi ya ujenzi wa barabara ambao haukuwa umedhibitiwa vizuri na Wizara ya Ujenzi Wakala wa Barabara nchini. Aidha ilibainika kuwa kulikuwa na usanifu duni wa miradi ya ujenzi wa barabara nchini ambapo ilisababisha kuongezeka kwa gharama na hivyo kuathiri bajeti iliyotengwa. Mwisho, ilibainika kuwa kulikosekana ufanisi katika usimamizi ubora wa barabara nchini. Hii inatokana na kukosekana kwa viwango vya udhibiti kwenye hatua ya uandaaji wa miradi ya ujenzi wa barabara.

8.2 Hali ya Ujumla ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali imebaini kuwa Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara nchini wameweza kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa kwa ngazi mbalimbali. Kielelezo 6.1 kinaonyesha kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo 20 yaliyotolewa kama yalivyofanyiwa uchambuzi kulingana na hali halisi iliyopo mpaka kufikia tarehe 31 Oktoba 2014.



Kielelezo 8.1: Utekelezaji wa Mapendekezo 20 yaliyotolewa kwa Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara nchini

Kielelezo 8.1 kinaonesha kuwa Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara nchini zimeweza kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa kwa asilimia 65. Katika mapendekezo 20 yaliyotolewa, mapendekezo 2 hayajatekelezwa wakati asilimia 25% yametekelezwa kwa kiasi tu na yanahitaji kufuatiliwa zaidi. Kwa ujumla , Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara nchini bado zinahitajika kuendelea kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Ofisi ya Ukaguzi wa Hesabu ambayo hayajatekelezwa kabisa au yametekelezwa kwa kiasi tu.Hii ni kwa kuwa mapendekezo haya ni muhimu yatekelezwe ili kuboresha ufanisi katika Ujenzi wa bara bara nchini.

8.2.1 Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa

Pendekezo 3.2: Udhibiti wa bajeti

Ufuatiliaji uliofanywa kwenye utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa umebaini kuwa kumekuwa na mapungufu kwenye ufanisi wa udhibiti wa bajeti ambao ungeweza kusaidia kuzuia ongezeko la gharama kati ya bajeti ya mwanzo na bajeti iliyofanyiwa marekebisho kwenye miradi ya Ujenzi wa bara bara nchini. Ilipendekezwa kuwa Wakala wa Barabara nchini ihakikishe

inakuwa na bajeti ambayo inakidhi matakwa ya mradi wote na kuwa na udhibiti madhubuti wa utekelezaji wa bajeti hiyo.

Aidha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imebainisha kuwa, licha ya kuwa na ukomo kwenye bajeti kama ilivyoelezwa na Wakala wa Barabara nchini kwenye utekelezaji wao, hakujawa na hatua zozote zilizochukuliwa kuboresha udhibiti wa bajeti ili kuepuka ongezeko la gharama kama ambavyo imeonekana wakati wa kufanya ukaguzi huo. Sababu ya kushindwa kutekeleza pendekezo hili ni kuwa bajeti iliyolengwa ilikuwa haikidhi mahitaji na inabadilika mara kwa mara , na hivyo kuchangia ucheleweshaji wa malipo, kukamilisha miradi kwa ujumla na kushindwa kukidhi vigezo vya mikataba. Madhara ya hali hii ni ongezekeo la gharama kwenye miradi ya ujenzi wa barabara nchini.

Pendekezo 3.11: Utumiaji wa fomula ya mabadiliko ya bei

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imebaini kuwa fomula ya kukokotoa mabadiliko ya bei imekuwa inatumika sana[9] kwa miradi ya Wakala wa Barabara nchini na imesababisha ongezeko kubwa la gharama kutokana na kubadilika kwa thamani yafedha. Ofisi ya Taifa ilipendekeza kuwa Wakala wa Barabara nchini inapaswa kupunguza muda wa kutumia fomula ya mabadiliko ya bei kwa kuigawa miradi ya barabara katika mafungu madogo madogo yatakayowezesha mradi kukamilika ndani ya muda mfupi.

Aidha, kwa mujibu wa Wakala wa Barabara nchini, pendekezo hili halijatekelezwa kwa kuwa lina madhara kwenye utekelezaji wa miradi yao. Wakati huo huo, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi bado inachukulia pendekezo hili kuwa ni muhimu sana na linahitaji kutekelezwa. Madhara ya kutokutekeleza pendekezo hili ni kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na kutumika kwa fomula ya mabadiliko ya bei kwa miradi ambayo ukamilishwaji wake unazidi miezi 18.

Uchambuzi zaidi ulifanyika wa mapendekezo yaliyotolewa kwa kila kundi kama unavyoonyeshwa kwenye Jedwali 8.1

[9]Miradi yote iliyochaguliwa inazidi kipindi cha miezi 18 na huhitaji kutumia fomula ya mabadiliko ya bei.

Jedwali 8.1: Idadi ya mapendekezo yasiyotekelezwa kwa kila kundi

Makundi ya Mapendekezo	Jumla ya Idadi ya Mapendekezo yaliyotolewa kwa makundi	Idadi ya mapendekezo yasiyotekelezwa
Uandaaji wa mipango	1	0
Udhibiti wa ubora	5	0
Upangajiwa bajeti	1	1
Ujengaji wa uawezo	2	0
Ufuatiliaji na tathmini	1	0
Uwazi	1	0
Utumiaji wa rasilimali	1	1
Uratibu	1	0
Manunuzi na usimamizi wa mikataba	3	0
Usimamiaji wa Ufanisi	2	0
Mgawanyo wa majukumu	1	0
Utunzaji wa taarifa	1	0

Uchambuzi uliofanyika kwenye Jedwali la 8.1 unaonesha kuwa mapendekezo kuhusiana na udhibiti wa bajeti na utumiaji wa rasilimali nyingine za ujenzi wa barabara nchini hazikutekelezwa wakati mapendekezo mengine yametekelezwa kwa kiasi au kikamilifu.

Hii inamaanisha kuwa suala la kutenga bajeti na utumiaji wa rasilimali zilizopo kwenye ujenzi wa barabara nchini bado linahitaji maboresho.

Mapendekezo ambayo Yametekelezwa kwa Kiasi

Pendekezo 3.3: Kuainisha wajibu na majukumu husika kwa wadau wanaotekeleza miradi ya Ujenzi wa barabara.

Wakati wa kufanya ukaguzi ilibainika kuwa majukumu na wajibu wa wadau wanaotekeleza miradi ya ujenzi wa barabara hayajaainishwa ipasavyo na kulikuwa na umuhimu wa kuchukua hatua ili kuainisha majukumu yao na kusimamia vihatarishi mbalimbali. Ilipendekezwa kuwa Wakala wa Barabara nchini wanapaswa kuainisha wajibu na majukumu kwa kila upande unaohusika kwenye utekelezaji wa miradi ya barabara. Wakala wa Barabara nchini imeweza kutenganisha majukumu na kuainisha wajibu na majukumu kwa kila upande unaohusishwa kwenye mradi wa ujenzi wa barabara kwa kuzingatia muda, gharama na ubora. Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara nchini haijafanya kazi ya uhamasishaji wa kuainisha na kusimamia vihatarishi mbalimbali vinavyoweza kuzuia kutimiza lengo la kukamilisha kazi zenyewe.

Madhara ya kushindwa kuainisha na kusimamia vihatarishi kwenye utekelezaji wa miradi ni kuchelewa kwa ukamilishaji wa miradi na mabadiliko kwenye gharama ya miradi. Aidha, Wakala wa Barabara nchini kwa sasa imeanza kuboresha uainishaji wa viatarishi baada ya kuanzisha uandikishaji wa viatarishi vya usimamizi, ambao kwa sasa bado upo kwenye mchakato wa awali.

Pendekezo 3.4: Kuanzisha uandikishaji wa mapendekezo

Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa, taarifa zinazohusiana na wakandarasi na washauri elekezi wanaofanya na wasiofanya kazi vizuri kwa kila mradi wa ujenzi wa barabara hazikuwa zinahifadhiwa. Ilipendekezwa kuwa Wakala wa Barabara nchini kuanzisha utumiaji wa kumbukumbu za wakandarasi na washauri elekezi na kuweka mapendekezo ili kuweza kusaidia ufuatiliaji na tathmini ya ufanisi wao kabla ya kuwapatia mikataba ya miradi mipya.

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa pendekezo hili umebaini kuwa, Wakala wa Barabara nchini haijaweka mfumo wowote wa kumbukumbu ambao utaonyesha athari za kutoa mikataba kwa mkandarasi au mshauri elekezi ambae hafanyi kazi vizuri, kitu ambacho kitaisababishia Serikali kuingia gharama kubwa.

Kwa upande mwingine Wakala wa Barabara nchini kwa sasa inapeleka taarifa za ufanisi/utekelezaji wa wakandarasi/washauri kwenye bodi ya usimamizi wa wakandarasi (CRB), Bodi ya usimamizi wa waandisi (ERB) na kwa sasa inafanya mchakato ambao utapendekeza njia sahihi ya kuhifadhi taarifa hizo.

Pendekezo 3.5: Kuboresha Uhifadhi wa Kumbukumbu

Ukaguzi umebaini kuwa utunzaji na kumbukumbu mbali mbali katika Ofisi ya Wakala wa Barabara nchini sio mzuri kiasi cha kuathiri ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi wa barabara. Ilipendekezwa kuwa Wakala wa Barabara nchini anapaswa kuboresha utunzaji wake wa kumbukumbu. Wakati wa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa pendekezo hili ilibainika kuwa Wakala wa Barabara nchini hajaweza kuanzisha sehemu ya utunzaji wa kumbukumbu za miradi yake ya barabara.

Kadhalika , ilibainika kuwa Wakala wa Barabara nchini ameweza tu kuanzisha mchakato wa uandaaji kuwa na mfumo mzuri wa utunzaji

wa kumbukumbu ambao utasaidia kutatua tatizo la utunzaji wa kumbu kumbu za miradi ya ujenzi wa barabara.

Pendekezo 3.6: Manunuzi kwa kuzingatia gharama

Ilibainika kuwa kulikuwa na ongezeko la gharama kwa miradi iliyokamilika na sababu kubwa ilikuwa ni tofauti kubwa ya kadirio la awali la ujenzi wa barabara na gharama halisi. Ilipendekezwa kuwa Wakala wa Barabara nchini ihakikishe inachukua wakandarasi kulingana na gharama halisi za miradi zilizokokotolewa kwa umakini.

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa pendekezo hili ilibaini kuwa Wakala wa Barabara nchini amefanya marekebisho ya mikataba ili kupunguza athari zitokanazo na wakandarasi ambao hawafanyi kazi kwa kiwango. Aidha haijaweza kuonyesha kuwa inafanya uteuzi wa wakandarasi kulingana na mahesabu ya gharama halisi za miradi. Athari za kuteua wakandarasi kwa vigezo vya makadirio ya mradi ambayo hayajumuishi mambo yote muhimu ya mradi ni kuwa na tofauti kubwa baina ya gharama za awali na gharama halisi mwishoni mwa mradi ambayo mara nyingi inakuwa kubwa sana.

Pendekezo 3.9: Kupunguza Ongezeko la Gharama (Uratibu)

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara ambayo ilitokana na ucheleweshaji wa kuhamisha miundombinu mbalimbali kama vile ya simu, umeme, maji, n.k ambayo hufanywa na makampuni husika katika kipindi cha Ujenzi. Ilipendekezwa kuwa Wakala wa Barabara nchini anapaswa kuchukua hatua za tahadhari ili kupunguza muda na ongezeko la gharama kwa kuongeza uratibu na makampuni hayo ya simu, umeme, maji n.k.

Katika kutekeleza pendekezo hili, Wakala wa Barabara nchini imeandaa mwongozo wa usimamizi wa hifadhi za barabara; lakini haijaweza kushirikiana na makampuni ya huduma za maji, umeme na simu ili kuweza kutatua tatizo la uchelewaji wa miradi ya barabara na ongezeko la gharama linalotokana na kushindwa kuhamishika kwa miundo mbinu.

Athari za kukosekana kwa uratibu na kushindwa kuhamishika kwa miundombinu imepelekea kuongezeka kwa gharama na muda wa kumaliza mradi.

Mapendekezo Yaliyotekelezwa Kikamilifu

Ukaguzi umebaini kuwa mapendekezo 13 katika utendaji yametekelezwa kikamilifu na kuboresha zaidi ufanisi wa Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara nchini kwenye usimamizi wa miradi ya ujenzi wa bara bara.Hali hii itaongeza ufanisi katika utumiaji wa rasilimali kwenye miradi ya ujenzi wa barabara nchini.

Mapendekezo 13 ambayo yametekelezwa kikamilifu yalikuwa yanahusu mambo yafuatayo:

a) Kuunda tume kwa ajili ya kupitia uwezekano wa kuimarisha uadilifu, taaluma na ufanisi wa mipango mikakati ya Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara nchini ili kuweza kutathmini kiwango cha uwazi na uwajibikaji.

b) Kuipatia Wakala wa Barabara nchini maelekezo kamili ya kuweza kusimamia Washauri elekekezi wa miradi ya Ujenzi wa barabara nchini,

c) Kufanya tathmini kwa kushitukia kuhusiana na ufanisi wa usanifu wa kazi za Wakala wa Barabara nchini, namna anavyofanya manunuzi, kutoa maelekezo na kusimamia washauri elekezi wa miradi ya ujenzi wa barabara nchini.

d) Kuipatia tume (Kama ilivyo hapo juu) maelekezo ya kutathmini namna nzuri ya kutimiza wajibu wa shughuli zinazohusiana na kazi za usanifu;

e) Kwa kuzingatia kazi ya tume iliyopendekezwa, serikali inapaswa kuipatia Wakala wa Barabara nchini maelekezo sahihi ya namna ya kuboresha kazi za usanifu na kuzifanyia mapitio kazi hizo.

f) Uhitaji wa Wizara ya ujenzi na Wakala wa Barabara nchini kuboresha huduma za shughuli za awali kama vile kutimiza masharti ya mikopo na hatua za manunuzi;

g) Mikataba kujumuisha kifungu cha adhabu kitakachotumika kwa wakandarasi ambao hawatakamilisha miradi yaokwa muda waliopewa wa kazi, bajeti na ubora wa bara bara;

h) Umuhimu wa Wakala wa Barabara nchini kubainisha bayana masharti yaliyopo kwenye mikataba kwa ajili ya kulipia kodi kwa wakandarasi.

i) **Masuala ya udhibiti wa ubora wakati wa kufanya usimamizi, ufuatiliaji, uchunguzi na tathmini yanapaswa kuchunguza matatizo ya ucheleweshaji, ongezeko la ubora wa kazi iliyofanyika.**

j) **Tathmini za miradi ya bara bara iliyokamilika inapaswa kutumika kupima na kuchambua mafanikio yaliyopatikana;**

k) **Uzoefu uliopatikana kutokana na utendaji wa miradi hii unapaswa kutumika kwenye kuandaa mipango mizuri, mafunzo na uboreshaji wa miradi inayoendelea au inayokuja**

l) **Wakala wa Barabara nchini anapaswa kuboresha uwazi wake kwa jamii na kuto taarifa mbalimbali za utekelezaji wa miradi yake. Na;**

m) **Michoro ya ujenzi wa barabara zilizokamilika inapaswa kuhifadhiwa na kutumika punde tu uhitaji wa kufanyika kwa matengenezokwa barabara husika yanajitokeza.**

8.3 Hitimisho na Matarajio

a) **Kulingana na uchambuzi uliofanyika wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa inahitimishwa kuwa Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara nchini wamejitahidi katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itaendelea kufanya ufuatiliaji wa mapendekezo ambayo hayajatekelezwa kabisa na yale yaliyotekelezwa kwa kiasi tu ili kuziwezesha taasisi hizo kuboresha utendaji wao katika usimamizi wa Miradi ya barabara nchini.**

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho cha kwanza: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Kuzuia na Kukabiliana na Mafuriko

S/N	Aina ya Mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Hali ya utekelezaji	Maoni ya NAOT
		Mapendekezo kwenda kwa *Mji wa Babati pamoja na Wilaya ya Babati*		
		Pendekezo 1: Vikinga Majani		
1.	**Ufuatiliaji**	**Pendekezo 1:** Halmashauri Babati inapaswa kufuatilia na kudhibiti ukuaji wa vikinga majani ili kuepuka kuzuia mtiririko wa maji katika matokeo ya maji ya Kigongoni. Aidha, ipige marufuku ufugaji wa ng'ombe katika eneo lililoko karibu na Ziwa Babati.	• Halmashauri ya Mji wa Babati imejiwekea mikakati ya usafi katika mtiririko wa Kigongoni kwa kufyeka nyasi hadi kiwango cha udongo kuruhusu maji kupita kwa urahisi • Halmashauri ya Mji wa Babati imeunda kamati ya mazingira katika ngazi ya kata ambayo inaendesha doria ili kuzuia ulishaji wa mifugo katika eneo linalozunguka Ziwa Babati • Baraza la Halmashauri ya Mji wa Babati linahamasisha wanajamii kuunda vikundi vya uzalishaji na kuwapa mafunzo ili kuboresha ufugaji na kupunguza idadi kubwa ya Mifugo. • Baraza linaendelea na ufuatiliaji na kudhibiti ukuaji wa nyasi, hivyo maji ya ziada yanatiririka kwa urahisi katika mtiririko wa Kigogoni.	***Limetekelezwa kikamilifu.***
		Pendekezo 2: Tuta ardhi na maporomoko bandia ya maji		
2.	**Maendeleo**	Pendekezo 2.1: Kuanzisha mfereji wenye kingo imara kutoka kwenye kingo ya asili ya zamani kuelekea kwenye korongo kubwa jipya na kujenga maporomoko mapya ya maji	• Baraza la Halmashauri limejenga mfereji na kingo za mito (Gabions) kubwa pamoja na tuta ili kuzuia kasi ya mtiririko wa maji na kuzuia	***Limetekelezwa kikamilifu.*** Mfereji na kingo za mto zimejengwa ili

S/N	Aina ya Mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Hali ya utekelezaji	Maoni ya NAOT
		mwanzoni mwa korongo ili kuzuia kupanuka zaidi kwa korongo pamoja na miundo mbinu ili kuzuia matope katika bonde.	kupanuka zaidi kwa bonde. • Jamii katika kata ya Nangara kuhamasishwa na kupewa mafunzo ya kujenga matuta kwenye mashamba yao ili kupatikana mwinuko na kupunguza kasi ya maji yanayoelekea kwenda kwenye kingo za korongo. .	kuzuia mtiririko wa maji kwa kasi kubwa.
3.	Utoaji maamuzi	*Pendekezo 2.2:* Kutangaza eneo kutokea tuta la Kigongoni hadi mwisho wa makorongo na maporomoko ya maji kuwa hakutoruhusiwa kufanya shughuli za kilimo, malisho ya mifugo, utengenezaji wa matofali nk na kupanda idadi kubwa ya miti na aina nyingine ya uoto ili kuzuia mmomonyoko wa udongo.	Baraza limeandaa tayari mpango wa mpito wa matumizi ya ardhi. Mpango huo unaoanisha eneo la maporomoko kama eneo la bwawa ambalo limezuiliwa kufanya shughuli za kilimo, ufugaji na ujenzi kwa kutengeneza matofali. nk. Matangazo katika Mabango kuhusu shughuli zisizo ruhusiwa yameshawekwa, na Halmashauri inaendelea kufanya ufutailiaji ili kutekelezwa.	*Limetekelezwa kwa kiasi.* Miti bado haijapandwa.
		Pendekezo 3:Maeneo ya Makazi ya watu na Biashara katika mji wa Babati		
4.	Mipango	*Pendekezo 3.1:* Maafisa wa mipango miji wa Halmashauri ya Mji wa Babati wanapaswa kuzingatia hatari ya mafuriko wakati wa kugawa ardhi. Aidha, jitihada zinapaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba miundo mbinu ya kuzuia /hatua inawekwa katika maeneo hatarishi ambayo yametengwa kwa malengo ya makazi na biashara.	Michoro ya mipango ya mji wa babati imeshaandaliwa kwa kuzingatia kukabili mafuriko katika eneo hilo. Mpango wa muda mfupi wa matumizi ya ardhi umetekelezwa kwa ufanisi katika maeneo yote	*Limetekelezwa kwa ukamilifu.* Kwa Sasa michoro ya upangaji wa mji wa Babati imezingatia hali ya mafuriko katika mji.

S/N	Aina ya Mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Hali ya utekelezaji	Maoni ya NAOT
5.	**Mipango**	***Pendekezo 3.2:*** Kuwepo na mpango kabambe wa mji wa Babati ili kuweza kutumika wakati wa kugawa maeneo kwa ajili ya makazi na biashara.	Mpango wa matumizi ya ardhi wa muda mfupiwa halmashauri lazima upitiwe upya na maeneo yenye hatari ya mafuriko yaweze kuainishwa.	*Halijatekelezwa.* Mapitio ya ILUP ya 2006-2016 hayajafanyika, ingawaje yameingizwa kwenye bajeti ya mwaka 2014/15
		Pendekezo 4: Mipango ya kuzuia maafa na fedha kwa ajili ya usimamizi wa mafuriko		
6.	**Bajeti**	***Pendekezo 4.1:*** Mamlaka za Miji na Mikoa zihakikishe zinaweka mpango wa maafa na mafuriko katika mipango yao ya kila mwaka	Baraza tayari limeomba kiasi cha Tsh.1, 200,000,000 / = ili kuweza kupambana na maafa.	*Halijatekelezwa.* Haipo katika mpango wa matumizi wa muda mfupi (MTEF)i.
7.	**Ushiriki wa jamii**	***Pendekezo 4.2:*** Mamlaka ya Mikoa na Wilaya inapaswa kuhakikisha kuwa asasi za kiraia na maafisa husika muhimu katika ngazi husika wanatimiza majukumu yao katika kuandaa programu za kukabiliana na mafuriko.	Baraza la Mji wa Babati limekuwa likifanya mikutano ya uhamasishaji na wadau wa mazingira na watu wanaoishi pembezoni mwa Ziwa Babati. Malisho ya Wanyama pamoja na kilimo na utengenezaji wa matofali umepigwa marufuku katika eneo la ziwa Babati na kumekuwa na usimamizi mkubwa. Udhibiti wa mazingira umefanywa kama agenda katika mikutano ya Mitaa na vijiji.	*Limetekelezwa kwa kiasi.* Hakuna ushahidi kuonyesha kwamba Maafisa wanaoshughulikia ngazi ya wilaya, kata, mtaa na kijiji wanatekeleza majukumu yao katika programu ya kukabiliana na mafuriko.
		Mapendekezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara		
		Pendekezo 4:Mipango ya fedha kwa ajili ya maandalizi ya usimamizi wa mafuriko		
8.	**Bajeti**	***Pendekezo 4.1:*** Mamlaka za Mikoa pamoja na Wilaya zinapaswa kuweka bajeti ya mafuriko katika bajeti zao za mwaka.	MTEF ya mwaka 2014 - 2016/17 ukurasa 56 umeingiza shughuli C01S08 kwa ajili ya kuratibu usimamizi na maandalizi ya majanga kufikia mwezi Juni, 2015	*Limetekelezwa kikamilifu*

S/N	Aina ya Mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Hali ya utekelezaji	Maoni ya NAOT
9.	Ushiriki wa jamii	***Pendekezo 4.2: :*** Mamlaka ya Mikoa na Wilaya inapaswa kuhakikisha kuwa asasi za kiraia na maafisa husika muhimu katika ngazi husika kutimiza majukumu yao katika kuandaa mipango ya mafuriko.	Mkuu wa Mkoa amekuwa akifanya mikutano ya uhamasishaji kwa wadau wa mazingira na watu wanaoishi pembezoni mwa Ziwa Babati wakati wa ufuatiliaji wake kwa kila robo mwaka. Kumekuwa hakuna mafuriko katika Mji wa Babati baada ya kutekeleza mipango ya kukabiliana na mafuriko ikiwa ni pamoja na upandaji wa miti, ujenzi wa miradi ya barabara kuu mwaka 2013, ujenzi wa kuta na mifereji katika maeneo yaliyoathirika. Pesa zilizotengwa katika mfuko huu zimekuwa zinatumika kwa ajili ya majanga mengine na kutatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji katika eneo la Kiteto, Mnada, Hanang, na Mbulu.	*Limetekelezwa kwa kiasi* Hakuna ushahidi ulioonyeshwa kuwa maofisa husika wa wilaya, kata, mtaa na kijiji wanatimiza majukumu yao ya kukabiliana na mafuriko.
10.	Mipango	***Pendekezo 4.3*** Sekretarieti ya Mkoa waManyara ihakikishe inaipa kipaumbele masuala ambayo yanahusiana na mafuriko na kuyaingiza katika mipango yao ya mwaka na bajeti.	MTEF ya mwaka 2014 - 2016/17 ukurasa 56 imeingiza shughuli C01S08 kwa ajili ya kuratibu usimamizi wa majanga na maandalizi kwa Juni, 2015. Kumekuwa hakuna mafuriko katika mji wa Babati baada ya kutekeleza mipango ya kupambana na mafuriko ikiwa ni pamoja na upandaji wa miti, ujenzi wa miradi ya barabara kuu mwaka 2013, ujenzi wa kuta na mifereji imejengwa katika maeneo yaliyoathirika .	*Imetekelezwa kikamilifu*
		Mapendekezo kwenda Wakala wa Barabara		
		Recommendation 5: Kuhusu kingo za Kigongoni		

S/N	Aina ya Mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Hali ya utekelezaji	Maoni ya NAOT
11.	**Maendeleo (Ujenzi)**	***Pendekezo 5.1:*** Kwa Wakala wa Barabara Manyara Ili Kupunguza hatari ya mafuriko kwa mji wa Babati, Wakala wa Barabara Manyara lazima iweke mipango ya muda mfupi ya kubadili Makaravati madogo na kuweka makubwa katika kingo za Kigongoni	Wakati wa uandaaji wa mradi wa barabara ya Singida-Babati-Minjingu, Wakala wa Barabara waliweza kumuelekeza Mzabuni mshauri, M / s Carl Bro wa Dernmark aweze kuzingatia tatizo la mafuriko la mji wa Babati ambalo limekuwa likisababishwa na kufurika kwa maji kutoka katika Ziwa Babati	*Limetekelezwa kikamilifu* Karavati lenye umbo la Boxi limewekwa katika kingo za Kigongoni ili kuruhusu mtiririko wa maji.
12.	**Mipango**	Pendekezo 5.2: Kwa Wakala wa Barabara -Makao Makuu TANROADS inapaswa kuhakikisha kuwa ubunifu wa miradi ya ujenzi wa barabara inayoendelea inazingatia uwezo wa karavati kupitisha maji katika kingo za Kigongoni ili kuwezesha mtiririko mzuri wa maji katika mji wa Babati.	Kipande cha Km 1.4 cha barabara ya Babati kuelekea Dodomakilijumuishwa kwenye mradi huu katika Fungu Namba 3 kwa nia ya kutatua tatizo la mafuriko katika Ziwa Babati . Miundo mbinu mikubwa iliyojengwa ili kukabiliana na mafuriko inajumuisha makaravati yenye vipande vinne katika eneo la Kigongoni ambalo linasaidia kutiririsha maji yaziwa Babati wakati wa mafuriko. Pia makaravati ya pande nne yenye kipimo cha 0+ 300 kuelekea Dodoma ambayo yanachukua maji toka ziwani na kuyamwaga katika eneo la maji la wazi lililojengwa.Bara bara katika eneo la Babati imeinuliwa na kuwekewa maeneo ya wazi makubwa ili kuruhusu utiririshaji mzuri wa maji toka ziwani.	*Limetekelezwai kikamilifu* Karavati lenye seli nne katika eneo la Kigongoni limeweza kujengwa. Pia bomba lenye seli mbili limejengwa.

S/N	Aina ya Mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Hali ya utekelezaji	Maoni ya NAOT
		Pendekezo namba 6:Daraja la Kiongozi		
13.	**Mipango**	**Kwa Wakala wa Barabara - Manyara** ***Pendekezo 6.1:*** Wakala wa Barabara - Manyara wanapaswa kuhakikisha kuwa kazi ya ukarabati wa barabara kwa ajili ya kukabiliana na mafuriko inafanywa mapema ili kuzuia barabara kufungwa na kuzuia uharibifu unaoweza kutokea kutokana na mafuriko kwa sikuzijazo.	Wakati wa uboreshaji wa barabara ya Singida-Babati-Minjingu, TANROADS ilitoa taarifa kwa mzabuni Mshauri, M / s Carl Bro ya Denmark, kuzingatia tatizo la mafuriko kwa mji wa Babati ambayo yamekuwa yakisababishwa hasa na kufurika kwa Ziwa Babati.	***Limetekelezwa kwa ukamilifu***
12.	**Kufuata Sheria**	***Pnednekezo la 1:*** **Viwango kwa ajili ya usimamizi wa taka ngumu.** Taasisi ya viwango nchini inapaswa kwa mujibu wa sheria[10], kuweka viwango vya	TBS wakisirikiana na VPO na wadau wengine wameandaa viwango vya usimamizi wa mazingira (viwango vya ubora wa hewa) kanuni ya mwaka	*Halijatekelezwa* Hakuna viwango kwa jaili ya usimamizi wa taka ngumu ambavyo vimewekwa na TBS.

[10] Environmental Management Act No. 20 of 2004 and TBS Act of 1975

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
		usimamizi wa taka ngumu ambavyo vinapaswa kufuata na halmashauri zote wanapotimiza majukumu yao ili kuhakikisha kunakuwa na usawa kwenye huduma zitolewazo.	2007za Usimamizi wa mazingira (viwango vya ubora wa udongo) kanuni ya mwaka 2007 Kanuni hizi zimeweza kutambua wajibu wa wadau katika kazi ya usimamizi wa viwango vya mazingra. Kanuni hizi tayari zimekwisha kusambazwa katika maduka ya vitabu vya serikali katika mikoa yote ya Tanzania Bara.	
		Mapendekezo kwa Wizara ya afya, ofisi ya makamu wa raisi kitengo cha mazingira na NEMC		
13.	**Mfumo wa Sera**	***Pendekezo namba 1:*** **Sera na kanuni za taka ngumu** Wizara ya afya , Ofisi ya Makamu wa rais na NEMC wanapaswa kuandaa sera na kanuni ili ziweze kutumika kwenye mifumo ya usimamizi wa taka ngumu.	**Wizara Ya Afya** Nakala 1000 za sera ya taka ngumu zimechapwa mwaka 2012, Nakala 110 zimekwisha kusambazwa katika Mikoa 21 na Miji 4 ya (Mwanza, Mbeya, Tanga na Dar es Salaam). Pia Nakala 690 zimeweza kusambazwa kwa halmashauri 168 ndani ya mwezi Januari 2015. Wizara ya Afya imeweza kuanzisha kanuni za kusimamia mabaki ya a binadamu katika hatua za utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Jamii. Rasimu za kanuni hizi zimeshapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuidhinishwa Maafisa Afya 4 wa Miji, Maafisa Afya 16 wa Manispaa na wafanyakazi 4	*Limetekelezwa kwa kiasi* Sera zimeweza kuandaliwa na kusambazwa katika mikoa yote, lakni kanuni zinazohusu usimamizi wa mabaki ya binadamu bado zinaendelea kungojea idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
			toka Wizara ya Afya walipewa mafunzo juu ya taka ngumu mwezi wa Juni 2011 katika mkoa wa Tanga. Mafunzo yalitolewa na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi na Muhimbili. Pia mafunzo haya yalifanyika mwaka 2014 kwa Makatibu Tawala wa Mkoa 21 na Wakurugenzi 4 kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Katika kipindi cha 2012/2013 – ukaguzi ulifanyika kwa Miji 4 kuhusiana na usimamazi wa taka ngumu katika miji mikubwa ya Mbeya; Tanga, Arusha na Mwanza Kwa mwaka 2013/2014 uboreshaji wa usimamizi wa taka ngumu umefanywa katika Halmashauri 6 ambazo ni Manispaa ya Ilemela, Shinyanga; Songea, Iringa; Dodoma na Singida. Mashindano ya usafi yamemekuwa yakifanywa kila mwaka tangu mwaka 2011 na yamekuwa yakishirikisha tathmini ya usafi na hali ya Miji, Manispaa Halmashauri na Jiji	
			Ofisi ya makamu wa Raisi Kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 kiasi cha fedha kiliweza kuingizwa kwenye bajeti ya mwaka, lakini hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha	***Limetekelezwa kwa kiasi*** Mapitio ya sera ya taifa ya mazingira ya mwaka 1997 yapo

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
			wa 2012 fedha hizo hazikuletwa kutoka hazina. Shughuli hii ilisogezwa kwenda mwaka mwingine wa fedha 2012/13. Kwa mwaka huo wa 2013 Ofisi imeweza kutengeneza Hadidu rejea kwa mtoa ushauri ambaye anapitia na kutoa ushauri kuhusu mfumo wa sera za taka ngumu. Kwa sasa rasimu ya ripoti inajadiliwa na wadau mbalimbali na itarudishwa kwa mtaalamu mshauri ili aweze kuikamilisha. Inategemewa itakamilika mwaka 2015. Kanuni za (usimamizi wa taka na madhara) zilianzishwa mwaka 2009. Kanuni hizi zinatumika katika uendeshaji na zinapatikana katika maduka yote ya vitabu ya serikali katika mikoa yote Tanzania.Pia mwaka 2009/10 na 2010/2011 baadhi ya nakala ziliweza kusambazwa kwa washiriki waliohudhuria warsha ya uelewa wa mbinu za usimamizi wa kisasa wa taka ngumu. Mafunzo ya kujenga uwezo wa wadau kuhusiana na taka hatarishi na uchafuzi wa bahari (MARPOL) yalifanyika katika mji wa Dar es Salaam na Tanga mwezi Julai na Novemba 2012.	katika hatua za mwisho. Kanuni zipo tayari,mikutano ya kujenga uwezo jamii imefanyika toka mwaka 2009/10, 2010/11 na 2011/12/.

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
		Mapendekezo kwenda kwa Serikali za Mitaa		
14.	**Mipango**	***Pendekezo la 1*** **Mkadirio ya kiwango kinachozalishwa cha taka ngumu** Kitengo cha usimamaizi wa shughuli za taka ngumu kwenye halmashauri kilipaswa kuandaa mfumo wa taarifa wa usimamizi wa taka ngumu ambao utategemewa na halmashauri kukadiria kiwango cha taka ngumu kinachozalishwa na kukusanywa kwa mwaka	Serikali za mitaa zinafanya tathmini ya uhitaji ili kuanzisha mfumo wa pamoja wa usimamizi wa taka ngumu TAMISEMI imeanzisha mfumo wa GIS ambao umeunganishwa kwenye Halmashauri za miji na manispaa 26 zilizopo kwenye utekelezaji wa miradi ya ULGSP na TSCP.	*Halikutekelezwa* TAMISEMI imefanya tathmini kwa kuanzisha mfumo wa pamoja wa usimamizi wa taka ngumu tu, na jitihada kuanzisha mfumo wa kijiografia umefanyika ambapo umeweza kuunganishwa kwa halmashuri 26 tu kati ya 168 zilizopo. Hakuna ufafanuzi zaidi wa namna zitakavyokuwa zinatumika kusaidia kukairia kiwango cha taka ngumu kinachozalishwa na kukusanywa.

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
15.	**Usimamizi wa kiutendaji**	***Pendekezo la 2*** **Kuweka viwango wazi vya mahitaji ya utendaji na malengo ya ukusanyaji taka ngumu** Kitengo cha usimamizi wa taka ngumu kwenye halmashauri kinapaswa kuandaa viwango vinavyohitajika kwa wakandarasi. Kitengo hiki kinapaswa kuhakikisha lengo la taka ngumu zinazopaswa kukusanywa kwa kila kata linaandaliwa na mkandarasi anatakiwa kufuata vigezo hivyo	Serikali za Mitaa zina viwango vya juu vya ukusanyaji wa taka, pia katika kila kata mkandarasi amewekewa kiwango cha juu cha ukusanyaji wa taka kulingana na malengo yaliyowekwa.	*Limetekelezwa kwa kiasi* Si Halmashauri zote zilizoweka viwango vya ukusanyaji wa taka ngumu hii ni kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo uwezo wa kitaaluma wa wafanyakazi na upungufu wa rasilimali.
16.	**Usiamizi wa utendaji kazi**	***Pendekezo la 3*** **Tofauti za kiutendaji miongoni mwa Makandarasi.** Kitengo cha Taka ngumu kilichopo kwenye halmashauri kinapaswa kukusanya taarifa za kutosha kutoka kwa wakandarasi ili kuweza kugundua sababu zinazopelekea tofauti za kiutendaji kati ya mkandarasi mmoja na mwingine kwa wingi, ubora na faida zinazopatikana kutokana na taka ngumu .	Halmashauri zimeweza kutunza tarifa za wakandarasi wao na wameendelea kuwafuatilia mara kwa mara ili kujua mafanikio yao na madhahaifu yao katika kazi .Wakandarasi ambao hawafanyi vizuri hutolewa baada ya kumaliza muda wao wa wa mkataba wa kufanya kazi .	*Limetekelezwa kikamilifu* Kuna muongozo wa ufuatiliaji na tathmini katika halmashauri, pia mikataba inayotolewa kwa wakandarasi inaweka vigezo vya ufanisi.

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
17.	**Usimamizi wa utendaji**	***Pendekezo la 4*** **Upimaji na Tathmini wa utendaji wa watoa huduma** Serikali za Mitaa wanapaswa kuunda timu ya kufanya tathmini ya uwezo wa watoa huduma na vikwazo wanavyokumbana navyo katika Kufikia ngazi inayokubalika ya utendaji. Timu hii inapaswa kukusanya maoni ya wadau kuhusu ubora wa huduma zinazotolewa na watoa huduma wa taka ngumu.	Halmashauri zina timu za kufanya tathmini shughuli za taka ngumu (kwa kipindi cha kila robo mwaka) ikijumuisha halmashauri zinazofanyia tathmini huduma zinazotolewa na kuwajulisha watoa maamuzi. Hatua hii imeimarisha kiwango cha ufanisi.	*Limetekelezwa kikamilifu* Tathmini zinafanywa katika kila robo mwaka
18.	**Usimamizi wa kiutendaji**	***Pendekezo la 5*** **Kuboresha mfumo kwa ajili ya ufuatiliaji wa Utendaji** Idara ya usimamizi wa taka ngumu ya halmashauri inapaswa kuboresha aina, kiasi na awamu za taarifa inayohitaji ili kuweza kufuatilia ufanisi wa watoa huduma wake. Katika kutekeleza hili, idara ya usimamizi wa taka ngumu inatakiwa kuweka uwasa katika uhitaji wake wa taarifa ikilinganisha na ukubwa uliowapa watoa huduma kutoa taarifa hizo.	Halmashauri zimefanyia marekebisho taarifa zao kuhusu usimamizi wa taka ngumu ili kuweza kufikia vigezo.	*Limetekelezwa kwa kiasi* Licha ya kuwa mipango mikakati ya halmashauri imekuwa ikifanyiwa maboresho ya mara kwa mara , bado halmashauri hazijaweza kufanyia maboresho taarifa zinazohusiana na kiasi, kiwango na idadi za taka ngumu ambazo ni muhimu kwenye usimamizi wa taka ngumu. Pia halmashauri haijaweza

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
		Pindi uhitaji wa taarifa utakapokuwa umebainishwa katika kitengo. Kitengo hicho kinapaswa kuhakikisha kuwa watoa huduma wanatoa huduma kwa mujibu wa makubaliano.		kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinapelekwa kwenye halmashauri na wakandarasi.
19.	**Utoaji wa taarifa**	***Pendekezo la 6*** **Hatua muafaka zinazoweza kusaidia kuboresha ongezeko la utoaji wa huduma kwa ufanisi.** Idara ya usimamizi wa taka ngumu katika halmashauri inapaswa kuendelea kuandaa na kuanzisha uwezo wa kusimamia shughuli zao miongoni mwao wenyewe. Hapa kitengo kinatakiwa kuchuka hatua sahihi na kunukuu maamuzi yanayofanywa ili kuweza kuimarisha na kuboresha ufanisi wa utoaji wa huduma.	Chini ya pogramu ya TSCP na ULGSP . Halmashauri zimeweza kugundua mapungufu na uwezo uliopo katika kusimamia taka ngumu. Mapungufu hayo yanafanyikwa kazi kwa kutoa mafunzo na kuwapatia nyenzo za kufanyia kazi. Pamoja na mwelekeo juu ya miongozo na maadili ya watumishi wa umma. Hili linatekelezwa katika Halmashauri 18 zilizo chini ya ULGSP ambazo zinazingatia mafunzo, vifaa na miundombinu endelevu.	***Limetekelezwa kwa kiasi*** Mafunzo ya kujengewa uwezo yamefanyika kwa lengo la kuboresha utendaji katika utoaji huduma kwa ufanisi . Hata hivyo ufikiwaji wa halmashauri zote ni tatizo kwani , halmashauri 142 za Mitaa hazikuweza kujumuishwa katika mpango huu. Zadi ya hapo shughuli ambazo zinafadhiliwa chini ya miradi hii miwili ya TSCP na ULGSP haikuwa endelevu kwa sababu programu hizi zimepewa muda maalumu wa uendeshaji.

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
20.	**Kusimamia mapato**	***Pendekezo la 7*** **Mfumo kwa ajili ya ada za taka ngumu** Halmashauri zinatakiwa kuanzisha mfumo wa ada za usimamizi wa taka ngumu ambao utajumuisha gharama zote za uendeshaji wa shughuli za taka ngumu. Hili litawezeshwa kwa kufanya mchanganuo wa bajeti zake na gharama za usimamizi wa shughuli hizo, na baadae kuainisha vyanzo vyote vya mapato ili waweze kukadiria mapato kamili ya makusanyo yanayopatikana. Pia halmashauri zinatakiwa kufanya utafiti kuhusiana na utayari wa wananchi kulipia gharama za uzoaji wa taka ngumu	Halmashauri zimeweza kufanya utafiti kuhusu utayari wa kulipa tozo za taka ngumu, pamoja an mafunzo kwa ajili ya huduma za taka ngumu katika maeneo yao ya mamlaka.	*Limetekelezwa kwa kiasi* Utafifiti kuhusu utayari wa kulipa ada za taka ngumu umeshafanyika. Matokeo yametumika katika kuandaa Mpango Mkakati wa kusimamia taka ngumu, Hivi sasa Muundo wa Ada upo katika maandalizi.
21.	**Usimamizi wa mapato**	***Pendekezo la 8*** Ili kuweza kuboresha ukusanyaji wa ada za taka ngumu, Idara ya Uhasibu kwenye halmashauri inapaswa kuhakikisha kuwa wanakuwa na hesabu kamili kaya, biashara na viwanda vilivyopo kwenye kila kata, pamoja na taarifa kuhusiana na kiwasi gani kila kaya au taasisi kinapaswa kulipa kama ada za shughuli za ukusanyaji	Idara ya taka ngumu pamoja na Idara ya Uhasibu wanafanya kazi kwa pamoja ili kupata na kutumia mfumo wa taarifa kuhusu taka ngumu ili kuweza kuanzisha malengo na matarajio ya mapato kutokana na taka ngumu.	*Halijatekelezwa* Mfumo unaoweza kukamata taarifa zote za za wakazi ,kaya, biashara na viwanda kwa ajili ya kupata mapato yao haujaweza kuanziswa.

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
		wa taka ngumu na kiasi gani kilicholipwa.		
22.	**Usimamizi wa mapato**	***Pendekezo la 9*** **Kuanzishwa kwa mfumo wa na mahesabu** Halmashauri zinapaswa kuwa na na mfumo thabiti wa hesabu ambao unaweza kuwa na taarifa zote zinazohusiana na idadai ya kaya, biashara na viwanda katika kata husika ili kuweza kuwa na orodha ya vyanzo muhimu vya mapato na kuepuka upotevu wa mapato unaofanywa na watoa wakandarasi.	Ukiondoa Dar es salaam, Halmashauri zingine zote zimefanyiwa utafiti kuhusu ukusanyaji wa mapato ili kuweza kuzisaidia sekta zingine pia. Ingawa Halmashauri chache sana ambazo ziko kwenye mpango wa TSCP ndizo zimefanya utafiti huu wa vyanzo vya mapato.	*Halijatekelezwa* Mfumo unaoweza kukamata taarifa zote za wakazi ,kaya, biashara na viwanda kwa ajili ya kupata mapato yao haujaweza kuanzishwa.
23.	**Usimamizi wa mapato**	***Pendekezo la 10*** **Upembuzi kuhusu ada zisizo kusanywa** Serikali za mitaa na idara ya taka ngumu katika serikali za mitaa zinatakiwa kueleza sababu za kutokusanya ada za taka ngumu kama ilivyo ainishwa kwenye sheria ndogo za serikali za mitaa.	Serikali za mitaa, katika kufanya utafiti kuhusu utayari wa kulipa ada ya taka ngumu wameweza kupata sababu za kutolipa ada za taka ngumu . Utafiti huo uliofanywa umeweza kuanzisha sababu zinazopelekea wananchi kutolipa ada za taka ngumu.	*Limetekelezwa kikamilifu*
24.	**Usimamizi wa mapato**	***Pendekezo la 11*** **Wajibu wa kukusanya tozo za taka ngumu** Serikali za mitaa zinatakiwa	Halmashauri za Serikali za Mitaa, wataweza kufuatilia mapendekezo hayo yatakayotokana na utafiti wa	*Halijatekelezwa* Hivi karibuni mtaalamu mtoa ushauri anakusanya

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
		kuwa na wajibu wa kukusanya tozo za taka ngumu na kuwalipa wakandarasi waliofanya kazi. Wakandarasi wanapaswa kuwa na wajibu wa kukusanya taka peke yake.	namna nzuri ya ulipaji wa tozo za taka ngumu kulingana na majibu yatakayopatikana.	takwimu kuhusu wajibu wa wakandarasi kuwa na jukumu la kukusanya taka tu, na kuacha wajibu wa kukusanya tozo chini ya Halmashauri .
25.	**Utekelezaji wa sheria**	***Pendekezo la 12*** **Utekelezaji wa mikataba** Kitengo cha usimamizi wa taka ngumu wanatakiwa kuwa na mfumo wa ufuatiliaji wa kutofuata makubaliano yaliyowekwa kwenye mikataba kati yake na Wakandarasi. Idara ya usimamizi wa taka ngumu wanatakiwa wawe na nakala ya kila mkataba, ili waweze kuwa na ufahamu wa vigezo na masharti iliyomo ya kwenye Mikataba.Ikiwa mikataba ina matakwa ambayo idara inadhani hayatatekelezeka , mikataba itatakiwa kufanyiwa marekebisho .	Serikali za Mitaa zimeweza kutekeleza mapendekezo haya kulingana na mikataba wanayoingia na wakandarasi. Nakala za Mikataba yote zinapatikana katika kitengo cha taka ngumu na inasimamiwa kwa ajili ya utekelezaji.	*Limetekelezwa kikamilifu*
26.	**Usimamizi wa mapato**	***Pendekezo la 13*** **Ukusanyaji wa ada za taka ngumu** Serikali za Mitaa, Kitengo cha usimamizi wa taka ngumu, kinatakiwa kuweza kubuni mbinu mpya za ukusanyaji wa	Ukiondoa Dar es salaam, Halmashauri zingine zote zimefanyiwa utafiti kuhusu ukusanyaji wa mapato ili kuweza kuzisaidia sekta zingine pia.	*Imetekelezwa kwa kiasi* Halmashauri za Serikali za mitaa hazikuweza kuandaa mbinu mpya kwa ajili

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
		ada ya taka ngumu kwa kufanya upembuzi yakinifu wa kuweza kujua vyanzo vyote vya mapato pamoja na kutambua chanzo sahihi kwa asilimia ili kuendeshea shughuli za taka ngumu.	Ingawa Halmashauri chache sana ambazo ziko kwenye mpango wa TSCP ndizo zimefanya utafiti huu wa vyanzo vya mapato.	ya ukusanyaji wa ada za taka ngumu.
27.	**Usimamizi wa utendaji**	***Pendekezo la 14*** **Mahitaji ya utendaji kwa watoa huduma** Idara ya usimamizi wa taka ngumu inapaswa kuweka viashiria vya kutumika kutathmini wakati wa kufuatilia utekelezaji wa mikataba ya taka ngumu ya wakandarasi. Viashiria hivi vinapaswa vitajwe wazi wazi katika mkataba na kufuatiliwa kwa karibu ili kuhakikisha utoaji wa huduma ya kuridhisha. Ufuatiliaji utaruhusu kitengo cha usimamizi wa taka ngumu kusimamia vizuri uwajibikaji wakati wa utendaji usioridhisha	Idara ya usimamizi wa taka ngumu pamoja na wakandarasi wa taka ngumu wanapewa majukumu yakuweka Viashiria katika Mikataba yao.	*Imetekelezwa kwa kiasi* Mikataba kwa watoa huduma imewekewa viashiria vya utendaji ambayo inahitaji kuzingatiwa. Hakuna ushahidi wa kuonyesha kwamba viashiria vya utendaji vimekuwa vikifuatiliwa kwa karibu na kama utendaji usioridhisha umekuwa ukiadhibiwa.
28.	**Usimamizi wa utendaji**	***Pendekezo la 15*** **Ukaguzi wa watoa huduma** Idara ya usimamizi wa taka ngumu inapaswa kufanya ukaguzi na ufuatiliaji kwenye ukaguzi huo.Matokeo na mapendekezo ya ukaguzi huo yanapaswa yawekwe kwenye	Serikali za Mitaa zinatekeleza mapendekezo ambapo Ukaguzi unafanywa na ripoti zinaandaliwa na maafisa wa afya kwenye Halmashauri husika.	*Imetekelezwa kwa kiasi* Ukaguzi unafanyika lakini ripoti za ukaguzi zinazotolewa hazioneshi dalili yoyote kwamba maeneo ya hatari

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
		kumbukumbu za maandishi. Mapendekezo yanayotokana na ukaguzi yatumike kuboresha utendaji wa watoa huduma. Mpango wa ukaguzi unapaswa kuzingatia maeneo ya hatari. Marudio ya ukaguzi uliofanywa lazima kuzingatia maboresho kutokana na ukaguzi uliopita.		yanapewa kipaumbele. Hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa ukaguzi uliofanywa ulizingatia kuleta maboresho kutokana na ukaguzi uliopita.
29.	**Utekelezaji wa sheria**	***Pendekezo la 16*** **Uwekwaji mzuri wa Vikwazo vinavyosimamiwa** Vikwazo dhidi ya wakiukaji wa usimamizi wa shughuli za taka ngumu lazima kuwekwa vizuri na kusimamiwa kama ilivyoelezwa katika mikataba. Ofisi ya sheria ikishirikiana na Idara ya usimamizi wa taka ngumu wanapaswa kuweka vikwazo ambavyo ni vya kutekelezeka kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa shughuli za usimamizi wa taka ngumu. Hata hivyo vinapaswa kutekelezeka.	Serikali za Mitaa tayari zimetengeneza sheria ndogondogo ili kuwawezesha kutekeleza usimamizi wa taka ngumu katika maeneo yao. Mikataba iliyotengenezwa na Serikali za Mitaa inawezesha kusimamia utekelezaji wa usimamaizi wa taka ngumu katika maeneo yao. Mikataba iliyotengenezwa na Serikali za Mitaa inaonesha kwa uwazi hatua za kuchukuliwa kwa wakiukaji wa makubaliano.	*Imetekelezwa kikamilifu*
30.	**Usimamizi wa utendaji**	***Pendekezo la 17*** **Kuboresha taratibu za Manunuzi ya watoa huduma na Makandarasi** Kitengo cha manunuzi kinapaswa kuboresha vigezo vya ufuatiliaji na hatua za	PMUs katika Serikali za Mitaa zinafanya kazi kulingana na Sheria ya Manunuzi.	*Haikufanyiwa kazi* Msisitizo uliowekwa ni idara ya manunuzi kufanya manunuzi yake yote kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma. Hata hivyo, hakuna ushahidi

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
		manunuzi ya wakandarasi wa taka ngumu ili kuhakikisha kuwa wale wakandarasi wanaokidhi vigezo tu ndio wanapewa mkataba. Tathmini ya kina ya uwezo wa kifedha, vifaa vya mzabuni, nguvu kazi na rasilimali nyingine inapaswa ifanyiwe tathmini ya kina kabla ya kuingia mkataba.		ulioonyesha kama kulifanyika tathmini ya kina ya uwezo wa mzabuni kifedha, vifaa, wafanyakazi na rasilimali nyingine alizonazo
31.	**Usimamizi wa utendaji**	***Pendekezo la 18*** Kitengo cha Manunuzi wanapaswa kuweka mahitaji ya utendaji kwa watoa huduma.	Idara za usimamizi wa taka ngumu zinapaswa kuweka mahitaji ya utendaji kwa ajili ya watoa huduma. Mahitaji ya utendaji yanawekwa katika mikataba kwa watoa huduma.	***Imetekelezwa kikamilifu***
32.	**Utoaji taarifa**	***Pendekezo la 19*** Timu ya usimamizi wa taka ngumu ianzishe mfumo wa utoaji wa mrejesho kati yao wenyewe na watoa huduma ili kuziwezesha halmashauri kupata mrejesho na taarifa muhimu za kuaminika na kwa wakati.	Timu ya usimamizi wa taka ngumu imeanzisha Orodha ambayo itawezesha kuwajulisha halmashauri juu ya maendeleo ya shughuli za taka ngumu. Orodha imeandaliwa na kutumwa kwa Maafisa wa afya ili kufuatilia shughuli zinazo fanyika kwa watoa huduma katika halmashauri. Orodha inajumuisha yafuatayo jina la mtoa huduma, eneo la kufanyia kazi, uwajibikaji, hadhi, maoni na afisa wa afya na saini ya afisa wa afya na mtoa huduma.	***Imetekelezwa kikamilifu***

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
33.	**Ufutiliaji**	***Pendekezo la 20*** Kitengo cha usimamizi wa taka ngumu kinapaswa kuandaa mifumo ya ufuatiliaji wa ukiukwaji wa mikataba kwa watoa huduma.	Miji saba imekamilisha mchakato wa kuandaa mpango mkakati kwa usimamizi wa TSCP na halmashauri 18 zipo kwenye mchakato. Mipango mikakati kwa usimamizi wa shughuli za taka ngumu imeandaliwa na mikataba imetolewa kwa watoa huduma ambayo inaonyesha nini kifanyike na namna gani kifanyike.	*Imetekelezwa kwa kiasi* Hakuna mfumo mzuri wa kusimamia ukiukwaji wa mikataba ya taka ngumu Hata hivyo, Mipango Mkakati inaonyesha nini kifanyike na jinsi gani. Lakini Mipango ya kimkakati imeandaliwa kwa Halmashauri 26 kati ya 168. Hata hivyo shughuli za kuunga mkono miradi hii miwili si endelevu kwa sababu uendeshaji wake umepewa.
34.	**Mgawanyo wa majukumu**	***Pendekezo la 21*** **Mgawanyo wa uendeshaji na ufuatiliaji kazi** Idara ya afya wanapaswa kuhakikisha kuna mgawanyo wa kazi kati ya kazi za ufuatiliaji na shughuli ya utoaji wa huduma ndani ya Sehemu ya SWM.	Serikali za Mitaa zina idara tofauti kwa ajili ya usimamizi. Ufuatiliaji unafanyika na idara ya usimamizi na huduma zinatolewa na watoa huduma.	*Haijatekelezwa* Hakuna mgawanyo wa kazi ambazo zinahusisha utoaji wa huduma na ufuatiliaji.
35.	**Usimamizi wa kiutendaji**	***Pendekezo la 22*** Idara ya usimamizi wa taka	Serikali za mitaa zinatumia matokeo ya uchunguzi huu kwa mujibu wa	*Limetekelezwa kwa kiasi* Uchunguzi ulifanywa

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
		ngumu inaweza ikamuhusisha mtafiti ili aweze kutafiti uzalishaji wa taka ngumu kwa kila kata na kuandaa makadirio yatakayotumika kama sehemu ya tathmini ya ufanisi kwa watoa huduma.	uzalishaji wa taka, usafirishaji, kusindika na matumizi ya mara ya pili.	kuhusu utayari wa kulipa tozo kutoka kwa wananchi, kama njia mojawapo ya kuongeza mapato yatokanayo na taka ngumu. Matokeo yatatumika kukamilisha mipango mikakati ya usimamizi wa taka ngumu. Hata hivyo hakuna ushahidi uliotolewa kuhusu utafiti kufanyika kuhusiana na uzalishaji wa taka ngumu katika ngazi ya kata.
36.	ufuatiliaji	***Pendekezo la 23*** Idara ya usimamizi wa taka ngumu inapaswa kuhakikisha kuwa kila mtoa huduma ana mfumo imara usimamizi wa ubora na ufuatiliaji wa uhakika.	Serikali za Mitaa wanapaswa kununua huduma za wakandarasi wa shughuli za usimamizi wa taka ngumu wenye mpango mzuri wa usimamizi wa viwango na ufuatiliaji wa uhakika.	***Limetekelezwa kikamilifu*** Watoa huduma wanaingia mikataba ambayo tayari inakuwa na makubaliano ya wanachotakiwa kutekeleza, ubora na hatua za kuchukuliwa kama mkandarasi atashindwa kutoa huduma kama inavyotakiwa.
37	Mipango na	***Pendekezo la 24*** Mpango wa Ada ya taka		***Imetekelezwa kikamilifu***

S/N	Aina ya mapendekezo	Mapendekezo yaliyotolewa	Utekelezaji wake	Maoni ya NAOT
	Bajeti	**ngumu** Idara ya usimamizi wa taka ngumu inapaswa pamoja na idara ya uhasibu kutengeneza bajeti ya msingi ili kuamua gharama ya kukusanya taka ngumu katika manispaa. Hii ni pamoja na makadirio ya gharama kwa ajili ya asilimia mbalimbali za taka ngumu zilizokusanywa.	Kupitia mipango ya kimkakati , operesheni ya kuamua mchakato wa gharama iko katika mpango wa kila halmashauri.	Uchambuzi wa gharama umefanyika na umeweza kuwekwa katika Mipango mikakati ya usimamizi wa taka ngumu katika Serikali za Mitaa.
38	**Usimamizi wa mapato**	***Pendekezo la 25*** **Mgawanyo wa ukusanyaji wa ada za taka ngumu na utoaji wa huduma kazi** Jukumu la kukusanya ada za taka ngumu linapaswa kuwa ni jikumu la halmashauri na sio la mkandarasi. Idara ya uhasibu inatakiwa kuwajibika kukusanya ada za taka ngumu. Wakandarasi wanapaswa kulipwa ada na halmashauri kwa kusimamia shughuli za uzoaji taka. Ada inayokusanywa inaweza kulinganishwa na mambo mbali mbali kama vile eneo la ukusanyaji taka na kiwango cha taka ngumu kilichokusanywa. Mkandarasi anapaswa kuwajibika na swala la kukusanya taka ngumu tu na sio kutoza ada	Serikali za Mitaa kuchukua hatua juu ya usimamizi wa utaratibu huu mpya	*Haikutekelezwa* Mtoa ushauri anakusanya taarifa kuhusu mgawanyo huu wa majukumu kwa Wakandarasi kuwa wakusanyaji taka na watoa huduma na Halmashauri kuwa wakusanyaji wa tozo. Kufikia December 2014 majukumu yote bado yanatekelezwa na mkandarasi

Kiambatanisho cha tano: Hali ya utekelezaji wa Mapendekezo Ukaguzi wa Kifanisi Kuhusiana na Usimamizi wa Ujenzi wa Barabara Tanzania

S/N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
		Pendekezo 1.0: Uboreshaji wa Taasisi		
1	**Udhibiti wa ubora**	***Pendekezo** 1.1:* Kuunda tume kwa ajili ya kupitia uwezekano wa kuimarisha uadilifu, taaluma na ufanisi wa mipango mikakati ya Wizara ya Kazi na TANROADS ili kuweza kutathmini uwazi na uwajibikaj	Usimamizi wa mzunguko wa mradi kama vile kuandaa miongozo, nakala za manunuzi zenye ubora, usimamizi na miongozo ya udhibiti wa ubora ambayo kwa sasa ipo tayari ili kuweza kusaidia wafanyakazi wa TANROADS katika hatua zote za miradi. Uwezo wa kiufundi wa TANROADS pia umewezeshwa kwa kupitia programu mbalimbali za mafunzo na zile zinazotoa msaada wa kitaalamu. Pia TANROADS imeweza kuajiri wataalamu wawili wa usimamizi wa mikataba, mtaalamu mmoja wa mazingira na masuala ya jamii, mtaalamu wa manunuzi na mshauri wa usimamizi wa miradi ili kuweza kutoa msaada wa kitaalamu kwa wafanyakazi wa TANROADS. TANROADS imepeleka Wizara ya Kazi ombi lake la kutaka (i) Uhitaji wa wafanyakazi wenye taaluma (ii) Kuwezeshwa kifedha kwa shughuli zake hasa miradi ya uendelezaji wa bara bara nk. Yote haya yanalenga kuboresha ufanisi wa kiutendaji	*Limetekelezwa kikamilifu* Kuwepo kwa vitendea kazi kama vile miongozo ni kitu muhimu cha kuhamasisha utaalamu katika utendaji. Wataalamu walioajiriwa pia wanategemewa kuongeza hali ya viwango vya utaalamu kwa TANROADS katika shughuli za Ujenzi wa bara bara Kuanzishwa kwa makubaliano ya kiutendaji wa kifanisi kati ya wizara ya kazi na TANROADS kutasaidia kuhakikisha utekelezaji wa mipango mikakati na uwajibikaji. Kipengele cha uwazi kinatekelezwa kulingana na utekelezaji unaofanyika.

S/N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
			Wizara ya kazi inawezesha TANROADS kwa kuwapatia rasilimali kulingana na uwezo wa serikali Mamlaka pia inaandaa mpango wa kibiashara na kufanya makubaliano ya kiutendaji na na Wizara ya kazi na pia kutumia nyaraka hizo kufuatilia ufanisi wa kiutendaji wa mamlaka. Kwa sasa TANROADS inaandaa mchakato wa awali wa kibiashara ambao utaleta maboresho kwenye utekelezaji wa shughuli zake nakuufanya kuwa wa kifanisi. Kazi hii inafanywa na M/s Egis Bceom chini ya udhamini wa EU.	
2	**Ujengaji wa Uwezo**	***Pendekezo 1.2:*** Kuipatia TANROADS maelekezo sahihi ya nanma ya kuweza kuwasimamia wakandarasi	TANROADS imejumuisha vifungu kwenye nyaraka ya vigezo vya utendaji (COPA) ili kuhimiza uwajibikaji kwa wakandarasi. Hii inajumuisha kubadilika kwa muda wa kumjulisha mkandarasi kutoka miezi 12 mpaka miezi 72, adhabu kuhusiana na kubadilisha wafanyakazi kwa kupunguza posho kwa kila ubadilishwaji unaofanywa Pia TANROADS inafanya mafunzo ya muda mfupi na mrefu kama njia ya kujenga uwezo kwa wafanyakazi wake wa usimamizi wa miradi.	*Limetekelezwa kikamilifu* TANROADS imetekeleza hili pendekezo kwa kiasi kizuri. Mapitio yaliyofanywa kwenye nyaraka ya masharti ya kiutendaji (COPA) na vifungu vilivyoongezwa ili kuweza kuongeza wajibikaji imeweza kutekeleza pendekezo hili. Hatua zaidi zilizochukuliwa kuhusiana na mafunzo ya muda mfupi na mrefu yamesaidia pia kuongeza uwezo wa TANROADS kusimamia wakandarasi wake.

S/N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
		Pendekezo *2: Uandaaji wa Miradi na michoro*		
3	**Udhibiti wa ubora**	***Pendekezo 2.1:*** Katika nyakati zisizo maalum kufanya tathmini za ufanisi wa kazi sanifu za TANROADS na kuangalia ni namna gani TANROADS inafanya manunuzi, inatoa maelekezo na kusimamia wakandarasi wake wa Usanifu.	, Wizara ya Kazi inaendelea Kufanya kaguzi za kitaalamu kupitia ripoti za utekelezaji za robo mwaka na mwaka. PPRA inafanya pia ukaguzi wa Ufanisi Wizara ya Ujenzi na inafuatilia mfumo unaotumika katika kufanya manunuzi ya timu za kisanifu na za kufanya tafiti.	*Limetekelezwa kikamilifu* Ufuatiliaji wa mfumo wa manunuzi ya timu za utafiti na timu za ufanisi utasaidia kuahikisha ubora wa kazi za kisanifu
4	**Udhibiti wa ubora**	***Pendekezo 2.2:*** Kuipatia tume iliyoundwa awali maelekezo ya kutathmini namna nzuri ya kutekeleza majukumu yaliyoainishwa hapo juu kuhusiana na kazi za usanifu	TANROADS inahamasisha uwezo wa timu za kazi sanifu kupitia kozi zinazolenga masuala ya manunuzi. Wizara ya Ujenzi inatumia taasisi zake kama ERB na CRB ili kuhakikisha kuwa ni kampuni zilizo nzuri tu ndizo zinaruhusiwa kufanya kazi nchini	*Limetekelezwa kikamilifu* Uhamasishaji uliofanywa kwa timu zinazofanya kazi za usanifu utatatua tatizo la uwajibikaji kwenye manunuzi na usimamizi wa wakandarasi wa usanifu.
5	**Ujengaji wa uwezo**	***Pendekezo 2.3:*** Kwa kuzingatia kazi ya tume iliyopendekezwa, serikali iipatie TANROADS maelekezo sahihi kuhusiana na namna ya kuboresha kazi za kisanifu na kufanya mapitio ya kazi sanifu.	Wizara ya ujenzi inatumia taasisi zake kama ERB na CRB ili kuhakikisha kuwa ni makampuni yaliyo mazuri tu ndio zinaruhusiwa kufanya kazi nchini	*Limetekelezwa kikamilifu* Uhamasishaji uliofanywa kwa timu za sanifu utatatua tatizo la uwajibikaji kwenye manunuzi na usimamizi wa wakandarasi wa usanifu.
		Pendekezo 3: Usimamizi wa Miradi na udhibiti wa ubora		

S/N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
6	**Usimamizi wa Utendaji/kifanisi**	***Pendekezo 3.1:*** **Wizara ya Miundombinu na TANROADS zinahitaji kuboresha shughuli za mwanzo kama vile kukidhi vigezo vya mikopo na hatua za manunuzi**	**TANROADS imeboresha uwezo kwa wafanyakazi wake kwa kuandaa na kutoa mafunzo mbalimbali kwa wahandisi kuhusiana na manunuzi na usimamizi wa miradi. Kwa mfano, wahandisi wote wameweza kuhudhuria mafunzo kwa awamu zote za usimamizi wa mikataba ya FIDIC.** **Pia, uwezo umeweza kuboreshwa kwa kuanza kuchukua wataalamu wa muda mfupi kwenye usimamizi wa mikataba (2), Manunuzi(2), Mazingira na masuala ya kijamii (1), mtaalamu wa ushauri wa usimamizi wa miradi (1) kwa kutumia mifuko ya fedha za wafadhili.** **Aidha, serikali imeweza kufanya maongezi na wafadhili kuhusu kuondolewa vigezo hivyo kwenye mradi wa bara bara wa Arusha - Holili kwa awamu ya kwanza, wafadhili waliondoa vigezo hivyo.** **Ili kuboresha muda wa kuanza kwa miradi mikakati ifuatayo inatekelezwa;** ✓ **Ulipwaji wa fidia kwa watu wanoathirika na miradi (PAP) unafanywa kwa awamu kwa mujibu wa hali ngumu ya kifedha ya serikali. Hii inajumuisha**	***Limetekelezwa kikamilifu*** **Mafunzo yaliyotajwa yanategemea kuboresha hatua za manunuzi katika ofisi za TANROADS.** **Maboresho kwenye vigezo kwa awamu ya kwanza yanategemewa kuboresha hali ya TANROADS katika kutimiza masharti ya mikopo**

S/N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
			suala lakazi kuanza kwa awamu badala ya kusubiria fidia kwa mradi wote wa bara bara. Hii imefanyika kwa miradi ifuatayo inayofadhiliwa kwa pamoja na ADB/JICA na serikaliya Taanzania ambayo ni ; Iringa – Dodoma, Namtumbo – Songea, Dodoma – Babati, Tunduru – Mangaka – Mtambasuala na mradi wa bara bara unaohusisha nchi mbili za Afrika Mashariki unaoanzia Arusha – Namang hadi Athi river Kenya. ✓ Pia, TANROADS imeanza kuhamisha watu na kuwalipa fidia wale wote wanaoathirika na mradi kabla ya kusaini mikataba ya mradi, kwa mfano mradi wa Ujenzi wa barabara ya Morocco – Mwenge – Tegeta na Kamata – BenderaTatu na uboreshaji wa makutano ya TAZARA.	
7	**Utengaji wa bajeti**	***Pendekezo3.2:*** **TANROADS inahitaji kuwa na bajeti inayojumuisha mradi wote na pia kutumia mfumo wa udhibiti wa bajeti kwa kipindi chote cha mradi.**	Bajeti iliyopendekezwa na TANROADS imetumwa kwa wizara ya ujenzi ambayo imejumuisha matukio ya vikwazo mbalimbali na yasiyokuwa na vikwazo vya utekelezaji. Bajeti ya mwisho inategemea makisio ya jumla ya serikali.	*Halijatekelezwa* Wizara ya ujenzi/ TANROADS haijaweza kutekeleza pendekezo hili kwa sababu ya mambo mengine yanayoathiri ufanisi wa bajeti yao ambao uko nje ya uwezo wao.

S/N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
			Kutokana na ufinyu wa bajeti ya serikali utoaji wa fedha kwenda TANROADS bado unaathiri udhibiti wa bajeti ya miradi. Ufinyu wa bajeti ya serikali ikilinganishwa na ukomo wa bajeti unaofanywa na wizara ya fedha inazuia kujumuisha mahitaji ya kifedha kwa miradi yote. Uhaba huu wa fedha upo nje ya uwezo wa TANROADS na Wizara ya Ujenzi Udhibiti wa bajeti kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mradi inategemeana na mkataba wa mradi. Wateja wanashindwa kukudhi vigezo vya mikataba kutokana na mapungufu katika utoaji wa fedha iliyobajetiwa na serikali kama vile uchelewaji katika utoaji wa fedha na utoaji wa fedha usio wa ukakika.	Bajeti imeathiriwa kwa ucheleweshwaji wa utoaji fedha, kushindwa kikidhi vigezo vya mikataba na ukomo wa bajeti kwa Wizara ya Fedha.
8	**Mgawanyo wa majukumu**	***Pendekezo 3.3:*** Kwa kila mradi ni muhimu kuwa na majukumu na kazi vilivyoainishwa vizuri miongoni mwa wahusika mbalimbali, na hii inatakiwa ifanywe kwa kuzingatia muda, gharama na ubora. Pia tahadhari inatakiwa zichukuliwe ili kuhamasisha uwezo wa TANROADS katika kuainisha na kusimamia viatarishi.	Majukumu ya wadau mbali mbali wanaotekeleza miradi ya bara bara (wakandarasi, mwajiri na wahandisi) yameainishwa vizuri kulingana na mikataba. Kazi na majukumu ya mwajiriwa pia yameainishwa kwenye muongozo wa kazi zao. Maboresho yamefanyika kwenye nyaraka za mikataba ambapo vifungu vya adhabu kwa wakandarasi watakaoshindwa kutimiza majukumu yao kwa muda mfano kuchelewa katika	*Limetekelezwa kwa kiasi* Maboresho katika hadidu za rejea yatatekeleza suala la kazi na majukumu ya pande mbali mbali zinazohusika. Kwa sasa TANROADS imeanza kuboresha uainishaji wa vihatarishi baada ya kuanzisha mfumo wa uandikishaji wa usimamizi wa viatarishi ambao bado upo kwenye mchakato.

S/N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
			kuwasilisha ripoti na kubadilisha wafanyakazi nk.	
9	**Usimamizi wa utendaji/ufanisi**	***Pendekezo 3.4:*** Faili na nyaraka nyingine muhimu lazimai ziwepo katika mpangilio. Wizara ya Miundo Mbinu inapaswa kuanzisha mfumo wa uandikishaji ili kuweka kumbukumbu za ufanisi wa wakandarasi na washauri kwa kila mradi wa Ujenzi wa bara bara.	Ripoti za kiutendaji kwa wakandarasi zinatumwa ERB na CRB mara moja kwa mwaka. Wakandarasi ambao hawatakuwa wanafanya vizuri wanatolewa taarifa kwenda PPRA kwa ajili ya kuwaingiza kwenye daftari jeusi. Kwa sasa TANROAD inafanya mchakato wa awali wa kibiashara ambao utapendekeza njia sahihi ya kutunza kumbukumbu. Kwa sasa mafaili maalumu kwa kila mkataba yanatunzwa kwenye makabati maalumu yaliyo imara.	*Limetekelezwa kwa sehemu* Hakuna ushahidi kuwa huu mfumo wa uandikishaji umeanzishwa ili kuweza kuweka kumbu kumbu za ufanisi/utendaji wa wakandarasi.
10	**Utunzaji wa Nyaraka**	***Pendekezo 3.5:*** TANROADS inapaswa kuboresha eneo lake la kutunzia nyaraka.	TANROADS kwa sasa imeanza kutumia eneo jipya ambalo lina nafasi zaidi ya kutosheleza kutunzia nyaraka. Chumba maalumu chenye makabati yaliyo salama kimetengwa kwa ajili ya kutunzia nyaraka za manunuzi. Mpango kwa ajili ya jengo jipya la TANROADS upo njiani. Nafasi kubwa itatengwa kwa ajili ya eneo la utunzaji wa nyaraka. Kwa sasa TANROADS inafanya mchakato wa maandalizi ya awali wa kibiashara ambao utaelekeza njia sahihi ya kutunza nyaraka.	*Limetekelezwa kwa kiasi* TANROAD haijaweza kutekeleza hili pendekezo kama inavyotakiwa. Suala la kuwa na sehemu ya kutunzuia nyaraka halijatekelezwa kwani bado linasubiria mpaka watakapo hamia kwenye jengo jipya litakalo kuwa na nafasi. TANROADS kwa sasa imeanzisha mchakato wa kibiashara ambao utatekeleza namna sahihi ya utunzaji wa nyaraka. Mchakato huu bado

S/ N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
				unaendelea.
11	**Manunuzi/ Usimamizi wa Mikataba**	***Pendekezo3.6:*** Ilipendekezwa kuwa TANROADS ihakikishe inachukua wakandarasi kulingana na mahesabu ya gharama za mwisho za kumalizia miradi. Na mahitaji ya ubora wa barabara kwenye mikataba inapaswa kusema kabisa viwango ambavyo havihusishi hitaji la jumla ili kufanya marekebisho baada ya kumaliza. Aidha, mikataba inapaswa kujumuisha vifungu vya adhabu kwa wakandarasi ambao hawatasimamia vigezo vya mikataba kama vile muda, bajeti na ubora wa bara bara.	Manunuzi yanafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013. TANROADS inaendelea kurekebisha nyaraka za mikataba ili kupunguza athari za wakandarasi wasiotimiza wajibu wao. Kwa mfano inajumuisha; malipo ya awali kwa awamu kulingana na utendaji kazi, udhamini wa kibenki kutoka kwenye mabenki yaliyopo nje ya nchi inapaswa iwe na mabenki husika nchini, kujaribu ubora wa kazi unafanyika kwa kila hatua na kuwepo kwa wasimamizi wanavyofanya kazi kulingana na vifungu vilivyopo kwenye nyaraka ya mkataba.	*Limetekelezwa kwa kiasi* Hatua ambazo zimechukuliwa kwa kiasi fulani zinatekeleza pendekezo lilotolewa. Lakini hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa manunuzi ya wakandarasi yanafanyika kwa kuzingatia gharama za mwisho za mradi wa Ujenzi wa bara bara.
12	**Usimamizi wa mikataba**	***Pendekezo 3.7:*** Mikataba inapaswa kujumuisha adhabu husika kwa wakandarasi ambao hawatasimamia muda waliopewa kwenye mikataba, bajeti na ubora wa bara bara.	Nyaraka za mikataba imejumuisha vifungu maalumu vya adhabu ambavyo inawezesha wakandarasi wasiotekeleza majukumu yao kusimamishwa. Hili limeweza kutekelezwa kwa wakandarasi wawili wakubwa na mkandarasi mmoja kuanzia mwaka 2010 hadi sasa.	*Limetekelezwa kikamilifu*

S/N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
13	**Usimamizi wa mikataba**	***Pendekezo 3.8:*** **Pia ni muhimu kuwa TANROADS iweke kwa uwazi vigezo vya utozwaji wa kodi kwa wakandarasi kwenye mikataba.**	**Maboresho yaliyofanyika katika eneo hili ni pamoja na kuwashawishi wafadhili kukubali mikataba iliyosainiwa na gharama za kodi. Mradi wa idara ya usafirishaji na mradi wa pili wa njia ya kati unaofadhiliwa na Bank Kuu ya Tanzania unaruhusu fedha za mkopo kulipiwa kodi. Pia ADB imekubali jumla ya fedha za mkataba isainiwe kwa kujumuisha kodi ambayo inalipwa na serikali ya Tanzania. Hii imepunguza ucheleweshaji unaotokana na uandaaji wa misamaha ya odi**	***Limetekelezwa kikamilifu***
14	**Uratibu**	***Pendekezo 3.9:*** **TANROADS inapaswa kuchukua hatua za tahadhari ili kuweza kupunguza muda na ongezeko la gharama kwa kuongeza uratibu na makampuni ya Ujenzi.**	**TANROADS imeandaa muongozo kwa ajili ya usimamizi wa hifadhi za bara bara ambao umeanza kufanyiwa kazi mwezi Julai 2014** **Maneja wa mikoa wanatoa vibali kwa wamiliki wa makampuni ikiwemo mbao za matangazo na vigezo vya kuviondoa ambayo inapunguza athari ziliyobainika kipindi cha utekelezaji wa miradi ya bara bara.**	***Limetekelezwa kwa kiasi*** **Hatua zilizochukuliwa na TANROADS kwa kiasi kubwa zinaridhisha na limekidhi pendekezo lililotolewa** **Aidha, TANROADS haijaweza kufanya uratibu na makampuni ya maji, umeme na simu ili kuweza kukabiliana na tatizo la ucheleweshwaji wa miradi na ongezeko la gharama kutokana na uchelewaji katika kuhamisha miundo mbinu zao.**
15	**Udhibiti wa**	***Pendekezo 3.10:***		***Limetekelezwa kikamilifu***

S/N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
	ubora	**Maswala ya udhibiti wa ubora wakati wa usimamizi, ufatiliaji, ukaguzi na tathmini yanapaswa kuangalia suala la uchelewaji, ongezeko la gharama na tatizo la ubora**	**Maneja wa mikoa, wakandarasi wa miradi toka TANROADS na wafanyakazi wa Wizara ya Ujenzi wameshiriki mafunzo ya FIDIC yanayohusiana na usimamizi wa mikataba ili kuweza kuboresha kiwango chao cha elimu kuhusiana na mikataba.** **TANROADS imeajiri wataalamu wawili wa usimamizi wa mikataba na mtaalamu mmoja wa usimamizi wa miradi kwa ajili ya mafunzo ya ndani kwa wahandisi wa miradi kuhusiana na mfumo wa usimamizi wa miradi wa kielektinik.** **TANROADS kwa sasa inafanya utafiti kuhusiana na ufanisi wa barabara za lami na ufanisi kulingana na usanifu na vigezo vilivyofanyiwa maboresho. Utafiti unafanywa kwa pamoja baina ya TANROADS na kituo cha Utafiti wa Sayansi ya Viwanda (CSIR) kilichopo Afrika Kusini.**	**Hatua zilizochukuliwa na TANROADS zinaridhisha kutatua tatizo la udhibiti wa ubora.**
16	**Utumiaji wa rasilimali**	***Pendekezo 3.11:*** **TANROADS inapaswa kupunguza muda wa kutumia fomula ya mabadiliko ya bei kwa kugawanya miradi ya barabara kwa awamu zikiwa na vipindi vifupi vya tarehe za mwisho**	**Pendekezo hili halijafanyiwa kazi kwa sababu linaathari kwenye utekelezaji wa mradi kwa kuwa miradi mingi inabana uwezo wa TANROADS kusimamia na pia kiwango cha gharama kwa kila kilomita itaongezeka kwa miradi midogo kutokana na kuelemewa. Hivyo basi, TANROADS kila siku inazingatia ubora.** **Aidha, kifungu kinachohusiana na**	***Halijatekelezwa***

S/ N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
			suala la fomula ya mabadiliko ya bei halitekelezeki kwa mikataba yote iliyo na kipindi cha Ujenzi kisichozidi miezi 18.	
17	**Ufuatiliaji na tathmini**	***Pendekezo 3.12:*** Tathmini kwa miradi ya bara bara iliyokamilika inatakiwa itumike kupima na kuchambua matokeo yaliyofikiwa	Wizara ya ujenzi, TANROADS na Wizara ya Fedha kila moja ifanye ukaguzi wa ndani kwa mwaka kwa miradi inayoendelea. Aidha, TANROADS imeajiri mkandarasi wa kujitegemea kwa ajili ya ukaguzi wa kitaalamu kwa miradi iliyokamilika.	*Limetekelezwa kikamilifu* Hatua zilizochukuliwa na Wizara ya ujezi na TANROADS zinategemewa kuleta maboresho.
18	**Uandaaji wa mipango**	***Pendekezo 3.13:*** Uzoefu uliopatikana unapaswa kutumika ilikuwa na uandaaji mzuri wa mipango, kujifunza na kuongeza maboresho.	Changamoto zilizopatikana katika kukamilisha miradi ya barabara inatumika kwenye uandaaji wa mipango mingine ya miradi mipya.	*Limetekelezwa kikamilifu* Uzoefu uliopatikana kwenye miradi iliyokamilika inatumika wakati wa kuandaa mipango ya miradi mipya.
19	**Uwazi**	***Pendekezo 3.14:*** TANROADS inapaswa kuboresha uwazi wake kwa umma.	Zabuni zinawekwa wazi kwa wale wote wanaokidhi vigezo Mikataba yote iliyosainiwa inawekwa kwenye tovuti ya TANROADS,PPRA, magazeti na mbao za matangazo kwa mujibu wa Sheria ya Manunuziya mwaka 2011 Pia taarifa za kina kwa kila mradi zinawekwa kwenye mbao za matangazo ili umma uweze kuona.	*Limetekelezwa kikamilifu* Hatua zilizochukuliwa na TANROADS zinategemewa kuboresha suala la uwazi wa TANROADS kwa umma
20	**Udhibiti wa ubora**	***Pendekezo 3.15:*** Michoro ya Ujenzi kwa miradi ya barabara	Michoro ya Ujenzi kwa barabara zilizokamilika inaandaliwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya bara bara.	*Limetekelezwa kikamilifu* Hatua zilizopendekezwa na TANROADS zinatosha

S/N	Aina ya mapendekezo	Pendekezo Lililotolewa	Hali ya Utekelezaji	Maoni ya NAOT
		iliyokamilika inapaswa kuifadhiwa na kufuatiliwa kwa muda wote wa uwepo wa barabara ili kuwezesha ufanyikaji wa matengenezo na kuorodhesha kazi za matengenezo zilizofanyika.	Tafiti za kimahesabu na vigezo zinafanyika kwa mwaka kwa ajili ya kulipa kipaumbele suala la matengenezo. Hizi zitahifadhiwa vizuri katika sehemu ya kutunzia nyaraka kama ilivyoonyeshwa kwenye kipengele 3.5.	kutekeleza pendekezo lililotolewa.